

AMALI ZA MADINA

Kimeandikwa na:
Sayyid Jawad al-Husaini Aali Ali ash-Shahrudi

Kimetarjumiwa na:
Alhaji Hemedi Lubumba

Kimehaririwa na:
Ustadh Abdallah Mohamed

Na:
Al-Haj Ramadhani K. Shemahimbo

©Haki ya kunakili imehifadhiwa na:
AL-ITRAH FOUNDATION

ISBN: 978 - 9987 - 512 - 82 - 9

Kimeandikwa na:
Sayyid Jawad al-Husaini Aali Ali ash-Shahrudi

Kimetarjumiwa na:
Alhaji Hemedi Lubumba

Kimehaririwa na:
Ustadh Abdallah Mohamed

Na:
Al-Haj Ramadhani K. Shemahimbo

Kimepangwa katika Kompyuta na:
Al-Itrah Foundation

Toleo la kwanza: Septemba, 2013

Nakala: 1000

Kimetolewa na kuchapishwa na:

Alitrah Foundation
S.L.P. - 19701, Dar es Salaam, Tanzania
Simu: +255 22 2110640 / 2127555
Barua Pepe: alitrah@yahoo.com
Tovuti: www.ibn-tv-com
Katika mtandao: w.w.w.alitrah.info

ترجمة

أداب الحرمين

أعمال المدينة

التأليف

السيد جواد الحسيني آل علي الشهردي

من اللغة العربية الى اللغة

السواحلية

YALIYOMO

Dibaji.....11

Faslu Ya Kwanza

Adabu Za Safari13

Faslu Ya Pili

Adabu Za Ziara19

Faslu Ya Tatu

Katika Kumzuru Mtume (S.A.W.W.)22

Ziyara Ya Kwanza:25

Ziyara Ya Pili:.....30

Ziyara Ya Tatu:33

Ziyara Ya Nne:.....42

Dua Isomwayo Katika Kitalu Kitukufu:44

Kusali Kwenye Nguzo Ya Abu Lubabah:.....48

Baada Ya Kusali Katika Nguzo Hii, Utasoma Dua Hii:49

Swaumu Ya Sunna Ya Huko Madina:51

Kusali Eneo Alilokuwa Akisimama Jibril (Maqam Jibril):52

Dua Ya Eneo Alilokuwa Akisimama Jibril (*Maqam Jibril*) Na
Hasa Kwa Mwenye Hedhi Aombe Ili Apate Tohara:57

Faslu Ya Nne

Fadhila Za Kumzuru Zahra (A.S.)60

Ziyara Ya Kwanza:61

Ziyara Ya Pili:.....	69
----------------------	----

Faslu Ya Tano

Kuwazuru Maimamu (A.S.) Huko Baqii	72
Sehemu Za Kuzuru Na Maeneo Matakatiifu Huko Baqii:	73
Aina Ya Kwanza Ya Kuomba Idhini Kwa Ajili Ya Ziyara:	74
Aina Ya Pili Ya Kuomba Idhini Kwa Ajili Ya Ziyara:.....	77
Ziyara Ya Kwanza Ya Maimamu Wa Huko Baqii:	79
Ziyara Ya Pili Ya Maimamu Wa Huko Baqii:.....	83
Kuwasalia Maimamu Hasan Na Husein (A.S.):.....	86
Kumsalia Imamu Zainul-Abidina (A.S.):.....	90
Kumsalia Imamu Muhammad Al-Baqir (A.S.):.....	91
Kumsalia Imamu Ja'far As-Sadiq (A.S.):	92
Namna Ya Kumzuru Sayyida Fatima Binti Asadi, Mama Mzazi Wa Amirul-Muuminina Ali (A.S.):.....	93
Namna Ya Kumzuru Ibrahim Mtoto Wa Mtume Wa Mwenyezi Mungu (S.A.W.W.):.....	97
Namna Ya Kuwazuru Mabinti Wa Mtume Wa Mwenyezi Mungu (S.A.W.W.):.....	102
Namna Ya Kuwazuru Shangazi Wawili Wa Mtume: Swafiyah Na Atiqah:	104
Namna Ya Kumzuru Bibi Fatima Ummul-Banina Mama Mzazi Wa Abul-Fadhli Abbas:	104
Namna Ya Kumzuru Bwana Wetu Aqil Nabwana Wetu Abdullah Bin Ja'far Tayyar (A.S.):.....	105
Namna Ya Kuwazuru Wahanga:.....	107
Namna Ya Kumzuru Bibi Halima Sa'diyya Aliyemnyonyesha Mtume Wa Mwenyezi Mungu (S.A.W.W.):.....	107
Namna Ya Kuwazuru Walio Makaburini:	108

Namna Ya Kumzuru Bwana Wetu Ismail Mtoto Wa Imam Ja'far As-Sadiq (A.S.):.....	110
Namna Ya Kumzuru Bwana Wetu Abdullah Bin Abdul-Muttalib Baba Mzazi Wa Mtume Wa Mwenyezi Mungu (S.A.W.W.): .	111
Ziyara Ya Pili:.....	113
Namna Ya Kumuaga Mtume (S.A.W.W.):.....	115
Ziyara Ya Kuwaaga Maimamu Huko Baqii:	119
Namna Ya Kuwazuru Maasumina Kumi Na Wanne Katika Siku Saba Za Juma	120
Ziyara Ya Mtume Wa Mwenyezi Mungu Siku Ya Jumamosi:	120
Ziyara Ya Amirul-Muuminina Siku Ya Jumapili:	124
Ziyara Ya Zahra (A.S.):	126
Ziyara Ya Imam Hasan (A.S.) Siku Ya Jumatatu:	127
Ziyara Ya Imam Husain (A.S.) Siku Ya Jumatatu:.....	129
Ziyara Ya Imam Zainul-Abidina, Imam Muhammad Al-Baqir Na Imam Ja'far As-Sadiq (A.S.) Siku Ya Jumanne:.....	131
Ziyara Ya Imam Musa Al-Kadhim, Imam Ali Ridha, Imam Muhammad Jawwad Na Imam Ali Al-Hadi (A.S.) Siku Ya Jumatano:	133
Ziyara Ya Imam Hasan Al-Askari (A.S.) Siku Ya Alhamisi:..	135
Ziyara Ya Imamu Wa Zama Hizi (A.S.) Siku Ya Ijumaa:	136
Namna Ya Kuwazuru Maasumina Kumi Na Nne (A) Kwa Mbali:.....	138
Dua Baada Ya Ziyara:.....	141
Dua Ya Kumwomba Hujjah (A.S.):	145
Sala Ya Ja'far Tayyar:.....	146
Faslu Ya Ya Sita	
Kumzuru Bwana Wetu Hamza	151

Utasema Katika Kumzuru Hamza Bwana Wa Wahanga (R.A.):	151
Namna Ya Kuwazuru Wahanga Huko Uhud:	157
Namna Ya Kumzuru Abu Dharr Al-Ghaffariy:	160
Fadhila Za Kumzuru Hamza Bwana Wa Wahanga, Na Wahanga Wengine Huko Uhud	163

Faslu Ya Saba

Inahusu Misikiti Na Maeneo Yaliyobarikiwa Huko Madina Na Pembezoni Mwake	164
Kwanza: Msikiti Wa Mtume (S.A.W.W.):	164
Pili: Msikiti Wa Quba:	166
Tatu: Chumba Cha Mama Yake Ibrahim:	168
Nne: Msikiti Wa Al-Fadhikhu:	168
Tano: Msikiti Wa Fat'hu:.....	170
Sita: Msikiti Wa Ali, Msikiti Wa Fatima Zahrau (A.S.), Na Msikiti Wa Salman (R.A.):	171
Saba: Nyumba Ya Imam Zainul-Abidin, Imam Ja'far As-Sadiq (A.S.) Na Msikiti Wa Mubahala (Maapizano):.....	171
Nane: Msikiti Wa Kibla Mbili (<i>Qiblatayn</i>):.....	172
Tisa: Misikiti Iliyomo Ndani Ya Mji Wa Madina:	174

Faslu Ya Nane

Yahusu Kuwazuru Wahanga Wa Badri (R.A.).....	175
--	-----

NENO LA MCHAPISHAJI

Kitabu kilichoko mikononi mwako ni tarjuma ya kitabu cha Kiarabu kiitwacho *Adabu 'l-Haramain* kilichoandikwa na Sayyid Jawad al-Husaini Aali Ali ash-Shahrudi. Sisi tumekiita, *Amali za Madina*.

Kitabu hiki kinaelezea mambo ya kuzingatiwa kuanzia wakati mtu anapoanza safari kwa ajili ya kufanya ziara (ziyara) katika mji mtukufu wa Madina (yaani Adabu za Ziara).

Kila safari ina taratibu zake na madhumuni yake. Kwa hiyo, msafiri hutakiwa kuzingatia utaratibu wa safari hiyo ili kufanikisha madhumuni yake. Safari ya Ziara ina utaratibu na kanuni zake zilizowekwa kisheria, hivyo, mtu anapokwenda mji wowote mtukufu kwa ajili ya Ziara lazima ayazingatie hayo ili afanikishe madhumuni ya safari yake hiyo muhimu.

Katika kitabu hiki mwandishi ameelezea kwa lugha fasaha hatua kwa hatua kuanzia mtu kuondoka kwenda kufanya ziara katika mji mtukufu wa Madina mpaka anapomaliza ziara yake na kurudi nyumbani. Mwandishi ameshughulikia kwa kina adabu na amali za kufanya kwa mwenye kufanya ziara Madina tukufu. Hata hivyo, ni matarajio yetu kwamba ataendelea kutufahamisha kuhusu adabu na amali za kufanya katika miji mingine mitukufu insha'Allah.

Kutokana na ukweli huo, Taasisi yetu ya Al-Itrah Foundation imeamua kukichapisha kitabu hiki kwa lugha ya Kiswahili kwa madhumuni yake yaleyale ya

kuwahudumia Waislamu, hususan wazungumzaji wa Kiswahili.

Tunamshukuru ndugu yetu Alhaj Hemedi Lubumba kwa kukubali jukumu hili la kukifanyia tarjuma kitabu hiki. Vilevile tunawashukuru wale wote walioshiriki kwa njia moja au nyingine hadi kufanikisha kuchapishwa kwake.

Ni matumaini yetu kwamba kitabu hiki kitakuwa ni chenye manufaa sana kwa wale wote wanaokusudia kufanya ziara kwa sasa na baadaye insha'Allah.

Mchapishaji:
Al-Itrah Foundation

DIBAJI

Hijja ni fursa ya Ummah wa Kiislamu kufikia hali ya Kiibrahim katika sekta ya kisiasa, kijamii, kitamaduni na kiroho. Mwenyezi Mungu amesema: **“Hakika Nyumba ya kwanza waliyowekewa watu ni ile iliyoko Makka yenye kubarikiwa na mwongozo kwa walimwengu.”** (Sura Aali Imran: 96).

Watu wamezoea zaidi kutimiza Hijja yao kwa mwonekano wa nje katika siku za mkutano huu wa kimungu ambao huwaleta pamoja waislamu toka pande zote za dunia bila kujali rangi zao, makabila wala mataifa na tamaduni za asili. Kwa kuwa Hijja ni mkusanyiko wa kiroho wenye kulenga kuchanua na kustawi katika nyanja zote za maisha ya mwanadamu, ni vizuri mahujaji wetu wakaelewa kwamba ibada hii ni kama ibada nyingine katika kuilea jamii katika sekta zote za maisha ya kisiasa, kitamaduni na kijamii, na hivyo ni lazima tuitumie fursa hii kama Bunge la Waislamu la Kimataifa na Baraza kuu la Waislamu duniani kupanga mikakati yao ya kiroho, kisiasa, kiuchumi, kijamii na kiutamaduni, ili kwamba lengo la Ibrahim (a.s.) lidhihirike ndani ya maisha yetu ya kila siku.

Ni juu ya Waislamu ambao hubeba ujumbe wa Mungu Mwenyezi, kufaidika kisiasa na kijamii na maudhui ya Hijja, na kamwe wasiridhike na mwonekano wa nje. Lakini ni lazima watambue kwamba ibada ya kisiasa na kijamii ya Hijja inaweza kupatikana iwapo tu tutatimiza na kufikia ibada ya kimaadili na kiroho.

Mji wa jihadi ya Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) ni kituo muhimu ambacho yapaswa kuheshimiwa kwa mahujaji kukipa kipaumbele. Makka na eneo la makaburi matukufu ni kioo cha msingi wa matukio makubwa ya

harakati za Manabii, Uislamu na ujumbe wa Mtume Muhammad (s.a.w.w.), nalo ni eneo ambalo walifika hapo Manabii wa Mwenyezi Mungu na Jibril. Sehemu hii inatukumbusha matatizo na mazito aliyovumilia Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) katika njia ya kuusimamisha Uislamu na kuulea ubinadamu kwa muda mfupi wenye mafanikio makubwa. Hakika uwepo wa mahujaji kwenye makaburi matukufu na maeneo matakatifu ukichukuliwa kwa mazingatio, unaonyesha wajibu mkubwa walionao katika kulinda mafanikio makubwa ya Uislamu, kwani ni mara ngapi Mtume (s.a.w.w.) kavumilia machungu na matatizo mazito kwa ajili ya haki na ni mara ngapi Maimam (a.s.) waliteseka kwa ugeni, kiu na njaa kwa ajili ya kuondoa batili.

Hakika walisimama kidete na imara wala hawakuyumbishwa na tuhuma na vitimbi vya watu mfano wa Abu Jahli, Abu Lahabi, Abu Sufyan, Muawiya na hata Yazid. Wakati wakipambana na ushetani huu na vitimbi vyao ni wakati huohuo waliendelea na harakati zao katika kuinua na kustawisha roho zao kwa Sala, Saumu, Zaka, sadaka, dua na tabia njema, yaani kwa ibada zote, ili kwamba ibada hizo zidhihiri katika ustawi wa uchumi wao, elimu zao, sayansi yao, teknolojia zao, utabibu wao, viwanda vyao, kilimo chao, ufugaji wao, utamaduni wao, idara zao, dola yao, uongozi wao, utawala wao, ulinzi wao, jamii zao na sekta zao zote za maisha yao, hivyo ni wajibu juu ya mahujaji kutambua falsafa ya Hijja na malengo yake ya kiroho, kisiasa, kiuchumi, kijamii na kiutamaduni ili kwamba iwe ni Hijja halisi ya Ibrahimu na si Hijja ya utalii na kumbukumbu.

Alhaji Hemedi Lubumba.

FASLU YA KWANZA

ADABU ZA SAFARI

Dua na adabu za safari ni nyingi, nasi hapa tutataja baadhi tu kati ya hizo:

1. Istikhara: Miongoni mwa adabu za safari na mambo yaliyo mustahabu kwa ajili ya safari sawa iwe ni ya Hijja au nyingineyo, ni kufanya Istikhara, na makusudio ya Istikhara ni dua na kuomba kheri kutoka kwa Mwenyezi Mungu katika kutenda jambo lolote na hasa Hijja.

Imepokewa kutoka kwa Imam al-Baqir (a.s.) kwamba alisema: “Hakika Ali bin Husein (a.s.) alikuwa akiifanya anaponuwia kwenda Hijja au Umra, au kuuza au kununua au kumwacha huru mtumwa.” Na katika riwaya zetu nyingi kuna katazo la kutenda amali yoyote bila kufanya Istikhara.

Sura nzuri ya Istikhara ni aseme:

أَسْتَخِيرُ اللَّهَ بِرَحْمَتِهِ خَيْرَةً فِي عَافِيَةٍ

“Namuomba Mwenyezi Mungu kheri kupitia rehema Zake katika lile lenye afya.”

Aseme hivyo mara tatu au saba au kumi au hamsini au sabini au mara mia moja. Mara zote hizo zimepokewa ndani ya Hadithi, kisha baada ya dua hii aendelee na amali yake au safari yake.

2. Kuchagua wakati: Imepokewa kutoka kwa Imam as-Sadiq (a.s.) kwamba alisema: “Anayetaka kusafiri basi

safari yake iwe ni siku ya jumamosi, kwani lau jiwe litadondoka toka mlimani siku ya Jumamosi basi Mwenyezi Mungu atalirudisha sehemu yake. Au siku ya Jumanne, kwani ndiyo siku ambayo Mwenyezi Mungu aliyayusha chuma kwa ajili ya Daud (a.s.). Au siku ya Alhamisi, kwani Mtume (s.a.w.w.) na masahaba zake walikuwa wakipigana ndani ya siku hii na wakishinda.”

Kuna riwaya zimepatikana zikikataza kusafiri siku ya Jumatatu, kwani ndio siku ambayo humo alifariki Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) na Wahyi ukakoma. Na ndio siku aliyouawa Husain (a.s.). Na imekatazwa kusafiri siku ya Jumatano, kwani ndio siku ambayo humo ziliumbwa nguzo za moto na kuangamizwa Ummah zilizotangulia. Na imekatazwa kusafiri siku ya Ijumaa kabla ya Sala. Na pia imekatazwa kusafiri siku ya tatu, ya nne, naya tano ya mwezi mwandamo.

3. Kutoa sadaka: Ni mustahabu kutoa sadaka kwa ajili ya safari. Na asome dua hii wakati wa kutoa sadaka hiyo:

اللهم انى اشتريت بهذه الصدقة سلامتى و سلامة سفرى و ما
معى. اللهم واحفظنى واحفظ ما معى و سلّمنى و سلّم ما معى
و بلّغنى و بلّغ ما معى ببلاغك الحسن الجميل.

“Ewe Mwenyezi Mungu! Hakika mimi kupitia sadaka hii nimenunua usalama wangu na usalama wa safari yangu na wa vile vilivyo pamoja nami. Ewe Mwenyezi Mungu! Nihifadhi na vihifadhi vile vilivyo pamoja nami, nisalimisha na visalimisha vile vilivyo pamoja nami, na

kwa mafikio yako mema na mazuri nifikishe mimi pamoja na vifikishe vile vilivyo pamoja nami.”

4. Wosia: Ni Sunna kukabidhi Wosia wakati wa kutoka, na hasa unaohusu haki za wajibu na za kidini.

5. Kuaga: Atakaponuia kutoka asali raka mbili au nne, kisha awaage wanafamilia yake na awaweke amana kwa Mola wake Mlezi, na amfanye Mwenyezi Mungu kuwa mrithi wake juu yao, aseme:

اللهمَّ إِنِّي أَسْتُوْدَعُكَ نَفْسِي وَأَهْلِي وَمَالِي وَذُرِّيَّتِي وَدُنْيَايَ
وَأَخْرَاقِي وَأَمَانَتِي وَخَاتَمَةَ عَمَلِي

“Ewe Mwenyezi Mungu! Hakika mimi naiweka Kwako kama amana nafsi yangu, ndugu zangu, mali yangu, kizazi changu, dunia yangu, akhera yangu, amani yangu na hatima ya amali yangu.”

Imepokewa kutoka kwa as-Sadiq (a.s.) kwamba alisema: “Mtu hawezi kuacha usimamizi bora kwa ajili ya familia yake kushinda huo, na hakuna mtu aliyeuacha kupitia dua hiyo ila Mwenyezi Mungu alimpa alichooomba.”

6. Awajulishe ndugu zake: Imepokewa kutoka kwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) kwamba alisema: “Ni haki juu ya mwislamu atakapokusafiri awajulishe ndugu zake, na ni haki juu ya ndugu zake atakaporejea waende kumlaki.”

7. Ni Sunna kusoma dua na Sura zilizofundishwa na Ahlul-Baiti, awekapo tu mguu katika kipando aseme:

سبحان الذي سخر لنا هذا وما كنا له مقرنين.

“Ametakasika Yeye aliyetutiishia haya na tusingeliweza kutenda haya wenyewe.”

Kisha aseme mara saba:

سبحان الله والحمد لله ولا إله إلا الله

“Ametakasika Mwenyezi Mungu, na kila sifa njema ni ya Mwenyezi Mungu, na hapana mungu ila Mwenyezi Mungu.”

Na dua nyinginezo miongoni mwa zile zilizofundishwa na Ahlul-Baiti.

8. Kuwasaidia wasafiri wenzake: Awasaidie wasafiri wenzake na awatangulie katika kutekeleza haja kwa kadiri awezavyo, na wala asipuuze kujitolea kwa juhudi zake katika kuwakidhia haja zao ili Mwenyezi Mungu amwondolee matatizo yake na amwepushe hapa duniani na huzuni na shida, na ili amwondolee shida adhimu siku ya Kiyama. Na imekuja katika hadithi kwamba: “Ndugu mbaya mno safarini ni yule ambaye ana uwezo wa kuwasaidia wengine lakini hawasaidii na bado anasubiri wengine wamsaidie.” Na kuna msisitizo wa kwamba awe mvumilivu kwa ndugu zake na awe na maadili mema kwao.

9. Atekeleze Sala ndani ya wakati wake: Azingatie safarini kutekeleza Sala za wajibu mwanzo wa wakati, na

iwapo sehemu na mazingira vitamlazimu kuwafuata Masunni katika Sala basi asipuuzie kufanya hivyo.

Inapasa kwa mwenye kwenda Hijja anapokuwa anakwenda Hijja nia yake iwe ni kwa ajili ya Mwenyezi Mungu tu, kiasi kwamba asiichanganye na malengo mengine ya kidunia, na wala sababu ya kwenda Hijja isiwe ila ni kutekeleza amri ya Mwenyezi Mungu, kupata thawabu Zake na kujiokoa na moto Wake. Ajihadhari sana kwamba asiwe na sababu nyingine ya siri moyoni mwake, kama vile kujionyesha kwa watu, kujihadhari na tuhuma za watu na kushutumwa kwa uovu iwapo hatakwenda Hijja, au kuhofia ufakiri na mali kuharibika iwapo hatokwenda Hijja, kama ilivyo mashuhuri kwamba mwenye kuacha kwenda Hijja atapata balaa la ufakiri na kurudi nyuma kiuchumi, au awe amekusudia kufanya biashara au shughuli nyingine. Hayo yote hukitoa kitendo katika wigo wa ikhlasi na hukizuia kutoa faida na kupata thawabu zilizoahidiwa kwacho.

Ni ujinga ulioje! Kuvumilia matendo mazito ambayo kwayo unaweza kupata mafanikio mema kwa ajili ya ndoto zisizo na faida ambazo hazisababishi chochote ila hasara. Hivyo ajitolee juhudi zake zote kwa kuifanya azma yake iwe ni kwa ajili ya Mwenyezi Mungu tu, iliyo mbali na kila aina ya kujionyesha kwa watu na kutaka kusifiwa. Na awe na yakini kwamba kusudio lake na amali yake havitokubaliwa ila iwapo tu ni mwenye ikhlasi, na kwamba uchafu mbaya mno ni kuiendea Nyumba ya Mfalme (Allah) na eneo lake tukufu ilihali anayekusudiwa ni mwingine (si Allah). Aisahihisha azma yake nafsini mwake, na kuisahihisha ni kuwa na ikhlasi kwa kujiepusha na kila aina ya kujionyesha na kutaka kusifiwa.

Atubie kwa Mwenyezi Mungu kwa toba halisi, na aadhimishe ndani ya nafsi yake hadhi ya Nyumba na hadhi ya Mola Mlezi wa Nyumba. Aiepushe nafsi yake na kila chenye kuushughulisha moyo wake, mpaka iwe hamu yake ni Mwenyezi Mungu tu, na moyo uwe umetulia umejielekeza kwa Mwenyezi Mungu na ukiadhimisha alama zake.

Masurufu yake yawe ni ya halali na awasaidie wengine masurufu hayo kwa moyo mkunjufu, asinung'unike kwa kutoa na kuwapa wengine, bali nafsi yake iwe radhi kwa hilo, kwani kutoa mali kwa ajili ya Hijja ni kutoa mali katika njia ya Mwenyezi Mungu, na dirhamu moja atoayo hapo ni sawa na kutoa dirhamu mia saba.

Awe na maadili mema na maneno mazuri, akithirishe unyenyekevu na ajiepushe na maadili mabaya na maneno machafu. Awe aliye rafurafu asiyejipamba, na asiwe ni mwenye kuelemea kwenye mambo yanayopelekea ufahari na kujilimbikizia mali ili asije kuandikwa katika orodha ya wenye kiburi na kutolewa kwenye kundi la wanyonge masikini.

FASLU YA PILI

ADABU ZA ZIARA

Adabu zinazopasa kutekelezwa maeneo matakatifu na kwenye makaburi matukufu ni nyingi mno, nasi hapa tutataja baadhi tu, nazo ni:

1. Kuoga unapokusudia kwenda kumzuru Mtume (s.a.w.w.) na Maimam (a.s.).
2. Kuwa katika hali ya tohara dhidi ya najisi, hadathi ndogo na hadathi kubwa.
3. Avae nguo yenye tohara na safi, na ni Sunna kwamba iwe mpya na nyeupe.
4. Atembee kwa hatua fupi fupi aelekeapo kwenye eneo tukufu, atembee kwa utulivu na unyenyekevu na hali ni mwenye hofu na aliyeinamisha kichwa chini na bila kugeuka huku na huku.
5. Asijinukize manukato ila tu aendapo kulizuru kaburi la Husain.
6. Aendapo kufanya Ziara aushughulishe ulimi wake kwa Takbira, Tasbihi, Tahlili, Tamjidi na kumsalia Mtume na aali zake.
7. Asimame kwenye mlango wa kuingilia eneo takatifu na aanze kuomba idhini ya kuingia kupitia mafundisho yaliyofundishwa na Ahlul-Baiti. Ajitahidi kuleta hali ya unyenyekevu na kuishiwa nguvu, ajiweke kama mtu aliye mbele ya hadhara ya mheshimiwa, na kwamba (huyo mheshimiwa)

anamuona, anasikia maneno yake na anamjibu salamu yake, kama zithibitishavyo hilo Ziyara¹ mbalimbali zilizofunzwa na Ahlul-Baiti. Atafakari huruma yao na mapenzi yao kwa wafuasi wao na kwa wale wenye kuwazuru. Atafakari kuhusu uharibifu wa nafsi yake, kuwatenga kwake, kukataa kwake mafunzo yao mengi na yale maudhi aliyowatendea wao, wafuasi wao na vipenzi vyao. Akijitazama mwenyewe mtazamo wa kutafakari na umakini basi nyayo zake zitashindwa kutembea, moyo wake utapatwa na hofu na hatimaye macho yake yatatokwa na machozi. Na huu ndio moyo hasa wa adabu zote za Ziara.

Na Ziara muhimu kushinda zote ni kumzuru Mtume (s.a.w.w.) na hasa kwa mahujaji, na kuna hadithi nyingi zikihimiza hilo, na hapa tutatosheka na hadithi moja. Imepokewa katika kitabu *al-Wasa'il* kutoka kwa Abu Abdillah (a.s.) kwamba alisema: “Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) alisema: 'Atakayekuja Makka kwa ajili ya Hijja na akawa hakunizuru mimi huko Madina, nitamnyanyapaa Siku ya Kiyama. Na atakayekuja kunizuru basi atawajibikiwa kupata Shufaa yangu, na atakayewajibikiwa kupata Shufaa yangu atawajibikiwa kuingia peponi. Na atakayekufa na hali akiwa katika hali ya kuhamia kwa Mwenyezi Mungu atafufuliwa Siku ya Kiyama pamoja na watu wa Badri.’”

¹ Haya ni maneno anayotamka au kuyasoma yule mwenye kufanya Ziara. Ama neno Ziara lenyewe linamaanisha shughuli nzima ya kumzuru marehemu, kama inavyosema Kamusi ya Kiswahili Sanifu, toleo la pili la Oxford University: “Ziara: 1- Ni tendo la kwenda mahala patakatifu kufanya kisomo au tendo maalumu la kidini. 2- Kaburi.” – Mtarjumu.

Mwenyezi Mungu anasema: **“Na bila shaka una tabia njema, tukufu.”** (Sura al-Qalami: 4).

Na Mwenyezi Mungu anasema: **“Bila shaka amekufikieni Mtume kutoka miongoni mwenu, yanamhuzunisha yanayokutaabisheni, anakuhangaikieni, kwa Waumini ni Mpole, Mwenye kurehemu.”** (Sura Tawba: 128).

FASLU YA TATU

KATIKA KUMZURU MTUME (S.A.W.W.)

Al-Kaf'amiy amesema: “Utakapotaka kuingia msikiti wa Mtume (s.a.w.w.) au moja ya maeneo matakatifu ya makaburi ya mmoja miongoni mwa Maimam, simama mlangoni na sema:

اللَّهُمَّ إِنِّي وَقَفْتُ عَلَى بَابٍ مِنْ أَبْوَابِ بُيُوتِ نَبِيِّكَ صَلَوَاتِكَ
عَلَيْهِ وَآلِهِ، وَقَدْ مَنَعَتِ النَّاسَ أَنْ يَدْخُلُوا إِلَّا بِإِذْنِهِ، فَقُلْتُ يَا
أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا لَا تَدْخُلُوا بُيُوتَ النَّبِيِّ إِلَّا أَنْ يُؤْذَنَ لَكُمْ، اللَّهُمَّ
إِنِّي أَعْتَقِدُ حُرْمَةَ صَاحِبِ هَذَا الْمَشْهَدِ الشَّرِيفِ فِي غَيْبَتِهِ كَمَا
أَعْتَقِدُهَا فِي حَضْرَتِهِ، وَأَعْلَمُ أَنَّ رَسُولَكَ وَخُلَفَاءَكَ عَلَيْهِمُ
السَّلَامُ أَحْيَاءٌ عِنْدَكَ يُرْزَقُونَ، يَرُونَ مَقَامِي، وَيَسْمَعُونَ كَلَامِي،
وَيَرُدُّونَ سَلَامِي، وَأَنَّكَ حَجَبْتَ عَنِّي سَعْيَ كَلَامِهِمْ، وَفَتَحْتَ بَابَ
فَهْمِي بِلَدْنِيذِ مُنَاجَاتِهِمْ، وَإِنِّي أَسْتَأْذِنُكَ يَا رَبِّ أَوَّلًا وَأَسْتَأْذِنُ
رَسُولَكَ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ ثَانِيًا، وَأَسْتَأْذِنُ خَلِيفَتَكَ الْإِمَامَ
الْبَقْرُوضَ عَلِيَّ طَاعَتُهُ الْحِجَّةُ ابْنِ الْحَسَنِ الْبَهْدِيِّ عَلَيْهِ

السلام. وَالْمَلَائِكَةُ الْمُؤَكِّدِينَ بِهَذِهِ الْبُقْعَةِ الْمُبَارَكَةِ ثَالِثًا،
 أَدْخُلْ يَا رَسُولَ اللَّهِ، أَدْخُلْ يَا حُجَّةَ اللَّهِ أَدْخُلْ يَا مَلَائِكَةَ اللَّهِ
 الْمُتَقَرَّبِينَ الْمُتَقَبِّبِينَ فِي هَذَا الشُّهْدِ، فَأَذِّنْ لِي يَا مَوْلَايَ فِي
 الدُّخُولِ أَفْضَلَ مَا أَدْنَتْ لِأَحَدٍ مِنْ أَوْلِيَائِكَ، فَإِنْ لَمْ أَكُنْ أَهْلًا
 لِنَدِيكَ فَانْتِ أَهْلٌ لِنَدِيكَ.

“Ewe Mwenyezi Mungu! Hakika mimi nimesimama mlangoni miongoni mwa milango ya nyumba za Nabii Wako sala na salamu ziwe juu yake na juu ya aali zake, na bila shaka umewakataza watu kuingia isipokuwa kwa idhini yake, ukasema: **“Enyi mlioamini! Msiingie nyumba za Nabii ila mtakapopewa idhini.”** Ewe mwenyezi Mungu! Hakika mimi naitakidi utukufu wa mwenye kaburi hili tukufu wakati wa ghaiba yake, kama ninavyoitakidi utukufu huo wakati wa hadhira yake. Na ninajua vilivyo kwamba Mtume Wako na Makhalifa Wako (a.s.) wangali hai, wako kwako wanaruzukiwa, wanaona kisimamo changu, wanasikia maneno yangu na wananjibu salamu yangu. Na hakika Wewe umezuia nisisikie maneno yao na umefungua mlango wa fahamu yangu kupitia utamu wa *munajati* wao. Na hakika mimi kwanza nakuomba idhini ewe Mola Mlezi na pili namuomba idhini Mtume Wako (s.a.w.w.), na ninamuomba idhini Khalifa Wako, Imam ambaye nimefaradhishiwa kumtii al-Hujja ibnu Hasan al-Mahdi amani iwe juu yake. Na tatu (ninawaomba idhini) malaika waliokabidhiwa eneo hili lenye kubarikiwa. Je niingie ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu. Je niingie

ewe Hoja wa Mwenyezi Mungu. Je niingie enyi malaika wa Mwenyezi Mungu mlio wakuruba wenye kuishi katika kaburi hili. Nipe idhini ya kuingia ewe Kiongozi wangu, idhini bora kushinda ile uliyompa yeyote miongoni mwa vipenzi vyako, kwani nikiwa sistahiki hilo, wewe ni mwenye kustahiki kufanya hivyo.”

(Na kama utakuwa katika kumzuru mmoja wa Maimam basi utataja jina lake na jina la baba yake badala ya jina al-Hujja ibnu Hasan al-Mahdi).

Ingia na sema:

بِسْمِ اللَّهِ وَبِاللَّهِ وَفِي سَبِيلِ اللَّهِ وَعَلَى مِلَّةِ رَسُولِ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ
عَلَيْهِ وَآلِهِ اللَّهُمَّ اغْفِرْ لِي وَارْحَمْنِي وَتُبْ عَلَيَّ إِنَّكَ أَنْتَ التَّوَّابُ
الرَّحِيمُ

“Kwa jina la Mwenyezi Mungu, na kwa Mwenyezi Mungu, na katika njia ya Mwenyezi Mungu, na kwa kufuata mila ya Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.), ewe Mwenyezi Mungu nighufirie, nihurumie na nikubalie toba, hakika Wewe ni Mwingi wa kukubali toba na Mwingi wa huruma.”

Ingia kupitia mlango wa Jibril, nao ni ule uliyopo upande wa Baqii. Kisha sema: “Allahu Akbar” mara mia moja. Kisha Sali rakaa mbili salamu ya msikiti, kisha nenda chumba kitukufu, kielekee na sema:

Ziyara ya Kwanza:

اَلسَّلَامُ عَلَیْكَ يَا رَسُوْلَ اللهِ، اَلسَّلَامُ عَلَیْكَ يَا نَبِیَّ اللهِ، اَلسَّلَامُ
عَلَیْكَ يَا مُحَمَّدَ بْنَ عَبْدِ اللهِ، اَلسَّلَامُ عَلَیْكَ يَا خَاتَمَ النَّبِیِّیْنَ،
اَشْهَدُ اَنَّكَ قَدْ بَلَّغْتَ الرِّسَالَةَ، وَاَقَمْتَ الصَّلَاةَ، وَاَتَيْتَ الزَّكَاةَ،
وَاَمَرْتَ بِالْمَعْرُوْفِ، وَنَهَيْتَ عَنِ الْمُنْكَرِ، وَعَبَدْتَ اللهَ مُخْلِصًا
حَتَّى اَتَاكَ الْیَقِیْنُ، فَصَلَّوْاْتُ اللهُ عَلَیْكَ وَرَحْمَتُهُ وَعَلَى اَهْلِ
بَيْتِكَ الطَّاهِرِیْنَ،

“Asalam Alayka ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu!
Asalam Alayka ewe Nabii wa Mwenyezi Mungu! Asalam
Alayka ewe Muhammad bin Abdillah! Asalam Alayka ewe
mwisho wa Manabii! Nashahidilia kwamba hakika wewe
umefikisha ujumbe, umesimamisha Sala, umetoa Zaka,
umeamrisha mema, umekataza maovu na umemwabudu
Mwenyezi Mungu kwa ikhlasi mpaka yakini (kifo)
ilipokufika, hivyo sala za Mwenyezi Mungu na rehema
Zake viwe juu yako na juu ya Ahlul-Baiti wako
watoharifu.”

Kisha simama kwenye nguzo tukufu kuliani mwa kaburi na
hali umeelekea Kibla, na bega lako la kulia likielekea
mimbari. Eneo hili ndipo kilipo kichwa cha Mtume
(s.a.w.w.), sema:

أَشْهَدُ أَنْ لَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ وَحْدَهُ لَا شَرِيكَ لَهُ، وَأَشْهَدُ أَنَّ مُحَمَّدًا
عَبْدُهُ وَرَسُولُهُ، وَأَشْهَدُ أَنَّكَ رَسُولُ اللَّهِ، وَأَنَّكَ مُحَمَّدُ بْنُ عَبْدِ
اللَّهِ، وَأَشْهَدُ أَنَّكَ قَدْ بَلَغْتَ رِسَالَاتِ رَبِّكَ، وَنَصَحْتَ لِأُمَّتِكَ،
وَجَاهَدْتَ فِي سَبِيلِ اللَّهِ، وَعَبَدْتَ اللَّهَ حَتَّى آتَاكَ الْيَقِينُ
بِالْحِكْمَةِ وَالْبُعْظَةِ الْحَسَنَةِ، وَأَدَّيْتَ الَّذِي عَلَيْكَ مِنَ الْحَقِّ،
وَأَنَّكَ قَدْ رُوِّفْتَ بِالْمُؤْمِنِينَ، وَغَلَطْتَ عَلَى الْكَافِرِينَ، فَبَدَّلَ اللَّهُ
بِكَ أَفْضَلَ شَرَفٍ مَحَلِّ الْبُكْرَةِ مِينَ،

الْحَبْدُ لِلَّهِ الَّذِي اسْتَنْقَذَنَا بِكَ مِنَ الشِّرْكِ وَالضَّلَالَةِ، اللَّهُمَّ
فَاجْعَلْ صَلَوَاتِكَ، وَصَلَوَاتِ مَلَائِكَتِكَ الْمُقَرَّبِينَ، وَأَنْبِيَائِكَ
الْبُرْسَلِينَ، وَعِبَادِكَ الصَّالِحِينَ، وَأَهْلِ السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضِينَ،
وَمَنْ سَبَّحَ لَكَ يَا رَبَّ الْعَالَمِينَ مِنَ الْأُولِينَ وَالْآخِرِينَ عَلَى
مُحَمَّدٍ عَبْدِكَ وَرَسُولِكَ وَنَبِيِّكَ وَأَمِينِكَ وَنَحِيِّكَ وَحَبِيبِكَ
وَصَفِيِّكَ وَخَاصَّتِكَ وَصَفْوَتِكَ وَخَيْرَتِكَ مِنْ خَلْقِكَ،

اللَّهُمَّ أَعْطِهِ الدَّرَجَةَ الرَّفِيعَةَ، وَآتِهِ الوَسِيلَةَ مِنَ الْجَنَّةِ،
 وَابْعَثْهُ مَقَاماً مَحْبُوداً يُغْبِطُهُ بِهِ الْأَوَّلُونَ وَالْآخِرُونَ، اللَّهُمَّ
 إِنَّكَ قُلْتَ: وَلَوْ أَنَّهُمْ إِذْ ظَلَمُوا أَنْفُسَهُمْ جَاءُوكَ فَاسْتَغْفَرُوا اللَّهَ
 وَاسْتَغْفَرَ لَهُمُ الرَّسُولُ لَوَجَدُوا اللَّهَ تَوَّاباً رَحِيماً وَإِنِّي أَتَيْتُكَ
 مُسْتَغْفِراً تَائِباً مِنْ دُنُوبِي، وَإِنِّي أَتَوَجَّهُ بِكَ إِلَى اللَّهِ رَبِّي وَرَبِّكَ
 لِيُغْفِرَ لِي دُنُوبِي.

“Nashahidilia kwamba hakuna mungu ila Mwenyezi Mungu, wa pekee hana mshirika. Na nashahidilia kwamba hakika Muhammad ni mja Wake na Mtume Wake. na nashahidilia kwamba hakika wewe ni Mtume wa Mwenyezi Mungu na hakika wewe ni Muhammad bin Abdullah. Na nashahidilia kwamba hakika wewe umefikisha ujumbe wa Mola Wako Mlezi, umeunasihii Ummah Wako, umepigana katika njia ya Mwenyezi Mungu, na umemwabudu Mwenyezi Mungu kwa ikhlasi, hikma na mawaidha mazuri mpaka kifo kilipokufika. Umetekeleza haki iliyokuwa juu yako, na umewafanyia upole waumini na ukali makafiri, hivyo Mwenyezi Mungu akakufikisha kwenye kilele cha ubora wa sehemu ya wale waliotukuzwa.

Kila sifa njema ni ya Mwenyezi Mungu aliyetuepusha na Shirki na upotovu kupitia Kwako. Ewe Mwenyezi Mungu! Weka sala Zako na sala za malaika Wako wakuruba, za

Manabii Wako waliotumwa, za waja Wako wema, za wakazi wa mbinguni na ardhini, na za kila aliyekutakasa ewe Mola Mlezi wa viumbe wote kuanzia za wale waliotangulia mpaka za wale watakaofuatia, juu ya Muhammad mja Wako, Mtume Wako, Nabii Wako, mwaminifu Wako, msiri Wako, kipenzi Chako, mteule Wako, muhtasi Wako na chaguo Lako miongoni mwa viumbe Wako.

Ewe Mwenyezi Mungu! Mpe daraja la juu, mpe wasila toka Peponi na muinue cheo kinachosifika, chenye kutamaniwa na waliotangulia na watakaokuja. Ewe Mwenyezi Mungu! Hakika umesema: **“Na lau wangelikujia walipojidhulumu nafsi zao wakaomba msamaha kwa Mwenyezi Mungu, na Mtume akawaombea msamaha, bila shaka wangemkuta Mwenyezi Mungu, Mwenye kupokea toba, Mwenye kurehemu.”**Nami nimekuja kwako na hali ni mwenye kuomba maghfira na mwenye kutubia dhambi zangu, nami bila shaka nakutanguliza kwa Mwenyezi Mungu Mola wangu Mlezi na Mola wako Mlezi ili anighufirie dhambi zangu.”

Kisha soma sala makhsusi ya Mtume (s.a.w.w.):

اللَّهُمَّ صَلِّ عَلَى مُحَمَّدٍ كَمَا حَبَلٌ وَحَيْكٌ، وَبَدِّغْ رِسَالَتِكَ،
وَصَلِّ عَلَى مُحَمَّدٍ كَمَا أَحَلَّ حَلَالُكَ، وَحَرَّمَ حَرَامَكَ، وَعَلَّمَ
كِتَابِكَ، وَصَلِّ عَلَى مُحَمَّدٍ كَمَا أَقَامَ الصَّلَاةَ، وَآتَى الزَّكَاةَ، وَدَعَا
إِلَى دِينِكَ، وَصَلِّ عَلَى مُحَمَّدٍ كَمَا صَدَّقَ بِوَعْدِكَ، وَأَشْفَقَ مِنْ

وَعَيْدِكَ، وَصَلِّ عَلَى مُحَمَّدٍ كَمَا غَفَرْتَ بِهِ الدُّنُوبَ، وَسَاتَرْتَ بِهِ
 الْعُيُوبَ وَفَرَّجْتَ بِهِ الْكُرُوبَ، وَصَلِّ عَلَى مُحَمَّدٍ كَمَا دَفَعْتَ بِهِ
 الشَّقَاءَ، وَكَشَفْتَ بِهِ الْغُبَاءَ، وَأَجَبْتَ بِهِ الدُّعَاءَ، وَنَجَّيْتَ بِهِ
 مِنَ الْبَلَاءِ، وَصَلِّ عَلَى مُحَمَّدٍ كَمَا رَحِمْتَ بِهِ الْعِبَادَ، وَأَحْيَيْتَ
 بِهِ الْبِلَادَ، وَقَصَصْتَ بِهِ الْجَبَابِرَةَ، وَأَهْلَكْتَ بِهِ الْفَرَاعِنَةَ، وَصَلِّ
 عَلَى مُحَمَّدٍ كَمَا أضعَفْتَ بِهِ الْأَمْوَالَ، وَأَحْرَزْتَ بِهِ مِنَ الْأَهْوَالِ،
 وَكَسَمْتَ بِهِ الْأَصْنَامَ، وَرَحِمْتَ بِهِ الْأَنَامَ، وَصَلِّ عَلَى مُحَمَّدٍ كَمَا
 بَعَثْتَهُ بِخَيْرِ الْأَدْيَانِ، وَأَعَزَّزْتَ بِهِ الْإِيَانَ، وَتَبَرَّرْتَ بِهِ الْأَوْثَانَ،
 وَعَظَّمْتَ بِهِ الْبَيْتَ الْحَرَامَ، وَصَلِّ عَلَى مُحَمَّدٍ وَأَهْلِ بَيْتِهِ
 الطَّاهِرِينَ الْأَخْيَارِ وَسَلِّمْ تَسْلِيمًا

“Ewe Mwenyezi Mungu! Msalie Muhammad kama alivyobeba wahyi Wako na akafikisha ujumbe Wako. Na msalie Muhammad kama alivyohalalisha halali Yako na akaharamisha haramu Yako na akafundisha Kitabu Chako. Na msalie Muhammad kama alivyosimamisha Sala, akatoa Zaka na akalingania katika dini Yako. Na msalie Muhammad kama alivyosadikisha ahadi ya adhabu Yako na akajiepusha na adhabu Yako. Na msalie Muhammad

kama ulivyomsamehe makosa, ukamsitiria aibu na ukamwondolea matatizo. Na msalie Muhammad kama ulivyomwondolea mashaka, ukamwondolea huzuni, ukamjibia dua na ukamwokoia na balaa. Na msalie Muhammad kama ulivyowarehemu waja kupitia kwake, ukahuisha nchi kupitia kwake, ukawang'oa majabari kupitia kwake na ukawahilikisha mafarao kupitia kwake. Na msalie Muhammad kama ulivyodhoofisha mali kupitia kwake, ukazuia vitisho kupitia kwake, ukateketeza masanamu kupitia kwake na ukawarehemu viumbe kupitia kwake. Na msalie Muhammad kama ulivyomtuma akiwa na dini bora, ukaipa nguvu imani kupitia kwake, ukaangamiza masanamu kupitia kwake na ukaitukuza Nyumba tukufu kupitia kwake. Na msalie Muhammad na watu wa nyumba yake watoharifu wema, na msalimie sana.”

Ziyara ya Pili:

Simama kwenye nguzo upande wa kulia wa kaburi tukufu kichwani, na useme:

السَّلَامُ عَلَيْكَ أَيُّهَا النَّبِيُّ وَرَحْمَةُ اللَّهِ وَبَرَكَاتُهُ ، السَّلَامُ عَلَيْكَ ،
 يَا أَبَا الْقَاسِمِ ، السَّلَامُ عَلَيْكَ يَا سَيِّدَ الْأَوَّلِينَ وَالْآخِرِينَ ،
 السَّلَامُ عَلَيْكَ يَا زَيْنَ الْقِيَامَةِ ، السَّلَامُ عَلَيْكَ يَا شَفِيعَ الْقِيَامَةِ
 ، أَشْهَدُ أَنْ لَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ ، وَحْدَهُ لَا شَرِيكَ لَهُ ، وَأَشْهَدُ أَنَّكَ عَبْدُهُ
 وَرَسُولُهُ ، بَلَّغْتَ الرِّسَالَةَ ، وَأَدَّيْتَ الْأَمَانَةَ ، وَنَصَحْتَ أُمَّتَكَ ،

وَجَاهَدْتُ فِي سَبِيلِ رَبِّكَ حَتَّى آتَاكَ الْيَقِينُ ، صَلَّى اللهُ عَلَيْكَ ،
 وَعَلَى أَهْلِ بَيْتِكَ ، طِبْتَ حَيًّا وَطِبْتَ مَيِّتًا ، صَلَّى اللهُ عَلَيْكَ
 وَعَلَى أَخِيكَ وَوَصِيِّكَ وَابْنِ عَمِّكَ أَمِيرِ الْمُؤْمِنِينَ ، وَعَلَى ابْنَتِكَ
 سَيِّدَةِ نِسَاءِ الْعَالَمِينَ ، وَعَلَى وَلَدَيْكَ الْحَسَنِ وَالْحُسَيْنِ ،
 أَفْضَلَ السَّلَامِ وَأَطْيَبَ التَّحِيَّةِ وَأَطْهَرَ الصَّلَاةِ ، وَعَلَيْنَا مِنْكُمْ
 السَّلَامُ وَرَحْمَةُ اللهِ وَبَرَكَاتُهُ

“Amani iwe juu yako ewe Nabii wa Mwenyezi Mungu na rehema za Mwenyezi Mungu na Baraka Zake! Amani iwe juu yako ewe Abul Qasim! Amani iwe juu yako ewe bwana wa waliotangulia na watakaokuja! Amani iwe juu yako ewe pambo la Kiyama! Amani iwe juu yako ewe mwombezi wa siku ya Kiyama! Nashuhudilia kwamba hapana mungu ila Mwenyezi Mungu wa pekee asiye na mshirika. Na nashuhudilia kwamba hakika wewe ni mja Wake na Mtume Wake,umefikisha ujumbe na umefikisha amana, umeunasihi Ummah wako na umejitolea katika njia ya Mola Wako Mlezi mpaka kifo kilipokufika. Sala za Mwenyezi Mungu ziwe juu yako na juu ya Ahlul-Baiti wako, ni mwema ukiwa hai na hata ukiwa maiti. Sala za Mwenyezi Mungu ziwe juu yako na juu ya ndugu yako, Wasii wako na binamu yako Amirul-Muuminina,na ziwe juu ya binti yako mbora wa wanawake wote wa ulimwenguni, na juu ya wanao Hasan na Husein, salamu bora, maamkizi mema na sala safi. Na ziwe juu yetu toka

kwenu salamu, rehema za Mwenyezi Mungu na Baraka Zake.”

Ni Sunna kwamba uweke mkono wako juu ya ukuta wa jiwe na useme:

أَتَيْتَكَ يَا رَسُولَ اللَّهِ مُهَاجِرًا إِلَيْكَ ، قَاضِيًا لَهَا أَوْجِبَهُ اللَّهُ عَلَيَّ
مَنْ قَصَدَكَ ، وَإِذْ لَمْ أُلْحِقْكَ حَيًّا ، فَقَدْ قَصَدْتِكَ بَعْدَ مَوْتِكَ
عَالِيًا أَنْ حُرِّمَتْكَ مَيِّتًا كَحُرْمَتِكَ حَيًّا ، فَكُنْ لِي بِذَلِكَ عِنْدَ
اللَّهِ شَاهِدًا

“Nimekuja kwako ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu na hali ni mwenye kuhamia kwako na mwenye kutimiza yale aliyoyawajibisha Mwenyezi Mungu juu ya yule mwenye kukukusudia. Ijapokuwa sijakudiriki ukiwa hai lakini bila shaka nimekukusudia baada ya kifo chako na hali ni mwenye kujua kwamba hakika utukufu wako wakati wa kifo chako ni sawa na utukufu wako wakati wa uhai wako, basi kuwa shahidi wa hayo mbele ya Mwenyezi Mungu.”

Ni Sunna kwamba upitisha kiganja chako juu ya uso wako na hali wasema:

اللَّهُمَّ اجْعَلْ ذَلِكَ بَيْعَةً مَرْضِيَّةً لَدَيْكَ ، وَعَهْدًا مُؤَكَّدًا عِنْدَكَ ،
تُحْيِيَنِي مَا أَحْيَيْتَنِي عَلَيْهِ ، وَعَلَى الْوَفَاءِ بِشَرَائِطِهِ وَحُدُودِهِ

وَحُقُوقِهِ وَأَحْكَامِهِ ، وَتَمَيَّنِي إِذَا أَمَّتَنِي عَلَيْهِ ، وَتَبَعْتَنِي إِذَا
بَعَثْتَنِي عَلَيْهِ

“Ewe Mwenyezi Mungu! Jaalia hayo yawe ni kiapo cha utii chenye kuridhiwa Kwako na ahadi yenye kuisisitizwa Kwako, nipe uhai madhali tu bado wanipa uhai wa kuitekeleza na kutimiza sharti zake, miko yake, haki zake na hukumu zake. Na unifishe madhali tu wanifisha juu yake, na unifufue madhali tu wanifufua juu yake.”

Ziyara ya Tatu:

Lielekee kaburi tukufu kwa kuipa mgongo Kibla, na sema:

السَّلَامُ عَلَيْكَ يَا نَبِيَّ اللَّهِ وَرَسُولَهُ. السَّلَامُ عَلَيْكَ يَا صَفْوَةَ اللَّهِ
وَخَيْرَتَهُ مِنْ خَلْقِهِ. السَّلَامُ عَلَيْكَ يَا أَمِينَ اللَّهِ وَحُجَّتَهُ. السَّلَامُ
عَلَيْكَ يَا خَاتِمَ النَّبِيِّينَ وَسَيِّدَ الْمُرْسَلِينَ. السَّلَامُ عَلَيْكَ أَيُّهَا
الْبَشِيرُ النَّذِيرُ. السَّلَامُ عَلَيْكَ أَيُّهَا الدَّاعِي إِلَى اللَّهِ وَالسِّرَاجِ
الْمُنِيرِ. السَّلَامُ عَلَيْكَ وَعَلَى أَهْلِ بَيْتِكَ الَّذِينَ أَذْهَبَ اللَّهُ عَنْهُمْ

الرَّجْسَ وَطَهَّرَهُمْ تَطْهِيراً. أَشْهَدُ أَنَّكَ يَا رَسُولَ اللَّهِ أَتَيْتَ بِالْحَقِّ
وَقُلْتَ بِالصِّدْقِ.

الْحَبْدُ لِلَّهِ الَّذِي وَفَّقَنِي لِلإِيَانِ وَالتَّصْدِيقِ وَمَنْ عَلَّمَ
بِطَاعَتِكَ وَاتِّبَاعِ سَبِيلِكَ، وَجَعَلَنِي مِنْ أُمَّتِكَ وَالمُجِيبِينَ
لِدَعْوَتِكَ، وَهَدَانِي إِلَى مَعْرِفَتِكَ، وَمَعْرِفَةِ الإِثْمَةِ مِنْ ذُرِّيَّتِكَ.
أَتَقَرَّبُ إِلَى اللَّهِ بِمَا يُرْضِيكَ، وَأَبْرَأُ إِلَى اللَّهِ مِمَّا يُسْخِطُكَ مُوَالِيًا
لِأَوْلِيَائِكَ، مُعَادِيًا لِأَعْدَائِكَ. جِئْتُكَ يَا رَسُولَ اللَّهِ زَائِرًا،
وَقَصَدْتُكَ رَاغِبًا مُتَوَسِّلًا إِلَى اللَّهِ سُبْحَانَهُ، وَأَنْتَ صَاحِبُ
الْوَسِيلَةِ وَالمُنْزِلَةِ المَجْلِيَّةِ، وَالمَشْفَاعَةِ المَقْبُولَةِ، وَالمَدْعُوَّةِ
المَسْئُوعَةِ، فَاشْفَعْ لِي إِلَى اللَّهِ تَعَالَى بِالمَغْفِرَانِ وَالمَرْحَمَةِ،
وَالمَتَّوْفِيقِ وَالمَعْصَمَةِ، فَقَدْ غَبَرْتُ الدُّنُوبَ، وَشَبَلْتُ العُيُوبَ،
وَأثْقَلْتُ الظُّهْرَ، وَتَضَاعَفَ الوِزْرُ.

وَقَدْ أَخْبَرْتَنَا وَخَبَرَكَ الصِّدْقُ أَنَّ تَعَالَى قَالَ، وَقَوْلُهُ الْحَقُّ: وَلَوْ أَنَّ
 تَهُمْ إِذْ ظَلَبُوا أَنْفُسَهُمْ جَاءُوكَ فَاسْتَغْفَرُوا اللَّهَ وَاسْتَغْفَرَ لَهُمْ
 الرَّسُولُ لَوَجَدُوا اللَّهَ تَوَّابًا رَحِيمًا وَقَدْ جِئْتِكَ يَا رَسُولَ اللَّهِ
 مُسْتَغْفِرًا مِنْ ذُنُوبِي، تَائِبًا مِنْ مَعَاصِيٍّ وَسَيِّئَاتِي، وَإِنِّي أُنْتَوِّجُهُ إِلَى
 اللَّهِ رَبِّي وَرَبِّكَ، لِيَغْفِرَ لِي ذُنُوبِي فَاشْفَعْ لِي يَا شَفِيعَ الْأُمَّةِ، وَأَجِرْنِي
 يَا نَبِيَّ الرَّحْمَةِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْكَ وَعَلَى آلِكَ الطَّاهِرِينَ

“Amani iwe juu yako ewe Nabii wa Mwenyezi Mungu na Mtume Wake! Amani iwe juu yako ewe mteule wa Mwenyezi Mungu na chaguo Lake toka katika viumbe Wake! Amani iwe juu yako ewe mwaminifu wa Mwenyezi Mungu na hoja Yake! Amani iwe juu yako ewe mwisho wa Manabii na sayidi wa Mitume! Amani iwe juu yako ewe mtoaji wa habari njema na mwonyaji! Amani iwe juu yako ewe muitaji kwa Mwenyezi Mungu na taa itoayo nuru! Amani iwe juu yako na juu ya Ahlul-Baiti wako ambao Mwenyezi Mungu amewaondolea uchafu na kuwatakasa kabisa. Nakiri kwamba hakika wewe ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu umeleta haki na umesema kweli.

Kila sifa njema ni ya Mwenyezi Mungu ambaye ameniwafikisha kuamini na kusadiki, na amenineemesha kukutii na kufuata njia yako, amenijaalia kuwa miongoni mwa Ummah wako na wenye kuitikia wito wako, na ameniongoza katika kukujua wewe na kuwajua Maimamu

toka katika kizazi chako. Najikurubisha kwa Mwenyezi Mungu kwa yale yanayokuridhisha na ninajisalimisha kwa Mwenyezi Mungu kwa kujiepusha na yale yanayokuchukiza, ni mwenye upendo kwa vipenzi vyako na ni mwenye uadui kwa maadui zako. Nimekuja kwako ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu na hali ni mwenye kukuzuru, na nimekukusudia na hali ni mwenye raghba nawe na ni mwenye kukufanya wasila wa kufikia kwa Mwenyezi Mungu, nawe ndiye mwenye wasila, cheo kitukufu, Shufaa yenye kukubalika na ombi lenye kukubaliwa. Hivyo niombe kwa Mwenyezi Mungu maghfira, rehema, taufiki na kinga, kwani bila shaka dhambi zimepindukia, aibu zimeenea, mgongo wangu umehemezwa, na uzito umeongezeka.

Na bila shaka umetupa habari na habari zako ni kweli tupu, kwamba Mwenyezi Mungu amesema na kauli Yake ni haki tupu: **“Na lau wangelikujia walipojidhulumu nafsi zao wakaomba msamaha kwa Mwenyezi Mungu, na Mtume akawaombea msamaha, bila shaka wangemkuta Mwenyezi Mungu, Mwenye kupokea toba, Mwenye kurehemu.”** Nami nimekujia ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu na hali ni mwenye kuomba maghfira dhidi ya dhambi zangu na ni mwenye kutubia maasi yangu na maovu yangu. Na hakika mimi naelekea kwa Mwenyezi Mungu Mola Wangu Mlezi na Mola Wako Mlezi ili anighufirie dhambi zangu, hivyo niombe ewe mwombezi wa Ummah na niokoe ewe Nabii wa rehema, sala za Mwenyezi Mungu ziwe juu yako na juu ya aali zako watoharifu.”

Soma dua ya Ali bin Husein Zaynul-'Abidin (a.s.) na hali umeegemeza mgongo wako kwenye kaburi. Kisha tambua kwamba kumpa kisogo Mtume ijapokuwa kidhahiri ni

utovu wa adabu, lakini si vibaya iwapo tu ni kwa lengo la kuelekea kwa Mwenyezi Mungu:

اللَّهُمَّ إِلَيْكَ أَلَجَاتُ أَمْرِي ، وَإِلَى قَبْرِ نَبِيِّكَ مُحَمَّدٍ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ
وَآلِهِ عَبْدُكَ وَرَسُولُكَ أَسْنَدْتُ ظَهْرِي ، وَالْقِبْلَةَ الَّتِي رَضِيتَ
لِ مُحَمَّدٍ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ اسْتَقْبَلْتُ . اللَّهُمَّ إِنِّي أَصْبَحْتُ لَا
أَمِدُّكَ لِنَفْسِي خَيْرَ مَا أَرْجُو لَهَا ، وَلَا أَدْفَعُ عَنْهَا شَيْئًا مَا أَحْذَرُ
عَلَيْهَا ، وَأَصْبَحْتُ الْأُمُورَ كُلَّهَا بِيَدِكَ ، وَلَا فَتْقِيرَ أَفْقَرُ مِنِّي ، إِنِّي
لِهَا أَنْزَلْتُ إِلَيَّ مِنْ خَيْرِ فَتْقِيرٍ . اللَّهُمَّ أَرِدْنِي مِنْكَ بِخَيْرٍ وَلَا رَادًا
لِفَضْلِكَ ، اللَّهُمَّ إِنِّي أَعُوذُ بِكَ مِنْ أَنْ تُبَدِّلَ إِسْمِي أَوْ تُغَيِّرَ جِسْمِي
أَوْ تُزِيلَ نِعْمَتَكَ عَنِّي ، اللَّهُمَّ زَيِّنِي بِالتَّقْوَى وَجَبِّلْنِي بِالنِّعَمِ
وَاعْبُرْنِي بِالعَافِيَةِ وَارْتُقِنِي شُكْرَ العَافِيَةِ

“Ewe Mwenyezi Mungu! Nimelileta jambo langu Kwako,nimeegemeza mgongo wangu kwenye kaburi la Nabii Wako Muhammad (s.a.w.w.) mja Wako na Mtume Wako,na nimeelekea kwenye Kibla Chako ulichomchagulia Muhammad (s.a.w.w.). Ewe Mwenyezi Mungu! Hakika mimi nimeamka ilihali similiki kheri yoyote ninayoitaraji kwa ajili ya nafsi yangu, na ilihali siwezi kuiondolea shari yoyote ninayoioigopa juu yake,

hivyo mambo yote yamepambazukiwa yakiwa mikononi Mwako na hakuna mhitaji kushinda mimi kwani hakika mimi ni mhitaji wa kheri utakayoniteremshia. Ewe Mwenyezi Mungu! Nirudishe na kheri toka Kwako kwani hakuna wa kuzuia fadhila Zako. Ewe Mwenyezi Mungu! Hakika mimi najikinga Kwako usilibadili jina langu na kughairi mwili wangu au kuondoa neema Yako kwangu. Ewe Mwenyezi Mungu nipambe kwa uchamungu, nipendezeshe kwa neema, nifunike afya njema, na niruzuku hali ya kushukuru afya.”

Omba haja yako kwani ina nafasi kubwa ya kukidhiwa. Ni Sunna kusoma Sura al-Qadri mara kumi na moja na uombe haja yako. Kisha Sali rakaa mbili na thawabu zake uzitoe zawadi kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.), useme:

اللَّهُمَّ إِنِّي صَلَّيْتُ وَرَكَعْتُ وَسَجَدْتُ لَكَ وَحَدَّكَ لِأَشْرِيكَ لَكَ لِأَنَّ
 الصَّلَاةَ وَالرُّكُوعَ وَالسُّجُودَ لَا يَكُونُ إِلَّا لَكَ لِأَنَّكَ أَنْتَ اللَّهُ لَا إِلَهَ إِلَّا
 أَنْتَ اللَّهُمَّ صَلِّ عَلَى مُحَمَّدٍ وَآلِ مُحَمَّدٍ وَأَبْلِغْهُمْ عَنِّي أَفْضَلَ
 السَّلَامِ وَالتَّحِيَّةِ وَارْدُدْ عَلَيَّ مِنْهُمْ السَّلَامَ اللَّهُمَّ وَهَاتَانِ
 الرُّكْعَتَانِ هَدِيَّةٌ مِنِّي إِلَى سَيِّدِي وَ مَوْلَايَ رَسُولِ اللَّهِ (ص)
 فَتَقَبَّلْهُمَا مِنِّي بِأَحْسَنِ قَبُولِكَ وَأَجْرُنِي عَلَيَّ ذَلِكَ بِأَفْضَلِ أَمَلِي
 وَرَجَائِي فِيكَ وَفِي رَسُولِكَ يَا وَلِيَّ الْمُؤْمِنِينَ

“Ewe Mwenyezi Mungu! Hakika mimi nimesali, nimerukuu na nimesujudu kwa ajili Yako Wewe peke Yako usiye na mshirika, kwa sababu Sala, rukuu na sijda havipasi kutekelezwa ila kwa ajili Yako, kwa sababu Wewe ndiye Allah Ambaye hakuna mungu ila Wewe. Ewe Mwenyezi Mungu msalie Muhammad na aali Muhammad, Na wafikishie salamu bora na maamkizi kutoka kwangu, Na nifikishie salamu kutoka kwao. Ewe Mwenyezi Mungu! Hizi rakaa mbili ni zawadi kutoka kwangu kwenda kwa bwana wangu na kiongozi wangu Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.), hivyo zipokee toka kwangu kwa mapokezi Yako mema, na unipe malipo juu yake kwa kiwango bora cha matumaini yangu na matarajio yangu Kwako na kwa Mtume Wako, ewe Kiongozi wa waumini.”

Ni Sunna pia kwamba baada ya Sala usome dua hii:

اللَّهُمَّ إِنَّكَ قُلْتَ لِنَبِيِّكَ مُحَمَّدٍ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ: وَلَوْ أَنَّهُمْ إِذْ
 ظَلَمُوا أَنفُسَهُمْ جَاءُوكَ فَاسْتَغْفَرُوا اللَّهَ وَاسْتَغْفَرَ لَهُمُ الرَّسُولُ
 لَوَجَدُوا اللَّهَ تَوَّابًا رَحِيمًا اللَّهُمَّ وَلَمْ أَحْضُرْ زَمَانَ رَسُولِكَ عَلَيْهِ
 وَآلِهِ السَّلَامُ، وَقَدْ زُرْتُهُ رَاغِبًا تَائِبًا مِنْ سَيِّئِ عَمَلِي،
 وَمُسْتَغْفِرًا لَكَ مِنْ ذُنُوبِي وَمُقَرَّرًا لَكَ بِهَا وَأَنْتَ أَعْلَمُ بِهَا مِنِّي،
 وَمُتَوَجِّهًا إِلَيْكَ بِنَبِيِّكَ نَبِيِّ الرَّحْمَةِ صَلَوَاتِكَ عَلَيْهِ وَآلِهِ،

فَاَجْعَلْنِي اَللّٰهُمَّ بِمُحَمَّدٍ وَاَهْلِ بَيْتِهِ عِنْدَكَ وَجِيهًا فِي الدُّنْيَا
وَالْآخِرَةِ وَمِنَ الْمُتَقَرَّبِينَ،

يَا مُحَمَّدُ يَا رَسُولَ اللَّهِ، يَا أَبِي أَنْتَ وَأُمِّي يَا نَبِيَّ اللَّهُ يَا سَيِّدَ خَلْقِ
اللَّهِ، إِنِّي أَتَوَجَّهُ بِكَ إِلَى اللَّهِ رَبِّكَ وَرَبِّي لِيَغْفِرَ لِي ذُنُوبِي، وَيَتَقَبَّلَ
مَنِّي عَلَيَّ، وَيَقْضِيَ لِي حَوَائِجِي، فَكُنْ لِي شَفِيعًا عِنْدَ رَبِّكَ وَرَبِّي،
فَنِعْمَ الْمَسْئُولُ الْمَوْلَى رَبِّي، وَنِعْمَ الشَّفِيعُ أَنْتَ يَا مُحَمَّدُ، عَلَيْكَ
وَعَلَى أَهْلِ بَيْتِكَ السَّلَامُ، اَللّٰهُمَّ وَاوْجِبْ لِي مِنْكَ الْمَغْفِرَةَ
وَالرَّحْمَةَ وَالرِّزْقَ الْوَاسِعَ الطَّيِّبَ التَّافِعَ، كَمَا أَوْجَبْتَ لِبَنِّ آتِي
نَبِيِّكَ مُحَمَّدًا صَلَوَاتِكَ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَهُوَ حَيٌّ، فَغَفَّرْتَ لَهُ بِرَحْمَتِكَ
يَا أَرْحَمَ الرَّاحِمِينَ، فَأَقْرَأْ لَهُ بِذُنُوبِهِ وَاسْتَغْفِرْ لَهُ رَسُولُكَ عَلَيْهِ
وَآلِهِ السَّلَامُ، وَصَلَّى اللَّهُ عَلَى مُحَمَّدٍ وَآلِهِ الطَّاهِرِينَ.

“Ewe Mwenyezi Mungu! Hakika Wewe ulimwambia Nabii
Wako Muhammad (s.a.w.w.):”**Na lau wangelikujia
walipojidhulumu nafsi zao wakaomba msamaha kwa
Mwenyezi Mungu, na Mtume akawaombea msamaha,
bila shaka wangemkuta Mwenyezi Mungu, Mwenye**

kupokea toba, Mwenye kurehemu.” Ewe Mwenyezi Mungu! Sikuzidiriki zama za Mtume Wako (a.s.), lakini bila shaka nimemzuru na hali ni mwenye raghba, ni mwenye kutubia ubaya wa amali yangu, ni mwenye kuomba maghfira Kwako dhidi ya dhambi zangu na ni mwenye kuungama dhambi hizo Kwako, Nawe wazijua zaidi kushinda mimi, na ni mwenye kuelekea Kwako kupitia Nabii Wako, Nabii wa rehema, sala Zako ziwe juu yake na juu ya aali zake, hivyo nijaalie ewe Mwenyezi Mungu kwa haki ya Muhammad na watu wa nyumba yake niwe mwenye hadhi Kwako duniani na akhera, na niwe miongoni mwa wenye kukurubishwa.

“Ewe Muhammad! Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu! (s.a.w.w.) Nakufidia kwa baba yangu, na mama yangu, ewe Nabii wa Mwenyezi Mungu! Ewe mbora wa viumbe vya Mwenyezi Mungu! Hakika mimi naelekea kupitia kwako kwa Mwenyezi Mungu Mola Wangu Mlezi na Mola Wako Mlezi ili anighufirie dhambi zangu, na apokee amali toka kwangu na anikidhie haja zangu. Hivyo kuwa mwombezi wangu mbele ya Mola Wako Mlezi na Mola Wangu Mlezi, muombwa bora aliye bwana ni Mola Wangu Mlezi, na muombezi bora ni wewe ewe Muhammad salamu ziwe juu yako na juu ya watu wa nyumba yako. Ewe Mwenyezi Mungu! Niwajibishie toka Kwako maghfira, rehema, riziki pana nzuri na yenye manufaa, kama ulivyowajibisha kwa yule aliyemjia Nabii Wako Muhammad (s.a.w.w.) wakati wa uhai wake, na akaungama dhambi zake Kwako; na Mtume Wako (s.a.w.w.) akanwombea maghfira, Nawe ukamghufiria kwa rehema Zako ewe mwenye kurehemu kushinda wote wenye kurehemu. Na sala za Mwenyezi Mungu ziwe juu ya Muhammad na aali zake watoharifu.”

Ziyara ya Nne:

Nayo ni ya kumzuru Mtume (s.a.w.w.) kwa mbali. Mtume (s.a.w.w.) amesema: “Atakayezuru kaburi langu baada ya kifo changu ni kama aliyenijia wakati wa uhai wangu, ikiwa hamtaweza kulizuru kaburi langu basi nitumieni salamu kwani hakika hunifikia.”

Imepokewa kutoka kwa Ahmad bin Abi Nasri al-Bazantiy kutoka kwa Ridha (a.s.) kwamba alisema: “Utasema baada ya Sala ya wajibu:

السَّلَامُ عَلَيْكَ يَا رَسُولَ اللَّهِ وَرَحْمَةُ اللَّهِ وَبَرَكَاتُهُ السَّلَامُ عَلَيْكَ
يَا مُحَمَّدُ بْنُ عَبْدِ اللَّهِ السَّلَامُ عَلَيْكَ يَا خَيْرَةَ اللَّهِ السَّلَامُ عَلَيْكَ
يَا حَبِيبَ اللَّهِ السَّلَامُ عَلَيْكَ يَا صَفْوَةَ اللَّهِ السَّلَامُ عَلَيْكَ يَا أَمِينَ
اللَّهُ أَشْهَدُ أَنَّكَ رَسُولُ اللَّهِ وَأَشْهَدُ أَنَّكَ مُحَمَّدُ بْنُ عَبْدِ اللَّهِ
وَأَشْهَدُ أَنَّكَ قَدْ نَصَحْتَ لِأُمَّتِكَ وَجَاهَدْتَ فِي سَبِيلِ رَبِّكَ
وَعَبَدْتَهُ حَتَّى أَتَاكَ الْيَقِينُ فَجَزَاكَ اللَّهُ يَا رَسُولَ اللَّهِ أَفْضَلَ مَا
جَزَى نَبِيًّا عَنْ أُمَّتِهِ اللَّهُمَّ صَلِّ عَلَى مُحَمَّدٍ وَآلِ مُحَمَّدٍ أَفْضَلَ
مَا صَلَّيْتَ عَلَى إِبْرَاهِيمَ وَآلِ إِبْرَاهِيمَ إِنَّكَ حَبِيدٌ مَجِيدٌ

“Amani iwe juu yako ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu na rehema za Mwenyezi Mungu na Baraka Zake! Amani iwe juu yako ewe Muhammad bin Abdullah! Amani iwe juu yako ewe chaguo la Mwenyezi Mungu! Amani iwe juu yako ewe kipenzi cha Mwenyezi Mungu! Amani iwe juu yako ewe mteule wa Mwenyezi Mungu! Amani iwe juu yako ewe mwaminifu wa Mwenyezi Mungu! Nashahidilia kwamba hakika wewe ni Mtume wa Mwenyezi Mungu, na nashahidilia kwamba hakika wewe ni Muhammad bin Abdullah, na nashahidilia kwamba hakika wewe umeunasihi Ummah wako na umepigana katika njia ya Mola Wako Mlezi, na umemwabudu kwa ikhlasi mpaka kifo kilipokufika, namwomba Mwenyezi Mungu akulipe ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu malipo bora kushinda yale aliyomlipa Nabii yeyote kwa ajili ya Ummah wake. Ewe Mwenyezi Mungu! Msalie Muhammad na aali Muhammad sala bora kushinda ile uliyomsalia Ibrahim na aali Ibrahim, hakika Wewe ni Mhimidiwa Msifika.”

Kithirisha kusalia ndani ya msikiti wa Nabii (s.a.w.w.), kwani hakika Sala moja humo ni sawa na Sala elfu moja nje ya humo, na hasa eneo lililopo kati ya mimbari na kaburi tukufu, kwani imekuja riwaya toka kwake (s.a.w.w.) kwamba alisema: “Eneo lililopo kati ya kaburi langu na mimbari yangu ni kitalu miongoni mwa vitalu vya peponi, na mimbari yangu ni sawa na mlango miongoni mwa milango ya Peponi.” Na mpaka wa kitalu kitukufu kwa urefu ni tokea kwenye kaburi tukufu mpaka eneo la mimbari, na kwa upana ni tokea kwenye mimbari hadi kwenye nguzo ya nne. Ni sunna kusoma dua hii eneo hilo la kitalu kitukufu:

Dua isomwayo katika kitalu kitukufu:

اللَّهُمَّ إِنَّ هَذِهِ رَوْضَةٌ مِنْ رِيَاضِ جَنَّتِكَ وَشُعْبَةٌ مِنْ شُعَبِ
رَحْمَتِكَ الَّتِي ذَكَرَهَا رَسُولُكَ وَأَبَانَ عَنْ فَضْلِهَا وَشَرَفِ التَّعْبُدِ
لَكَ فِيهَا فَقَدْ بَلَغْتَنِيهَا فِي سَلَامَةٍ نَفْسِي فَذَكَ الْاِحْدُ يَا سَيِّدِي
عَلَى عَظِيمِ نِعْمَتِكَ عَلَيَّ فِي ذَلِكَ وَعَلَى مَا زَرَقْتَنِيهِ مِنْ طَاعَتِكَ
وَطَلَبِ مَرْضَاتِكَ وَتَعْظِيمِ حُرْمَةِ نَبِيِّكَ بِزِيَارَةِ قَبْرِهِ وَالتَّسْلِيمِ
عَلَيْهِ وَالتَّرَدُّدِ فِي مَشَاهِدِهِ وَمَوَاقِفِهِ

فَذَكَ الْاِحْدُ يَا مَوْلَايَ حَمْدًا يَنْتَظِمُ بِهِ مَحَامِدُ حَمَلَةِ عَرْشِكَ
وَسُكَّانِ سَبَوَاتِكَ وَيَقْصُرُ عَنْهُ حَمْدُ مَنْ مَضَى وَيَفْضُلُ حَمْدَ مَنْ
بَقِيَ مِنْ خَلْقِكَ وَلَكَ الْاِحْدُ يَا مَوْلَايَ حَمْدًا مَنْ عَرَفَ الْاِحْدُ
لَكَ وَالتَّوْفِيقَ لِلْحَمْدِ مِنْكَ حَمْدًا يَبْلَأُ مَا خَلَقْتَ، وَيَبْدَعُ حَيْثُ
مَا أَرَدْتَ، وَلَا يَحْجُبُ عَنْكَ، وَلَا يَنْقُضِي دُونَكَ، وَيَبْدَعُ أَقْصَى
رِضَاكَ، وَلَا يَبْدَعُ آخِرَهُ أَوْ ائِلَ مَحَامِدَ خَلْقِكَ لَكَ وَلَكَ الْاِحْدُ

مَا عَرِفَ الْحَبْدُ وَاعْتَقَدَ الْحَبْدُ وَجُعِلَ ابْتِدَاءُ الْكَلَامِ الْحَبْدُ
يَا بَاقِيَ الْعِزِّ وَالْعِظَمَةِ وَدَائِمَ السُّلْطَانِ وَالْقُدْرَةَ وَشَدِيدَ الْبَطْشِ
وَالْقُوَّةَ، وَنَافِذَ الْأَمْرِ وَالْإِرَادَةَ وَوَاسِعَ الرَّحْمَةِ وَالْبُغْفَرَةَ وَرَبَّ
الدُّنْيَا وَالْآخِرَةِ، كَمْ مِنْ نِعْمَةٍ لَكَ عَلَيَّ يَقْضُمُ عَنْ أَيْسَرِهَا
حَبْدِي، وَلَا يَيْدُغُ أَذْنَاهَا شُكْرِي

وَكَم مِنْ صَنَاءِعٍ مِنْكَ إِلَيَّ لَا يُحِيطُ بِكَثْرَتِهَا وَهِيَ، وَلَا يُقَيِّدُهَا
فِكْرِي اللَّهُمَّ صَلِّ عَلَى نَبِيِّكَ الْمُصْطَفَى بَيْنَ الْبَرِّيَّةِ طِفْلاً وَخَيْرِهِ
شَاباً وَكَهْلاً أَطْهَرَ الْبُطْهَرِينَ شَيْبَةً وَأَجُودُ الْمُسْتَطْبِرِينَ دِيبَةً،
وَأَعْظَمِ الْخَلْقِ جُرْثُومَةَ الَّذِي أَوْضَحْتَ بِهِ الدَّلَالَاتِ وَأَقْبَتَ بِهِ
الرِّسَالَاتِ، وَخَتَبْتَ بِهِ التُّبُوتِ وَفَتَحْتَ بِهِ الْخَرِيَاتِ وَأَظْهَرْتَ
مُظْهَرًا وَابْتَعَثْتَهُ نَبِيًّا وَهَادِيًّا، أَمِينًا مَهْدِيًّا وَدَاعِيًّا إِلَيْكَ وَدَالًّا
عَلَيْكَ وَحُجَّةً بَيْنَ يَدَيْكَ اللَّهُمَّ صَلِّ عَلَى الْمُعْصُومِينَ مِنْ عَثْرَتِهِ
وَالطَّيِّبِينَ مِنْ أَسْرَتِهِ، وَشَرِّفْ لَدَيْكَ مَنَازِلَهُمْ، وَعَظِّمْ عِنْدَكَ

مَرَاتِبَهُمْ، وَاجْعَلْ فِي الرَّفِيقِ الْأَعْلَى مَجَالِسَهُمْ وَارْفَعْ إِلَى قَرَبِ
رَسُولِكَ دَرَجَاتَهُمْ، وَتَبِّم بِلِقَائِهِ سُورَهُمْ وَوَفِّرْ بِكَأَنَّهُ أَنْسَهُمْ

“Ewe Mwenyezi Mungu! Hakika hiki ni kitalu miongoni mwa vitalu vya Pepo Yako, na ni mkondo miongoni mwa mikondo ya rehema Zako ambao ametaja Mtume Wako na akabainisha fadhila zake na sharafu ya kufanyia ibada humo, bila shaka umenifikisha katika mkondo huo na hali nafsi yangu ikiwa salama, hivyo una kila sifa njema ewe Bwana Wangu kutokana na neema Yako adhimu uliyonipa katika hilo, na kutokana na yale uliyoniruzuku ikiwemo kitendo cha kukutii Wewe, kutafuta radhi Yako na kutukuza heshima ya Nabii Wako kwa kulizuru kaburi lake, kumtolea salamu na kutaradadi maeneo yake na sehemu alizosimama.

“Una kila sifa njema ewe Kiongozi Wangu sifa njema ambazo kwazo unanadhimika kwa ajili Yako utukuzaji wa wabebaji wa Arshi Yako na wakazi wa mbingu Yako, na ambazo kwa ajili Yako hazifikiwi na himidi za waliopita na zinazishinda himidi za waliobakia miongoni mwa viumbe Wako. Na una kila sifa njema ewe Kiongozi Wangu sifa njema ya yule aliyejua kukuhimidi Wewe na akawafikishwa kupata tawfiki ya kukuhimidi toka Kwako. Sifa njema inayojaza ulivyoumba na inafika kiwango unachotoka, haiweki kizuizi dhidi Yako na wala haitoweki bila Wewe, inafika kileleni mwa ridhaa Yako na wala ile iliyo kinara miongoni mwa himidi za viumbe Wako Kwako haifiki mkiani mwake. Una sifa njema muda wote niliojua kuhimidi, ninaoitakidi kuhimidi na uliofanywa mwanzo wa maneno ni kuhimidi. Ewe mwenye utukufu na adhama ya

kuendelea na mwenye utawala na uwezo wa kudumu, mwenye mateso makali na nguvu na mwenye kupenyeza amri na utashi, mwingi wa huruma na maghfira na Mola Mlezi wa dunia na akhera, ni neema Zako ngapi nilizonazo ambapo himidi yangu inashindwa kuifikia angalau ile iliyo ndogo kabisa, na shukrani yangu haiifikii angalau ile iliyo chini kabisa.

Ni vitendo vingapi vya wema ambavyo umenitendea, kutokana na wingi wake mawazo yangu hayavikumbuki na wala fikra zangu hazividhibiti. Ewe Mwenyezi Mungu! Msalie Nabii Wako mteule utotoni kati ya viumbe Wako, mbora wao ujanani na uzeeni, mtakasifu kushinda watakaswa wote kihulka, mkarimu kushinda wote wenye kuendelea kiukarimu, na kiumbe mtukufu kiasili, ambaye kupitia yeye umeweka wazi dalili mbalimbali, umezuia risala mbalimbali, umehitimisha unabii mbalimbali na umefungua heri mbalimbali, umemdhihirisha waziwazi na ukamtuma akiwa Nabii, Kiongozi, Mwaminifu, Mwongozaji, Muitaji Kwako, Dalili Yako na Hoja mbele Yako. Ewe Mwenyezi Mungu! Wasalie Maasumina toka katika kizazi chake na wema toka katika familia yake. Kitukuze cheo chao mbele Yako kupitia kwake, na adhimisha nafasi yao Kwako, weka vikao vyao katika urafiki wa hadhi ya juu na nyanyua daraja yao mpaka karibu na Mtume Wako, kamilisha furaha yao kwa kukutana naye na watimizie urafiki wao kupitia sehemu yake.”

Na inahimizwa kumzuru yeye (s.a.w.w.) siku tukufu na nyakati na muda wenye Baraka na hasa nyakati ambazo zinamhusu yeye (s.a.w.w.), kama vile siku ya kuzaliwa kwake nayo ni siku ya kumi na saba ya mfunguo sita, na inasemekana ni siku ya kumi na mbili ya mwezi huo. Na

siku ya kufa kwake nayo ni siku ya ishirini na nane ya mfunguo tano, na siku ya kukabidhiwa kwake unabii nayo ni siku ya ishirini na saba ya mwezi wa Rajabu.

Na siku ambazo Mwenyezi Mungu alimpa ushindi dhidi ya maadui zake au alimwepusha na shari zao kama ilivyotajwa katika historia yake. Na siku ya Maapizano yake dhidi ya Wakristo wa Najran, nayo ni siku ya ishirini na nne ya mfunguo tatu, na inasemekana ni siku ya ishirini na tano ya mwezi huo, na siku aliyohama toka Makka kwenda Madina nayo ni usiku wa kwanza wa mfunguo sita, na siku aliyolingia Madina nayo ni siku ya kumi na mbili ya mfunguo sita, na siku aliyotoka katika bonde la Abu Talib nayo ni katikati ya mwezi wa Rajabu, na siku ambayo mimba yake ilitunga, nayo ni usiku wa kumi na tisa wa mfunguo tisa, na siku aliyokwenda Miraji, nayo ni siku ya ishirini na moja ya mwezi wa Ramadhani, na inasemekana ni siku ya tisa ya ya mfunguo tatu, na inasemwa pia ni siku ya kumi na saba ya mfunguo sita, na siku aliyomuoa Khadija (r.a.) nayo ni siku ya kumi ya mfunguo sita.

Kusali kwenye nguzo ya Abu Lubabah:

Sali raka mbili kwenye nguzo ya Abu Lubabah inayojulikana kama nguzo ya toba. Abu Lubabah ni Bashir bin Abdul-Mundhir, hakujumuika na jeshi la Waislamu katika Vita vya Tabuk, nayo ni ile Vita aliyoingoza Mtume mwenyewe na akamwacha Ali Madina kama kiongozi, na akamwambia ile kauli mashuhuri: “Wewe kwangu mimi una cheo cha Harun kwa Musa.” Abu Lubabah akajutia hilo na akajifunga kwenye moja ya nguzo za Msikiti wa Mtume (s.a.w.w.) na akala yamini kwamba hatokula wala kunywa mpaka Mwenyezi Mungu akubali toba yake au afikwe na kifo.

Alibakia siku saba katika hali hiyo na akazimia mpaka Mwenyezi Mungu akamteremshia Mtume wake Aya hii: **“Na wengine waliokiri dhambi zao wakachanganya vitendo vyao vizuri na vingine vibaya, huenda Mwenyezi Mungu kapokea toba zao, hakika Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa kusamehe, Mwenye kurehemu.”** (Sura Tawba: 102), ndipo Mtume wa Mwenyezi Mungu akaja msikitini na kumfungua toka kwenye nguzo hiyo ambayo baadaye ilipewa jina lake na jina la nguzo ya toba kutokana na kukubaliwa toba yake. na inasemekana kwamba aliyekataa kujumuika na jeshi kwenda vitani alikuwa ni mtu mwingine kama ilivyo ndani ya vitabu vya tafsiri. Na inasemekana kwamba sababu ya kuteremka kwa Aya hiyo ni lile tukio lake la Bani Quraydha pale aliposema: “Ikiwa mtakubali hukumu ya Sa’d bin Ma’adh basi ni kuchinjwa.” Punde tu alipojua kuwa kamkhini Mwenyezi Mungu na Mtume wake alijutia hapo hapo.

Baada ya kusali katika nguzo hii, utasoma dua hii:

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ لَا تُهَيِّ بِالْفَقْرِ، وَلَا تُدَلِّلْنِي
 بِالذُّبَيْنِ وَلَا تُرِدِّنِي إِلَى الْهَلَكَةِ وَأَعِصِنِي كَيْ أَعْتَصِمَ وَأَصْلِحُنِي كَيْ
 أَنْصَحَ وَاهْدِنِي كَيْ أَهْتَدِيَ اللَّهُمَّ أَعِنِّي عَلَى اجْتِهَادِ نَفْسِي وَلَا
 تُعَذِّبْنِي بِسُوءِ ظَنِّي وَلَا تُهْلِكْنِي وَأَنْتَ رَجَائِي وَأَنْتَ أَهْلٌ أَنْ
 تُغْفِرَ لِي وَقَدْ أَخْطَأْتُ وَأَنْتَ أَهْلٌ أَنْ تَعْفُوَ عَنِّي وَقَدْ أَقْرَرْتُ وَأَنْتَ

أَهْلٌ أَنْ تُقِيلَ وَقَدْ عَثَرْتُ وَأَنْتَ أَهْلٌ أَنْ تُحْسِنَ وَقَدْ أَسَأْتُ
 وَأَنْتَ أَهْلُ التَّقْوَى وَالْبُغْفَرَةِ فَوَقِّفْنِي لِمَا تُحِبُّ وَتَرْضَى وَيَسِّرْ لِي
 الْيَسِيرَ وَجَنِّبْنِي كُلَّ عَسِيرٍ أَلَّهْمَّ أَغْنِنِي بِالْحَلَالِ مِنَ الْحَرَامِ
 وَبِالطَّاعَاتِ عَنِ الْمَعَاصِي وَبِالْغِنَى عَنِ الْفَقْرِ وَبِالْجَنَّةِ عَنِ النَّارِ
 وَبِالْأَبْرَارِ عَنِ الْفَجَّارِ يَا مَنْ لَيْسَ كَبَشِيرِهِ شَيْءٌ وَهُوَ السَّبِيْعُ
 الْبَصِيرُ وَأَنْتَ عَلَى كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ

“Kwa jina la Mwenyezi Mungu Mwingi wa rehema Mwenye kurehemu. Ewe Mwenyezi Mungu! Usinilize kwa ufakiri, usinidhalilishe kwa deni na wala usinirudishe kwenye maangamio, nihifadhi ili nijihifadhi, nirekebishe ili nijirekebishe na niongoze ili niongozeke. Ewe Mwenyezi Mungu! Nisaidie kupambana na nafsi yangu na wala usiniadhibu kutokana na dhana yangu mbaya, na wala usiniangamize ilihali Wewe ndio tarajio langu, Wewe ndiye mwenye uwezo wa kunighufiria, nami nimeshakosea, Wewe ndiye mwenye uwezo wa kunisamehe nami nimeshaungama, Wewe ndiye mwenye uwezo wa kuninyanyua nami nimeshajikwaa, Wewe ndiye mwenye uwezo wa kunitendea wema nami nimeshatenda uovu, na Wewe ndiye mmiliki wa taqwa na maghfira hivyo niwafikishe katika lile ulipendalo na uliridhialo, nirahisishie mepesi na niepushe na kila zito. Ewe Mwenyezi Mungu! Nitosheleze kwa halali badala ya haramu, mambo ya utiifu badala ya maasi na utajiri badala

ya ufakiri, pepo badala ya moto, na watu wema badala ya waovu. Ewe Ambaye hufanani na chochote Naye ni Msikivu Mwenye kuona, na Wewe juu ya kila kitu ni Muweza.” (Kisha omba haja yako bila shaka itajibiwa inshaallah.)

Swaumu ya Sunna ya huko Madina:

Ni Sunna kufunga huko Madina siku tatu kwa ajili ya kukidhiwa haja hata kama mtu huyo atakuwa ni msafiri. Na Swaumu hiyo inapasa iwe siku ya jumatano, alhamisi na ijumaa. Na ni Sunna kusali kwenye nguzo hii ya Abu Lubabah usiku wa jumatano na mchana wake, na kwenye nguzo inayofuatia usiku wa alhamisi na mchana wake, na kwenye nguzo iliyopo pembezoni mwa mihrabu ya Mtume (s.a.w.w.w.) usiku wa ijumaa na mchana wake. Na uomnbe haja zako za kidunia na kiakhera, na miongoni mwa dua za kuomba ni useme:

اللَّهُمَّ مَا كَانَتْ إِلَيْكَ مِنْ حَاجَةٍ شَرَعْتُ أَنَا فِي طَلِبِهَا أَوْ الْتَمَسْتُ
أَوْ لَمْ أَشْرَعْ، سَأَلْتُكَهَا أَوْ لَمْ أَسْأَلْكَهَا، فَإِنِّي أَتَوَجَّهُ إِلَيْكَ بِنَبِيِّكَ
مُحَمَّدٍ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ نَبِيِّ الرَّحْمَةِ، فِي قَضَاءِ حَوَائِجِي
صَغِيرِهَا وَكَبِيرِهَا، اللَّهُمَّ إِنِّي أَسْأَلُكَ بِعِزَّتِكَ وَقُوَّتِكَ وَقُدْرَتِكَ،
وَجَبِيحِ مَا أَحَاطَ بِهِ عِلْمُكَ، أَنْ تُصَلِّيَ عَلَيَّ عَلَى مُحَمَّدٍ وَآلِ مُحَمَّدٍ،
صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ، وَأَنْ تَفْعَلَ بِي كَذَا وَكَذَا

“Ewe Mwenyezi Mungu! Haja yoyote ambayo mimi nilianza kuitafuta au kuitaka, au sijaanza lakini nimekuomba haja hiyo au sijakuomba, basi hakika mimi naelekea Kwako kupitia Nabii Wako Muhammad (s.a.w.w.) Nabii wa rehema unikiidhie haja zangu ndogo na kubwa. Ewe Mwenyezi Mungu! Hakika mimi nakuomba kwa utukufu Wako na nguvu Zako na uwezo Wako na kila kile kilichodhibitiwa na elimu Yako, umsalie Muhammad na aali Muhammad (s.a.w.w.) na unifanyie kadha wa kadha.” (Badala ya neno *kadha wa kadha* taja haja zako inshaallah dua yako itajibiwa.)

Kusali eneo alilokuwa akisimama Jibril (Maqam Jibril):

Ni Sunna kusali Maqam Jibril, nalo ni eneo ambalo Jibril alikuwa akisimama na kuomba idhini ya kuingia kwa Mtume (s.a.w.w.), nalo ni lile la chini ya bomba lililokuwa juu ya mlango wa Fatima (a.s.), na mlango wa Fatima (a.s.) ni ule mlango uliyo pembeni mwa kaburi lake kwa yule anayeona kuwa kaburi lake limo ndani ya nyumba yake kama ilivyopokewa katika baadhi ya habari. Baada ya kusali sema:

يَا مَنْ خَلَقَ السَّمَاوَاتِ، وَمَلَأَهَا جُنُوداً مِنَ الْمُسَبِّحِينَ لَهُ مِنْ
مَلَائِكَتِهِ، وَالْمُهَجِّدِينَ لِقُدْرَتِهِ وَعَظَمَتِهِ، وَأَفْرَغَ عَلَى أَيْدِيهِمْ
حُلَلَ الْكِرَامَاتِ، وَأَنْطَقَ أَلْسِنَتَهُمْ بِضُرُوبِ اللُّغَاتِ، وَالْبَسَهُمْ
شِعَارَ التَّقْوَى، وَقَلَّدَهُمْ قَلَائِدَ التُّهَى، وَجَعَلَهُمْ أَوْفَرَ أَجْنَاسِ

خَلَقَهُ مَعْرِفَةً بِوَحْدَانِيَّتِهِ وَقُدْرَتِهِ وَجَلَالَتِهِ وَعَظَمَتِهِ، وَأَكْبَلَهُمْ
عِلْمَابِهِ، وَأَشَدَّهُمْ فِرْقًا، وَأَدْوَمَهُمْ لَهُ طَاعَةً وَخُضُوعًا وَاسْتِكَانَةً
وَخُشُوعًا، يَا مَنْ فَضَّلَ الْأَمِينَ جَبْرِيْلَ عَلَيْهِ السَّلَامُ بِخَصَائِصِهِ
وَدَرَاجَاتِهِ وَمَنَازِلِهِ، وَاخْتَارَهُ لِرُوحِهِ وَسِفَارَتِهِ وَعَهْدِهِ
وَأَمَاتَتِهِ، وَإِنْزَالِ كُتُبِهِ وَأَوَامِرِهِ عَلَى أَنْبِيَائِهِ وَرُسُلِهِ، وَجَعَلَهُ
وَاسِطَةً بَيْنَ نَفْسِهِ وَبَيْنَهُمْ،

أَسْأَلُكَ أَنْ تُصَلِّيَ عَلَيَّ مُحَمَّدٍ وَآلِ مُحَمَّدٍ، وَعَلَى جَمِيعِ
مَلَائِكَتِكَ وَسُكَّانِ سَمَاوَاتِكَ، أَعْلَمِ خَلْقِكَ بِكَ، وَأَخُوفِ خَلْقِكَ
لَكَ، وَأَقْرَبِ خَلْقِكَ مِنْكَ، وَأَعْمَلِ خَلْقِكَ بِطَاعَتِكَ، الَّذِينَ لَا
يَغْشَاهُمْ نَوْمُ الْعُيُونِ، وَلَا سَهْوُ الْعُقُولِ، وَلَا فَتْرَةُ الْأَبْدَانِ،
الْبُكَرَمِيِّينَ بِجَوَارِكَ، وَالْمُؤْتَمِنِينَ عَلَى وَحْيِكَ، الْمُجْتَنِبِينَ
الْأَفَاتِ، وَالْمُوقِينَ السَّيِّئَاتِ. اللَّهُمَّ وَاحْصِ الرُّوحَ
الْأَمِينَ، صَلَوَاتِكَ عَلَيْهِ بِأَضْعَافِهَا مِنْكَ، وَعَلَى مَلَائِكَتِكَ

الْبَقَرِيِّينَ وَطَبَقَاتِ الْكُرُوبِيِّينَ وَالرُّوحَانِيِّينَ، وَزِدْ فِي مَرَاتِبِهِ
عِنْدَكَ، وَحُقُوقِهِ الَّتِي لَهُ عَلَى أَهْلِ الْأَرْضِ، بِمَا كَانَ يُنْزَلُ بِهِ مِنْ
شَرَائِعِ دِينِكَ، وَمَا بَيَّنَّتَهُ عَلَى أَلْسِنَةِ أَنْبِيَائِكَ، مِنْ مُحَلَّلَاتِكَ
وَمُحَرَّمَاتِكَ. اللَّهُمَّ أَكْثَرُ صَلَوَاتِكَ عَلَى جَبْرِئِيلَ، فَإِنَّهُ قُدْوَةٌ
الْأَنْبِيَاءِ، وَهَادِي الْأَصْفِيَاءِ وَسَادِسُ أَصْحَابِ الْكِسَاءِ.

اللَّهُمَّ اجْعَلْ وَقُوفِي فِي مَقَامِهِ هَذَا سَبَبًا لِنُزُولِ رَحْمَتِكَ عَلَيَّ،
وَتَجَاوِزِكَ عَنِّي، رَبَّنَا إِنَّا سَبَعْنَا مُنَادِيًا يُنَادِي لِأَيَّامِنَ، أَنْ
آمَنُوا بِرَبِّكُمْ فَاْمَنَّا، رَبَّنَا فَاعْفُفْ لَنَا ذُنُوبَنَا، وَكَفِّرْ عَنَّا سَيِّئَاتِنَا
وَتَوَقَّنَا مَعَ الْأَبْرَارِ، رَبَّنَا وَآتِنَا مَا وَعَدْتَنَا عَلَى رُسُلِكَ، وَلَا
تُخْزِنَا يَوْمَ الْقِيَامَةِ، إِنَّكَ لَا تُخْلِفُ الْبِعَادَ أَيَّ جَوَادُ أَيَّ كَرِيمٍ،
أَيَّ قَرِيبُ أَيَّ بَعِيدُ، أَسْأَلُكَ أَنْ تُصَلِّيَ عَلَيَّ مُحَمَّدٍ وَآلِ
مُحَمَّدٍ، وَأَنْ تُوَقِّفَنِي لِطَاعَتِكَ، وَلَا تُزِيلَ عَنِّي نِعْمَتَكَ، وَأَنْ
تَرْزُقَنِي الْجَنَّةَ بِرَحْمَتِكَ، وَتُوسِّعَ عَلَيَّ مِنْ فَضْلِكَ، وَتُعِينَنِي

عَنْ شِرَارِ خَلْقِكَ، وَتُلْهِمَنِي شُكْرَكَ وَذِكْرَكَ، وَلَا تُخَيِّبْ يَا رَبِّ
دُعَائِي، وَلَا تَقْطَعْ رَجَائِي، بِمُحَمَّدٍ وَآلِهِ

وَأَسْأَلُكَ بِأَنَّكَ أَنْتَ اللَّهُ لَيْسَ كَمِثْلِكَ شَيْءٌ، أَنْ تَعْصِمَنِي مِنَ
الْبَهَالِكِ، وَأَنْ تَسَلِّبَنِي مِنْ آفَاتِ الدُّنْيَا وَالْآخِرَةِ، وَوَعَثَاءِ
السَّفَرِ وَسُوِّ الْمُنْقَلَبِ، وَأَنْ تَرُدَّنِي سَالِباً إِلَى وَطَنِي، بَعْدَ حَجِّ
مَقْبُولٍ وَسَعْيٍ مَشْكُورٍ وَعَمَلٍ مُتَقَبَّلٍ، وَلَا تَجْعَلْهُ آخِرَ الْعَهْدِ
مِنْ حَرَمِكَ وَحَرَمِ نَبِيِّكَ، صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ أَيُّ جَوَادٍ أَيُّ
كَرِيمٍ، أَيُّ قَرِيبٍ أَيُّ بَعِيدٍ، أَسْأَلُكَ أَنْ تُصَلِّيَ عَلَيَّ مُحَمَّدٍ وَأَهْلِ
بَيْتِهِ، وَأَنْ تَرُدَّ عَلَيَّ نِعْمَتَكَ

“Ewe Ambaye ameumba mbingu na kuzijaza jeshi miongoni mwa malaika wenye kumsabihi na wenye kutukuza uwezo Wake na adhama Yake, akaweka juu ya miili yao mapambo ya karama na akazitamkisha ndimi zao lugha mbalimbali, akawavisha vazi la uchamungu na akawavisha mkufu wa akili, akawafanya kuwa wenye maarifa ya umoja Wake, uwezo Wake, utukufu Wake na adhama Yake kushinda aina nyingine za viumbe Wake, ni wenye kumjua zaidi na ni wenye fadhaa zaidi kushinda wengine, ni wenye utii wa kudumu Kwake, unyenyekevu

na woga. Ewe Ambaye amemfadhilisha Jibril mwaminifu kwa sifa zake za pekee, daraja zake na vyeo vyake, akamteua kwa ajili ya Wahyi Wake, ubalozi Wake, ahadi Yake, amana Yake na kuteremsha vitabu Vyake na amri Zake kwa Manabii Wake na Mitume Wake, na akamfanya kiungo baina Yake mwenyewe na wao.

“Nakuomba umsalie Muhammad na aali Muhammad na malaika Zako wote na wakazi wa mbingu Zako, wale wakujua kuliko viumbe Wako wengine, wenye hofu Nawe kuliko viumbe Wako wengine, wenye ukaribu Nawe kuliko viumbe Wako wengine, wenye kukutii sana Wewe kuliko viumbe Wako wengine, ambao hawafunikwi na usingizi wa macho wala sahau ya akili, wala uchovu wa miili, wenye kukirimiwa pembezoni Mwako, wenye kuaminiwa Wahyi Wako, wenye kuepushwa na maangamizi, wenye kuingwa dhidi ya maovu. Ewe Mwenyezi Mungu! Mtengee toka Kwako maradufu ya hayo Roho mwaminifu (Jibril), sala Zako ziwe juu yake na juu ya malaika Wako waliokurubishwa na juu ya matabaka ya wale waliokurubishwa na wale maruhani. Mzidishie cheo chake Kwako na haki zake alizonazo kwa wakazi wa ardhini kutokana na zile sheria za dini Yako alizokuwa akiziteremsha, na kutokana na yale uliyoyabainisha juu ya ndimi za Manabii Wako miongoni mwa yale uliyohalalisha na uliyoharamisha. Ewe Mwenyezi Mungu! Kithirisha sala Zako juu ya Jibril kwani hakika yeye ni kigezo cha Manabii, kiongozi wa wateule na wa sita kati ya watu wa kishamia.

“Ewe Mwenyezi Mungu! Jaalia kusimama kwangu sehemu yake hii kuwe sababu ya kuteremkiwa na rehema Zako na kunisamehe Kwako. Mola Wetu Mlezi! Hakika tumemsikia mwitaji anayeitia kwenye imani kwamba: Mwaminini

Mola Wenu Mlezi, nasi tukaamini. Mola Wetu Mlezi! Tusamehe madhambi yetu na utufutie maovu yetu na utufishe pamoja na watu wema. Mola Wetu Mlezi! Na umpe uliyotuahidi kwa Mitume Wako wala usitufedheheshe Siku ya Kiyama, hakika Wewe huvunji miadi. Ewe Mkarimu! Ewe Karimu! Ewe uliye karibu! Ewe wa mbali! Nakuomba umsalie Muhammad na aali Muhammad na uniwafikishe kukutii Wewe na wala usiondoe neema Zako kwangu, na unirusuku pepo kwa rehema Zako na unizidishie fadhila Zako na unitosheleze dhidi ya waovu miongoni mwa viumbe Wako, nipe ilhamu ya kukushukuru Wewe na kukutaja Wewe, usiirudishe bila kitu dua yangu ewe Mola Mlezi na wala usivunje matumaini yangu, kwa haki ya Muhammad na aali zake.

“Na ninakuomba kwa sababu Wewe ndiye Allah ambaye haufanani na chochote unikinge dhidi ya maangamio, unisalimishe na mihangaiko ya dunia na akhera na mashaka ya safari na ubaya wa marejeo. Na unirusishe mjini kwangu nikiwa salama baada ya Hijja yenye kukubaliwa na juhudi zenye kuthaminiwa na amali zenye kupokewa, na wala usiifanye kuwa ahadi yangu ya mwisho ya kukutana na eneo Lako takatifu na eneo takatifu la Mtume Wako (s.a.w.w.). Ewe Mkarim! Ewe Karim! Ewe uliye karibu! Ewe uliye mbali! Nakuomba umsalie Muhammadna watu wa nyumba yake na unirusishe neema Zako.”

Dua ya eneo alilokuwa akisimama Jibril (*Maqam Jibril*) na hasa kwa mwenye hedhi aombe ili apate tohara:

Imepokewa kwamba mwanamke aliye katika hedhi atakapoomba dua eneo hili la *Maqam Jibril* ili apate tohara dhidi ya damu aliyोजना inshaallah itakubaliwa. Maelezo

ya Hadithi yanasema: Amepokea al-Kulayniy katika Hadithi Sahihi kutoka kwa Muawiya bin Ammar kutoka kwa Abu Abdullah (a.s.) kwamba alisema: “Mwanamke akiingia kwenye ibada zake za Hijja na hali ni mwenye hedhi, basi aoge na asimame eneo alilokuwa akisimama Jibril (Maqam Jibril), na wanawake wenzake wawe nyuma yake wakiitikia dua yake, aseme:

اللَّهُمَّ إِنِّي أَسْأَلُكَ بِكُلِّ اسْمٍ هُوَ لَكَ ، أَوْ تَسَبَّيْتَ بِهِ لِأَحَدٍ مِنْ
 خَلْقِكَ ، أَوْ اسْتَأْثَرْتَ بِهِ فِي عِلْمِ الْغَيْبِ عِنْدَكَ ، وَأَسْأَلُكَ
 بِاسْمِكَ الْأَعْظَمِ الْأَعْظَمِ ، وَبِكُلِّ حَرْفٍ أَنْزَلْتَهُ عَلَى مُوسَى ، وَبِكُلِّ
 حَرْفٍ أَنْزَلْتَهُ عَلَى عِيسَى ، وَبِكُلِّ حَرْفٍ أَنْزَلْتَهُ عَلَى مُحَمَّدٍ صَلَّى
 اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ إِلَّا أَذْهَبَتْ عَنِّي هَذَا الدَّمِ .

“Ewe Mwenyezi Mungu! Hakika mimi nakuomba kupitia kila jina ambalo ni Lako au umejiita kwalo kupitia yeyoye miongoni mwa viumbe Wako au umelipa kipaumbele Kwako katika elimu ya ghaibu, na ninakuomba kupitia jina Lako tukufu Al-'Adhamu, na kupitia kila herufi uliyoiteremsha kwa Musa, na kupitia kila herufi uliyoiteremsha kwa Isa, na kupitia kila herufi uliyoiteremsha kwa Muhammad (s.a.w.w.), ila uwe umeniondolea ghamu hii.”

Utakapotaka kuingia Msikiti Mtukufu au Msikiti wa Mtume (s.a.w.w.) fanya kama hivyo.(akaendelea kueleza mpaka akasema):- Mwanamke mwenye hedhi

hatamwomba Mwenyezi Mungu kwa dua ya damu eneo hilo na hali ameelekea Kibla ila atapata tohara.”

Nasema: Huenda makusudio ya mwenye hedhi hapa ni mwenye istihadha isiyokatika, kama alivyosema al-Majlisiy katika kitabu *al-Bihar*.

Ibnu Qawalayhi amepokea kwa sanadi zake kutoka kwa Muhammad bin Mas'ud kwamba alisema: Nilimwona as-Sadiq (a.s.) akiwa ameweka mkono wake mtukufu juu ya kaburi la Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) na akasema:

أَسْأَلُ اللَّهَ الَّذِي اجْتَبَاكَ وَاخْتَارَكَ وَهَدَاكَ وَهَدَى بِكَ أَنْ
يُصَلِّيَ عَلَيْكَ [ثم قال: إِنَّ اللَّهَ وَمَلَائِكَتَهُ يُصَلُّونَ عَلَى النَّبِيِّ
يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا صَلُّوا عَلَيْهِ وَسَلِّمُوا تَسْلِيمًا

“Namuomba Mwenyezi Mungu Ambaye alikuteua, alikuchagua na alikuongoza na akaongoza kupitia Kwako, akusalie wewe. Hakika Mwenyezi Mungu na Malaika Wake humsalia Mtume, enyi mlioamini! Msalieni na muombeeni amani.”

Ukimaliza kuomba dua kwenye kaburi tukufu nenda mimbarini na simama hapo, muhimidi Mwenyezi Mungu na mtukuze kisha omba haja yako. Na kwa kuwa mimbari ya asili hivi sasa haipo lakini iliyopo hivi sasa imechukua nafasi ya ile ya asili basi si vibaya kufanya hivyo kwa kutaraji kupata utakacho, kisha utakwenda maqam Nabii na usali uwezavyo.

FASLU YA NNE

FADHILA ZA KUMZURU ZAHRA (A.S.)

Allama al-Majlisiy ametaja kutoka kwenye kitabu *Musbahul-An'war* kutoka kwa Fatima (a.s.) kwamba alisema: “Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) alisema: 'Ewe Fatima! Atakayekusalia Mwenyezi Mungu atamghufiria na atamkutanisha nami pale nitakapokuwepo Peponi.”

Wametofautiana kuhusu pale lilipo kaburi lake, baadhi wakasema kuwa amezikwa katika eneo (kitalu) lililopo kati ya mimbari na kaburi la Mtume (s.a.w.w.). Wengine wakasema amezikwa ndani ya nyumba yake, nalo ni eneo lililopo mbele ya mlango wa Jibril, na dhahiri ni kwamba dirisha linalozunguka kaburi la Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) ndilo linalozunguka chumba na nyumba ya Fatima (a.s.), na huenda kutokana na upanuzi wa Msikiti hivi sasa kaburi lake limekuwa Msikitini, kama ilivyo katika riwaya ya al-Bazantiy alisema: “Nilimuuliza Ridha (a.s.) kuhusu kaburi la Fatima (a.s.) akasema: Alizikwa ndani ya nyumba yake, Bani Umaiyya walipofanya upanuzi wa Msikiti akawa msikitini.”

Na inasemekana kwamba alizikwa huko Baqii, na maswahiba zetu wengi wanasema kuwa alizikwa eneo (kitalu) lililopo kati ya mimbari na kaburi la Mtume (s.a.w.w.). Ni hali nzito kwa vipenzi wasijue kaburi la binti ya Nabii wao hasa ukizingatia kwamba Mtume baada ya kufa hakuacha ila binti mmoja tu.

Ni Sunna kumzuru Fatima (a.s.) sehemu tatu:

Ziyara ya kwanza:

يَا مُبْتَحَنَةً اُمْتَحَنَكَ اللهُ الَّذِي خَلَقَكَ قَبْلَ أَنْ يَخْلُقَكَ،
فَوَجَدَكَ لَهَا اُمْتَحَنَكَ صَابِرَةً، وَزَعَمْنَا أَنَّا لِكَ أَوْلِيَاءُ وَمُصَدِّقُونَ
وَصَابِرُونَ لِكُلِّ مَا آتَانَا بِهِ أَبُوكَ صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَآتَى بِهِ
وَصِيَّهُ، فَإِنَّا نَسْأَلُكَ إِن كُنَّا صَدَقْنَاكَ إِلَّا الْحَقَّتْنَا بِتَصَدِّقِنَا
لَهُمَا لِنُبَشِّرَهُ أَنْفُسَنَا بِأَنَّا قَدْ طَهَّرْنَا بِوَلَايَتِكَ

“Ewe mtahiniwa! Mwenyezi Mungu aliyekuumba alikutahini kabla hajakuumba, akakukuta ni mwenye subira kwa yale aliyokutahini nayo. Na tukadai kwamba sisi ni vipenzi vyako, ni wenye kusadikisha na ni wenye subira dhidi ya kila alilotuletea baba yako (s.a.w.w.) na kila alilotuletea Wasii wake, hivyo sisi tunakuomba ikiwa kweli tumekusadikisha utukutanishe nao kupitia usadiki wetu ili tuzipe habari njema nafsi zetu kwamba tumetakasika kupitia mapenzi yetu kwako.”

Ni Sunna useme:

السَّلَامُ عَلَيْكَ يَا بِنْتَ رَسُولِ اللهِ، السَّلَامُ عَلَيْكَ يَا بِنْتَ نَبِيِّ
الله، السَّلَامُ عَلَيْكَ يَا بِنْتَ حَبِيبِ اللهِ، السَّلَامُ عَلَيْكَ يَا بِنْتَ

خَلِيلِ اللَّهِ، السَّلَامُ عَلَيْكَ يَا بِنْتَ صَغِيِّ اللَّهِ، السَّلَامُ عَلَيْكَ يَا
بِنْتَ أَمِينِ اللَّهِ، السَّلَامُ عَلَيْكَ يَا بِنْتَ خَيْرِ خَلْقِ اللَّهِ، السَّلَامُ
عَلَيْكَ يَا بِنْتَ أَفْضَلِ أَنْبِيَاءِ اللَّهِ وَرُسُلِهِ وَمَلَائِكَتِهِ، السَّلَامُ
عَلَيْكَ يَا بِنْتَ خَيْرِ الْبَرِيَّةِ، السَّلَامُ عَلَيْكَ يَا سَيِّدَةَ نِسَاءِ
الْعَالَمِينَ مِنَ الْأُولِينَ وَالْآخِرِينَ،

السَّلَامُ عَلَيْكَ يَا رَوْجَةَ وَلِيِّ اللَّهِ وَخَيْرِ الْخَلْقِ بَعْدَ رَسُولِ اللَّهِ،
السَّلَامُ عَلَيْكَ يَا أُمَّ الْحَسَنِ وَالْحُسَيْنِ سَيِّدَيْ شَبَابِ أَهْلِ
الْجَنَّةِ، السَّلَامُ عَلَيْكَ أَيَّتُهَا الصِّدِّيقَةُ الشَّهِيدَةُ، السَّلَامُ
عَلَيْكَ أَيَّتُهَا الرِّضِيَّةُ الْبُرْضِيَّةُ، السَّلَامُ عَلَيْكَ أَيَّتُهَا الْفَاضِلَةُ
الرِّزْكَيَّةُ، السَّلَامُ عَلَيْكَ أَيَّتُهَا الْحَوْرَاءُ الْأَنْسِيَّةُ، السَّلَامُ
عَلَيْكَ أَيَّتُهَا النَّعِيمَةُ النَّعِيمَةُ، السَّلَامُ عَلَيْكَ أَيَّتُهَا الْمُحَدَّثَةُ
الْعَلِيَّةُ، السَّلَامُ عَلَيْكَ أَيَّتُهَا الْمَظْلُومَةُ الْمَعْصُومَةُ، السَّلَامُ

عَلَيْكَ أَيُّهَا الْبُظْهَدَةُ الْبُقْهُورَةُ، أَسْلَامُ عَلَيْكَ يَا فَاطِمَةَ بِنْتَ
رَسُولِ اللَّهِ وَرَحْمَةُ اللَّهِ وَبَرَكَاتُهُ،

صَلَّى اللَّهُ عَلَيْكَ وَعَلَى رُوحِكَ وَبَدَنِكَ، أَشْهَدُ أَنَّكَ مَضَيْتِ عَلَى
بَيِّنَةٍ مِنْ رَبِّكَ، وَأَنَّ مَنْ سَرَّكَ فَقَدْ سَرَّ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ
عَلَيْهِ وَآلِهِ، وَمَنْ جَفَاكَ فَقَدْ جَفَا رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ
وَآلِهِ، وَمَنْ آذَاكَ فَقَدْ آذَى رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ،
وَمَنْ وَصَلَكَ فَقَدْ وَصَلَ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ، وَمَنْ
قَطَعَكَ فَقَدْ قَطَعَ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ، لِأَنَّكَ بِضَعَةٌ
مِنْهُ وَرُوحُهُ الَّذِي بَيْنَ جَنْبَيْهِ،

أَشْهَدُ اللَّهُ وَرُسُلُهُ وَمَلَائِكَتُهُ أَنِّي رَاضٍ عَمَّنْ رَضِيَتْ عَنْهُ،
سَاخِطٌ عَلَى مَنْ سَخِطَ عَلَيْهِ مُتَبَرِّئٌ وَمِنْ تَبَرَّاتٍ مِنْهُ، مُوَالٍ
لِئِنَّ وَالِيَّتِ، مُعَادٍ لِئِنَّ عَادِيَّتِ، مُبْغِضٌ لِئِنَّ أَبْغَضْتِ، مُحِبٌّ
لِئِنَّ أَحْبَبْتِ، وَكَفَى بِاللَّهِ شَهِيداً وَحَسِيباً وَجَازِياً وَمُثِيباً

“Amani iwe juu Yako ewe binti wa Mtume wa Mwenyezi Mungu! Amani iwe juu Yako ewe binti wa Nabii wa Mwenyezi Mungu! Amani iwe juu Yako ewe binti wa hababi wa Mwenyezi Mungu! Amani iwe juu Yako ewe binti wa kipenzi cha Mwenyezi Mungu! Amani iwe juu Yako ewe binti wa mteule wa Mwenyezi Mungu! Amani iwe juu Yako ewe binti wa mwaminifu wa Mwenyezi Mungu! Amani iwe juu Yako ewe binti wa mbora wa viumbe wa Mwenyezi Mungu! Amani iwe juu Yako ewe binti wa mbora wa Manabii wa Mwenyezi Mungu, Mitume Wake na Malaika Wake! Amani iwe juu Yako ewe binti wa mwema wa viumbe! Amani iwe juu Yako ewe mbora wa wanawake wote wa ulimwenguni kuanzia wa mwanzo hadi wa mwisho!

“Amani iwe juu Yako ewe mke wa Walii na kiumbe bora baada ya Mtume wa Mwenyezi Mungu! Amani iwe juu Yako ewe mama mzazi wa Hasan na Husain mabwana wawili wa vijana wa peponi! Amani iwe juu Yako ewe mkweli uliyekufa kishahidi! Amani iwe juu Yako ewe mwenye kuridhia mwenye kuridhiwa! Amani iwe juu Yako ewe mwema mtakasifu! Amani iwe juu Yako ewe Hurulaini wa kibinadamu! Amani iwe juu Yako ewe mchamungu uliye msafi! Amani iwe juu Yako ewe msimuliwa mjuzi! Amani iwe juu Yako ewe mdhulumiwa mporwaji! Amani iwe juu Yako ewe mwenye kukandamizwa mwenye kuonewa! Amani iwe juu Yako ewe Fatima binti ya Mtume wa Mwenyezi Mungu na pia rehema za Mwenyezi Mungu na Baraka Zake!

“Mwenyezi Mungu akusalie wewe, roho yako na mwili wako. Nashahidilia kwamba hakika wewe umepita juu ya hoja toka kwa Mola Wako Mlezi, na kwamba mwenye kukufurahisha wewe bila shaka amemfurahisha Mtume wa

Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.), na mwenye kukutenga wewe bila shaka amemtenga Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.), na mwenye kukuudhi wewe bila shaka amemuudhi Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.), na mwenye kuendeleza mahusiano nawe bila shaka ameendeleza mahusiano na Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.), na mwenye kukata mahusiano nawe bila shaka amekata mahusiano na Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.), kwa sababu wewe ni pande la nyama yake na ni roho yake anayotembea nayo.

“Namshuhudilishia Mwenyezi Mungu, Mitume Wake na malaika Wake kuwa kwa hakika mimi ni mwenye kuwa radhi na yule uliyokuwa radhi naye, na si mwenye kuwa radhi na yule usiyokuwa radhi naye, ni mwenye kujitenga na wale uliojitenga nao, ni mwenye kuwapenda wale uliowapenda, ni mwenye uadui na wale uliokuwa na uadui nao, ni mwenye kuchukizwa na wale uliochukizwa nao, na ni mwenye mapenzi na wale uliokuwa na mapenzi nao. Na Mwenyezi Mungu atosha kabisa kuwa Shahidi, Mwenye kuhasibu, Mwenye kulipa na Mwenye kutoa thawabu.”

Kisha msalie Nabii (s.a.w.w.) na Maimamu (a.s.), na ni Sunna baada ya hapo usali rakaa mbili kwa ajili ya ziyara na uzitowe thawabu zake zawadi kwa Fatima Zahra (a.s.), kisha uombe dua hii:

اللَّهُمَّ إِنِّي أَتُوجَّهُ إِلَيْكَ بِنَبِيِّنَا مُحَمَّدٍ، وَبِأَهْلِ بَيْتِهِ صَلَوَاتِكَ عَلَيْهِمْ، وَأَسْأَلُكَ بِحَقِّكَ الْعَظِيمِ الَّذِي لَا يَعْلَمُ كُنْهَهُ سِوَاكَ، وَأَسْأَلُكَ بِحَقِّ مَنْ حَقُّهُ عِنْدَكَ عَظِيمٌ، وَبِأَسْمَائِكَ الْحُسْنَى الَّتِي

أَمَرْتَنِي أَنْ أَدْعُوكَ بِهَا، وَأَسْأَلُكَ بِاسْمِكَ الْأَعْظَمِ الَّذِي أَمَرْتَ بِهِ
إِبْرَاهِيمَ، أَنْ يَدْعُوَ بِهِ الطَّيْرَ فَأَجَابْتَهُ، وَبِاسْمِكَ الْعَظِيمِ الَّذِي
قُلْتَ لِلنَّارِ “ كُونِي بَرْدًا وَسَلَامًا عَلَىٰ إِبْرَاهِيمَ ” ، فَكَانَتْ بَرْدًا ،
وَبِأَحَبِّ الْأَسْمَاءِ إِلَيْكَ وَأَشْرَفِهَا وَأَعْظَمِهَا لَدَيْكَ ، وَأَسْرَعِهَا إِجَابَةً
وَأَنْجَحِهَا طَلِبَةً ، وَبِأَنْتَ أَهْلُهُ وَمُسْتَحِقُّهُ وَمُسْتَوْجِبُهُ ،

وَأَتَوَسَّلُ إِلَيْكَ وَأَرْغَبُ إِلَيْكَ ، وَأَتَضَرَّعُ إِلَيْكَ ، وَاللِّحُّ عَلَيْكَ ،
وَأَسْأَلُكَ بِكِتَابِكَ الَّتِي أَنْزَلْتَهَا عَلَىٰ أَنْبِيَائِكَ وَرُسُلِكَ صَلَوَاتِكَ
عَلَيْهِمْ ، مِنَ التَّوْرَةِ وَالْإِنْجِيلِ وَالزَّبُورِ وَالْقُرْآنِ الْعَظِيمِ ، فَإِنَّ
فِيهَا اسْمَكَ الْأَعْظَمَ ، وَبِهَا فِيهَا مِنْ أَسْمَائِكَ الْعُظْمَى ، أَنْ
تُصَلِّيَ عَلَىٰ مُحَمَّدٍ وَآلِ مُحَمَّدٍ ، وَأَنْ تَفَرِّجَ عَنِ آلِ مُحَمَّدٍ
وَشِيَعَتِهِمْ وَمُحِبِّيهِمْ وَعَنِّي ، وَتَفْتَحَ أَبْوَابَ السَّمَاءِ لِدُعَائِي ،
وَتَرْفَعَهُ فِي عِلِّيِّينَ ، وَتَأْذَنَ لِي فِي هَذَا الْيَوْمِ وَفِي هَذِهِ السَّاعَةِ
بِفَرَاجِي وَإِعْطَاءِ أَمَلِي وَسُؤْلِي فِي الدُّنْيَا وَالْآخِرَةِ ،

يَا مَنْ لَا يَعْلَمُ أَحَدٌ كَيْفَ هُوَ وَقُدِّرَتْهُ إِلَّا هُوَ، يَا مَنْ سَدَّ الْهَوَاءَ
 بِالسَّيِّئِ، وَكَبَسَ الْأَرْضَ عَلَى الْمَاءِ، وَاخْتَارَ لِنَفْسِهِ أَحْسَنَ
 الْأَسْمَاءِ، يَا مَنْ سَمَى نَفْسَهُ بِالِاسْمِ الَّذِي تُقْضَى بِهِ حَاجَةٌ مَنْ
 يَدْعُوهُ، أَسْأَلُكَ بِحَقِّ ذَلِكَ الْاسْمِ، فَلَا شَفِيعَ أَقْوَى لِي مِنْهُ، أَنْ
 تُصَلِّيَ عَلَيَّ مُحَمَّدٍ وَآلِ مُحَمَّدٍ، وَأَنْ تُقْضِيَ لِي حَوَائِجِي،
 وَتُسَبِّحَ بِمُحَمَّدٍ وَعَلَى وَفَاطِمَةَ وَالْحَسَنِ وَالْحُسَيْنِ، وَعَلَى بُنِ
 الْحُسَيْنِ، وَمُحَمَّدِ بْنِ عَلِيٍّ وَجَعْفَرِ بْنِ مُحَمَّدٍ، وَمُوسَى بْنِ
 جَعْفَرٍ وَعَلَى بُنِ مُوسَى، وَمُحَمَّدِ بْنِ عَلِيٍّ وَعَلَى بُنِ مُحَمَّدٍ،
 وَالْحَسَنِ بْنِ عَلِيٍّ وَالْحُجَّةِ الْبُنْتَنَظَرِ لِذُنُكَ، صَلَوَاتِكَ وَسَلَامِكَ
 وَرَحْمَتِكَ وَبَرَكَاتِكَ عَلَيْهِمْ صَوْتِي لِيُشْفِعُوا لِي إِلَيْكَ، وَتُشَفِّعَهُمْ
 لِي، وَلَا تُرَدَّنِي خَائِبًا، بِحَقِّ لَا إِلَهَ إِلَّا أَنْتَ.

“Ewe Mwenyezi Mungu! Hakika mimi naelekea Kwako kupitia Nabii wetu Muhammad (s.a.w.w.) na watu wa nyumba yake sala Zako ziwe juu yao. Na ninakuomba kupitia haki Yako adhimu ambayo hakuna ajuaye kiini chake ila Wewe. Na ninakuomba kupitia haki ya yule ambaye haki yake Kwako ni adhimu, na kupitia majina

Yako mema ambayo umeniamuru nikuombe kwayo. Na ninakuomba kupitia jina Lako tukufu mno ambalo ulimwamrisha Ibrahim kupitia kwalo amwite ndege na ukawa umemjibu, na kupitia jina Lako tukufu ambalo kupitia kwalo uliuambia moto kuwa baridi na salama kwa Ibrahim na ukawa baridi na salama, na kupitia jina ulipendalo mno kati ya majina Yako, ambalo ni tukufu kuliko yote na adhimu kuliko yote Kwako, ambalo hutoa jibu haraka kuliko yote na hufanikisha ombi kuliko yote, na kupitia lile ambalo Wewe ndiye mwenye nalo, mwenye kustahiki na mwenye kuwajibika nalo.

“Na ninatawassali Kwako, ninaelekea Kwako kwa shauku, ninanyenyekea na ninakusisitiza. Na ninakuomba kupitia vitabu Vyako ambavyo umeviteremsha kwa Manabii Wako na Mitume Wako (a.s.) kuanzia Taurati, Injili, Zaburi hadi Qur’an Tukufu, kwani hakika humo mna jina Lako tukufu mno, na kupitia majina Yako matukufu yaliyomo humo, umsalie Muhammad na aali Muhammad na uwape faraja aali Muhammad, wafuasi wao, vipenzi vyao na mimi mwenyewe, uifungulie dua yangu milango ya mbinguni na uiinue hadi katika wale walio juu kabisa, na utoe idhini kwa ajili yangu leo hii na katika saa hii kwa kunipa faraja, kunipa matumaini yangu na ombi langu duniani na akhera.

“Ewe Ambaye hakuna yeyote ajuaye jinsi Yeye alivyo, na uwezo Wake ila Yeye mwenyewe! Ewe Ambaye aliiziba hewa kupitia mbingu na akaiweka ardhi juu ya maji na akajichagulia mwenyewe majina mazuri! Ewe Ambaye alijiita kwa jina ambalo kwalo haja za mwenye kumwomba hukidhiwa! Ninakuomba kupitia haki ya jina hilo, kwani sina mwombezi mwenye nguvu kuliko lenyewe, umsalie Muhammad na aali Muhammad na unikidhie haja zangu na usikie sauti yangu kupitia Muhammad, Ali, Fatima, Hasan,

Husein, Ali bin Husein, Muhammad bin Ali, Ja'far bin Muhammad, Musa bin Ja'far, Ali bin Musa, Muhammad bin Ali, Ali bin Muhammad, Hasan bin Ali na al-Huja mwenye kungojea idhini Yako, sala Zako, salamu Zako, rehema Zako na Baraka Zako viwe juu yao, ili waniombee Kwako na uwape ruhusa ya kuniombea, na wala usinirudishe bila kufanikiwa, kwa haki ya tamko: Hapana mungu ila Wewe.”

Ziyara ya Pili:

Ameitaja Sayyid ibnu Tawuus (r.a):

السَّلَامُ عَلَيْكَ يَا سَيِّدَةَ نِسَاءِ الْعَالَمِينَ ، السَّلَامُ عَلَيْكَ يَا
وَالِدَةَ الْحُجَجِ عَلَى النَّاسِ أَجْمَعِينَ ، السَّلَامُ عَلَيْكَ أَيَّتُهَا
الْبَطْلُومَةُ الْمَنْوُوعَةُ حَقُّهَا. اللَّهُمَّ صَلِّ عَلَى أُمَّتِكَ وَابْنَةِ نَبِيِّكَ
وَرَوْجَةِ وَصِيِّ نَبِيِّكَ صَلَاةً تُزَلِّفُهَا فَوْقَ زُلْفَى عِبَادِكَ الْبُكْرَمِينَ
مِنْ أَهْلِ السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضِينَ.

“Amani iwe juu Yako ewe mbora wa wanawake wote wa ulimwenguni! Amani iwe juu Yako ewe mzazi wa wale walio hoja juu ya watu wote! Amani iwe juu Yako ewe mdhulumiwa mzuiliwa haki yake! Ewe Mwenyezi Mungu! Msalie mja Wako wa kike na binti ya Nabii Wako na mke wa Wasii wa Nabii Wako, sala utakazozipa daraja kushinda daraja la waja Wako wenye kukirimiwa miongoni mwa wakazi wa mbinguni na ardhini.”

Imepokewa kwamba atakayemzuru (a.s.) kupitia ziyara hii na akaomba maghfira kwa Mwenyezi Mungu basi Mwenyezi Mungu atamghufiria dhambi zake na kumwingiza peponi. Na baadhi ya ulamaa wameona ni Ziyara makhsusi kwa ajili ya siku ya kufa kwake, yaani siku ya tatu ya mfunguo tisa.

Katika kumsalia sema:

اللَّهُمَّ صَلِّ عَلَى الصِّدِّيقَةِ فَاطِمَةَ الزَّكِيَّةِ حَبِيبَةَ حَبِيبِكَ
وَنَبِيِّكَ، وَأُمَّرِ أَحِبَّائِكَ وَأَصْفِيَاءِكَ، الَّتِي اتَّجَبْتَهَا وَفَضَّلْتَهَا
وَاخْتَرْتَهَا عَلَى نِسَاءِ الْعَالَمِينَ، اللَّهُمَّ كُنِ الطَّالِبَ لَهَا مِنْ
ظَلَمِهَا وَاسْتَخَفَّ بِحَقِّهَا، وَكُنِ الشَّائِرَ لِلَّهِمَّ بِدَمِ أَوْلَادِهَا،
اللَّهُمَّ وَكَمَا جَعَلْتَهَا أُمَّرَ أَيْبَةِ الْهُدَى، وَحَلِيلَةَ صَاحِبِ الْوَأْدِ،
وَالْكَرِيمَةَ عِنْدَ الْبَلَاءِ الْأَعْلَى، فَصَلِّ عَلَيْهَا وَعَلَى أُمَّهَا صَلَاةً
تُكْرَمُ بِهَا وَجَهَ أَبِيهَا مُحَمَّدَ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ، وَتُقْرَأُ بِهَا
أَعْيُنَ ذُرِّيَّتِهَا، وَأَبْلِغْهُمْ عَنِّي فِي هَذِهِ السَّاعَةِ أَفْضَلَ التَّحِيَّةِ
وَالسَّلَامِ.

“Ewe Mwenyezi Mungu! Msalie mkweli Fatima mtakasifu kipenzi cha hababi Wako na Nabii Wako, na mama wa

vipenzi Vyako na wateule Wako ambaye umemteua na kumfadhilisha na kumchagua kuwa bora kushinda wanawake wote wa ulimwenguni. Ewe Mwenyezi Mungu! Kuwa Mwenye kuomba haki yake toka kwa aliyemdhulumu na akapuza haki yake, na kuwa mlipiza kisasi wa damu ya wanawe ewe Mwenyezi Mungu. Ewe Mwenyezi Mungu! Kama ulivyomfanya kuwa mama wa Maimamu wa uongofu, mke wa mshika bendera ya Mtume na mheshimiwa kwenye mkutano mtukufu, hivyo hivyo msalie yeye na mama yake sala ambayo kwayo utaupa heshima uso wa baba yake Muhammad (s.a.w.w.) na kutuliza macho ya kizazi chake, na niwafikishe katika saa hii maamkizi bora na salamu kutoka kwangu.”

Ni wazi kwamba kumzuru (a.s.) nyakati, saa tukufu na muda ulio makhsusi kwake ni bora zaidi na ni mnasaba, kama vile siku ya kuzaliwa kwake ambayo ni siku ya ishirini ya mfunguo tisa au siku ya kumi ya mwezi huo kwa mujibu wa baadhi ya kauli, na siku ya kufariki kwake ambayo ni siku ya tatu ya mfunguo tisa au siku nyingine kama ilivyo katika baadhi ya riwaya. Na siku ya kuolewa kwake na Amirul-Muuminina (a.s.), nayo ni katikati ya mwezi wa Rajabu au mwanzoni mwa mfunguo tatu au siku ya sita ya mwezi huo, au usiku wa kupelekwa kwa mumewe nao ni usiku wa ishirini na moja wa mfunguo nne. Na pia siku nyinginezo ambazo humo ilidhihiri karama na fadhila yake, kama vile siku ya maapizano na siku ya kuteremka Sura Dahri ambayo ni siku ya ishirini na tano ya mfunguo tatu, na siku nyingine zenye minasaba inayomhusu.

FASLU YA TANO

KUWAZURU MAIMAMU (A.S.) HUKO BAQII

Allama al-Majlisiy (r.a) amesema katika Hadithi kutoka kwa Abdullah bin Abbas kutoka kwa Mtume (s.a.w.w.) kwamba alisema: “Atakayemzuru Hasan huko Baqii basi nyayo zake zitathibiti kwenye Sirati siku ambayo nyayo zitateleza.” Na katika kitabu *al-Muqnia* imepokewa kutoka kwa as-Sadiq (a.s.) kwamba alisema: “Atakayenizuru Mwenyezi Mungu atamghufiria dhambi zake na hatokufa fakiri.”

Na Ibnu Qawalayhi ametaja katika kitabu *al-Kamil* kwamba imepokewa kutoka kwa Hisham bin Salim alisema katika Hadithi ndefu kwamba as-Sadiq (a.s.) alijiwa na mtu akasema: “Je mzazi wako hufanyiwa ziara?”

Akasema: Ndio.

Akasema: “Atapata nini mwenye kumzuru?”

Akasema: “Pepo ikiwa anafuata uimamu wake.”

Akasema: “Atapata nini atakayeacha kwa kutompenda?”

Akasema: “Ni majuto siku ya majuto.”

Na katika kitabu *al-Fusuul* cha Sayyid al-Murtaza amenukuu kutoka kwa Sheikh wake al-Mufid (r.a.) kwamba alisema: Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) alimwambia Hasan (a.s.): “Atakayekuzuru baada ya kifo chako au akamzuru baba yako au ndugu yako atapata pepo.”

Sehemu za kuzuru na maeneo matakatifu huko Baqii:

Kwanza: Makaburi ya Maimamu (a.s.):

1. Kaburi la Imam Hasan bin Ali (a.s.)
2. Kaburi la Imam Zainul-Abidin Ali bin Husein (a.s.)
3. Kaburi la Imam Muhammad bin Ali al-Baqir (a.s.)
4. Kaburi la Imam Ja'far bin Muhammad as-Sadiq (a.s.)

Makaburi haya manne yapo sehemu moja.

Pili: Makaburi mengine nayo ni kwa utaratibu huu:

1. Kaburi la Abbas bin Abdul-Mutalib, ami yake Mtume (s.a.w.w.)
2. Kaburi la Fatima binti Asad mama mzazi wa Amirul-Muuminina Ali (a.s.)

Makaburi haya mawili yameungana na makaburi ya Maimamu huko Baqii, na huenda hata kaburi la Fatima Zahrau (a.s.) likawepo eneo hili.

Tatu: Makaburi ya mabinti wa Mtume wa Mwenyezi Mungu: Nao ni Zainab, Kulthum na Ruqayyah. Makaburi yao yapo karibu na makaburi ya Maimamu huko Baqii.

Nne: Makaburi matatu yaliyopo karibu na mlango wa kutokea: Nayo ni ya shangazi wawili wa Mtume (s.a.w.w.) na Saiyyida Ummul-Banina mama yake na Abul-Fadhli Abbas (a.s.).

Tano: Kaburi la Abdullah bin Ja'far Tayyari: Hili lipo sehemu moja pamoja na kaburi la ami yake Aqil bin Abu Talib, na la Sufyan bin al-Harith.

Sita: Kaburi la Ibrahim mtoto wa Mtume (s.a.w.w.): Hili lipo karibu na mlango wa kuingilia.

Saba: Makaburi ya wakeze Mtume (s.a.w.w.).

Nane: Kaburi la Ismail mtoto wa Imam Ja'far as-Sadiq (a.s.): Hili lilikuwa nje ya Baqii, na baadaye mwili wake ukahamishiwa ndani ya Baqii.

Tisa: Kaburi la Sayyida Halima Sa'adiyya, naye ni yule aliyemnyonyesha Mtukufu Mtume (s.a.w.w.): Kaburi lake lipo mwishoni mwa Baqii.

Kumi: Makaburi ya wahanga wa tukio la Hura na wahanga wa Vita vya Uhudi: Katika uwanja huu mtukufu wamezikwa maswahaba na tabiina wengi, na hakuna Ziyara makhsusi inayowahusu wao hivyo inatosha salamu yoyote ile baada ya kuwasomea sehemu fulani ya Qur'an. Hizi hapa Ziyara ambazo ni Sunna kwa ajili ya maeneo haya matukufu, lakini kabla ya kuanza kusoma ziyara ni Sunna kuomba idhini, hapa tutataja namna mbili za kuomba idhini:

Aina ya kwanza ya kuomba idhini kwa ajili ya Ziyara:

Utasimama kwenye mlango wa Baqii na useme:

اللَّهُمَّ إِنِّي وَقَفْتُ عَلَى بَابٍ مِنْ أَبْوَابِ بُيُوتِ نَبِيِّكَ صَلَوَاتِكَ
 عَلَيْهِ وَآلِهِ، وَقَدْ مَنَعْتَ النَّاسَ أَنْ يَدْخُلُوا إِلَّا بِإِذْنِهِ، فَقُلْتُ يَا
 أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا لَا تَدْخُلُوا بُيُوتَ النَّبِيِّ إِلَّا أَنْ يُؤْذَنَ لَكُمْ،
 اللَّهُمَّ إِنِّي أَعْتَقِدُ حُرْمَةَ صَاحِبِ هَذَا الْمَشْهَدِ الشَّرِيفِ فِي غَيْبَتِهِ
 كَمَا أَعْتَقِدُهَا فِي حَضْرَتِهِ، وَأَعْلَمُ أَنَّ رَسُولَكَ وَخُلَفَاءَكَ عَلَيْهِمُ
 السَّلَامُ أَحْيَاءٌ عِنْدَكَ يُرْزَقُونَ، يَرُونَ مَقَامِي، وَيَسْمَعُونَ كَلَامِي،
 وَيَرُدُّونَ سَلَامِي، وَأَنَّكَ حَاجَبْتَنِي عَنْ سَمْعِي كَلَامَهُمْ، وَفَتَحْتَ بَابَ
 فَهْمِي بِلَذِيذِ مُنَاجَاتِهِمْ، وَإِنِّي أَسْتَأْذِنُكَ يَا رَبِّ أَوَّلًا وَأَسْتَأْذِنُ
 رَسُولَكَ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ ثَانِيًا، وَأَسْتَأْذِنُ خَلِيفَتَكَ الْإِمَامَ
 الْبَغْرُوضَ عَلِيَّ طَاعَتُهُ حَسَنُ بَنِ عَلِيٍّ، عَلِيُّ بْنُ حُسَيْنٍ، مُحَمَّدُ
 بْنُ عَلِيٍّ، وَجَعْفَرُ بْنُ مُحَمَّدٍ عَلَيْهِ السَّلَامُ وَالْمَلَائِكَةَ الْمُرْسَلِينَ
 بِهَذِهِ الْبُقْعَةِ الْمُبَارَكَةِ ثَالِثًا، أَدْخُلْ يَا رَسُولَ اللَّهِ، أَدْخُلْ يَا
 حُجَّاجَ اللَّهِ أَدْخُلْ يَا مَلَائِكَةَ اللَّهِ الْمُقَرَّبِينَ الْمُتَقِيِينَ فِي هَذَا

الشَّهَدِ، فَأَذِنَ لِي يَا مَوْلَايَ فِي الدُّخُولِ أَفْضَلَ مَا أَذِنْتَ لِأَحَدٍ
 مِنْ أَوْلِيَاءِكَ، فَإِنَّ لَمْ أَكُنْ أَهْلًا لِدِينِكَ فَأَنْتَ أَهْلٌ لِدِينِكَ

“Ewe Mwenyezi Mungu! Nimesimama kwenye mlango miongoni mwa milango ya nyumba za Nabii Wako, sala Zako na salamu ziwe juu yake na juu ya aali zake, na bila shaka uliwazuia watu wasiingie humo ila kwa idhini yake, ukasema: **“Enyi mlioamini! Msiingie nyumba za Nabii ila mtakapopewa idhini.”** Ewe mwenyezi Mungu! Hakika mimi naitakidi utukufu wa wenye makaburi haya matukufu wakati hawapo, kama ninavyoitakidi utukufu huo wakati wa hadhira yao. Na ninajua vilivyo kwamba Mtume Wako na Makhalifa Wako (a.s.) wangali hai, wako kwako wanaruzukiwa, wanaona kisimamo changu, wanasikia maneno yangu na wananjibu salamu yangu. Na hakika Wewe umezuia nisisikie maneno yao na umefungua mlango wa fahamu yangu kupitia utamu wa munajati wao. Na hakika mimi kwanza nakuomba idhini ewe Mola Mlezi na pili namuomba idhini Mtume Wako (s.a.w.w.).

“Na tatu ninawaomba idhini Makhalifa Wako Maimam ambao nimefaradhishiwa kuwatii Hasan bin Ali, Ali bin Husain, Muhammad bin Ali na Ja’far bin Muhammad amani iwe juu yao, na malaika waliokabidhiwa makaburi haya. Je niingie ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu. Je niingie enyi Hoja wa Mwenyezi Mungu. Je niingie enyi Malaika wa Mwenyezi Mungu mlio wakuruba wenye kuishi katika eneo hili lililobarikiwa. Nipeni idhini ya kuingia enyi viongozi wangu, idhini bora kushinda ile mliyompa yeyote miongoni mwa vipenzi vyenu, kwani

nikiwa sistahiki hilo, ninyi ni wenye kustahiki kufanya hivyo.”

Ingia na sema:

بِسْمِ اللَّهِ وَبِاللَّهِ وَفِي سَبِيلِ اللَّهِ وَعَلَى مِلَّةِ رَسُولِ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ
عَلَيْهِ وَآلِهِ اللَّهُمَّ اغْفِرْ لِي وَارْحَمْنِي وَتُبْ عَلَيَّ إِنَّكَ أَنْتَ التَّوَّابُ
الرَّحِيمُ

“Kwa jina la Mwenyezi Mungu, na kwa Mwenyezi Mungu, na katika njia ya Mwenyezi Mungu, na kwa kufuata mila ya Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.), ewe Mwenyezi Mungu nighufirie, nihurumie na nikubalie toba, hakika Wewe ni Mwingi wa kukubali toba na Mwingi wa huruma.”

Aina ya pili ya kuomba idhini kwa ajili ya Ziyara:

يَا مَوَالِيَّ يَا أَبْنَاءَ رَسُولِ اللَّهِ، عَبْدُكُمْ وَابْنُ أُمَّتِكُمُ الدَّلِيلُ بَيْنَ
أَيْدِيكُمْ، وَالْبُضْعُ فِي عُلُقِ قَدْرِكُمْ، وَالْبُعْتَرُ بِحَقِّكُمْ، جَاءَكُمْ
مُسْتَجِيرًا بِكُمْ، قَاصِدًا إِلَى حَرَمِكُمْ، مُتَقَرِّبًا إِلَى مَقَامِكُمْ،
مُتَوَسِّلًا إِلَى اللَّهِ تَعَالَى بِكُمْ، أَدْخُلْ يَا مَوَالِيَّ، أَدْخُلْ يَا أَوْلِيَاءَ

اللَّهُ، أَدْخُلْ يَا مَلَائِكَةَ اللَّهِ الْإِحْسَانَ بِهَذَا الْحَمْرِ الْمُتَقِيينَ
بِهَذَا الشُّهْدِ

“Enyi wapendwa wangu! Enyi watoto wa Mtume wa Mwenyezi Mungu! Mtumwa wenu na mtoto wa mjakazi wenu, aliye dhalili mbele yenu, mwenye kutukuza heshima ya hadhi yenu na mwenye kutambua haki yenu, amekuja kwenu na hali ni mwenye kuomba ujirani wenu, ni mwenye kulikusudia eneo lenu tukufu, ni mwenye kujikurubisha kwenye makazi yenu na ni mwenye kutawasali kwa Mwenyezi Mungu kupitia kwenu. Je niingie enyi wapendwa wangu, je niingie enyi mawalii wa Mwenyezi Mungu, je niingie enyi malaika wa Mwenyezi Mungu wenye kulizunguka eneo hili tukufu na wenye kuishi katika jengo hili.”

Nyenyekwa kwa Mola Wako Mlezi na ulie, moyo wako utakapolainika na macho yako kutoka machozi, tambua hiyo ni alama ya kukubaliwa na kupewa idhini, kisha tanguliza mguu wako wa kulia na sema na hali ukiwa ni mnyenyekevu mwenye utulivu:

اللَّهُ أَكْبَرُ كَبِيرًا، وَالْحَمْدُ لِلَّهِ كَثِيرًا، وَسُبْحَانَ اللَّهِ بُكْرَةً وَأَصِيلًا،
وَالْحَمْدُ لِلَّهِ الْفَرْدِ الْوَحِيدِ الْبَاقِدِ الْأَحَدِ الْمُتَفَضِّلِ الْمَنَّانِ،

الْبُتْطُولِ الْحَنَّانِ الَّذِي مَنَّ بِطَوْلِهِ، وَسَهَّلَ زِيَارَةَ سَادَاتِي
بِإِحْسَانِهِ، وَلَمْ يَجْعَلْنِي عَنْ زِيَارَتِهِمْ مَبْنُوعًا بَلْ تَطَوَّلَ وَمَنَحَ

“Allah ni Mtukufu mno, Mwenyezi Mungu ana sifa njema nyingi mno, na utakatifu ni wa Mwenyezi Mungu asubuhi na jioni. Kila sifa njema ni ya Mwenyezi Mungu mmoja mkusudiwa wa haja, mtukuzwa wa pekee, mfadhili aliye mpaji, mwenye uwezo mwenye huruma, Ambaye ametoa kwa uwezo Wake, na amesahilisha kitendo cha kuwazuru mabwana zangu kwa ihsani Yake, na wala hajanifanya niwe mwenye kushindwa kuwazuru, bali amekuwa na uwezo na akatoa.”

Ziyara ya kwanza ya Maimamu wa huko Baqii:

Baadhi ya ulamaa wameitaja, na ameitaja pia Shaikh Saduq (q.s) katika kitabu *al-Fiqhi* kwa tofauti ndogo. Simama kwenye makaburi yao matukufu yaelekee na ukipe Kibla mgongo, sema:

عَلَيْكُمْ أَئْتَى الْهُدَى، السَّلَامُ عَلَيْكُمْ أَهْلَ التَّقْوَى، السَّلَامُ
عَلَيْكُمْ أَيُّهَا الْحُجَّجُ عَلَى أَهْلِ الدُّنْيَا، السَّلَامُ عَلَيْكُمْ أَيُّهَا الْقَوَّامُ
فِي الْبَرِّيَّةِ بِالنَّقِصِطِ، السَّلَامُ عَلَيْكُمْ أَهْلَ الصَّفْوَةِ، السَّلَامُ عَلَيْكُمْ
أَلِ رَسُولِ اللَّهِ، السَّلَامُ عَلَيْكُمْ أَهْلَ النَّجْوَى، أَشْهَدُ أَنَّكُمْ قَدْ

بَلَّغْتُمْ وَنَصَحْتُمْ وَصَبَرْتُمْ فِي ذَاتِ اللَّهِ، وَكُذِّبْتُمْ وَأَسَىءَ إِلَيْكُمْ
 فَغَفَرْتُمْ، وَأَشْهَدُ أَنَّكُمْ الْأَيْبَةُ الرَّاشِدُونَ الْمُهْتَدُونَ، وَأَنَّ
 طَاعَتَكُمْ مَفْرُوضَةٌ، وَأَنَّ قَوْلَكُمْ الصِّدْقُ، وَأَنَّكُمْ دَعَوْتُمْ فَلَمْ
 تُجَابُوا، وَأَمَرْتُمْ فَلَمْ تُطَاعُوا، وَأَنَّكُمْ دَعَائِمُ الدِّينِ وَأَرْكَانُ
 الْأَرْضِ، لَمْ تَزَالُوا بِعَيْنِ اللَّهِ يَنْسَخُكُمْ مِنْ أَصْلَابِ كُلِّ مُطَهَّرٍ،
 وَيُنْقَلِكُمْ مِنْ أَرْحَامِ الْمُطَهَّرَاتِ، لَمْ تُدَيِّسْكُمْ الْجَاهِلِيَّةُ
 الْجُهْلَاءُ، وَلَمْ تَشْرِكْ فِيكُمْ فِتْنُ الْأَهْوَاءِ،

طَبَّيْتُمْ وَطَابَ مَنَبَتِكُمْ، مَنْ بَكُمْ عَلَيْنَا دِيَانُ الدِّينِ، فَجَعَلَكُمْ فِي
 بُيُوتِ أَذْنِ اللَّهِ أَنْ تَرْفَعَ وَيُذَكَّرَ فِيهَا سُبُّهُ، وَجَعَلَ صَلَاتَنَا
 عَلَيْكُمْ رَحْمَةً لَنَا وَكَفَّارَةً لِدُنُوبِنَا، إِذِ اخْتَارَكُمْ اللَّهُ لَنَا، وَطَيَّبَ
 خَلْقَنَا بِهَا مَنْ عَلَيْنَا مِنْ وِلَايَتِكُمْ، وَكُنَّا عِنْدَهُ مُسَبِّينَ
 بِعَلْبِكُمْ، مُعْتَرِفِينَ بِتَضَدِّيقِنَا إِيَّاكُمْ، وَهَذَا مَقَامٌ مَنْ أَسْرَفَ
 وَأَخْطَأَ وَاسْتَكَانَ وَأَقْرَبَ بِهَا جَنَى وَرَجَا بِمَقَامِهِ الْخِلَاصَ، وَأَنَّ

يَسْتَقْدَهُ بِكُمْ مُسْتَقْدُ الْهَلْكَى مِنَ الرَّدى، فَكُونُوا لى شُفَعَاءَ،
 قَدَّ وَفَدَّتْ اِىْكُمْ اِذْ رَغَبَ عَنْكُمْ اَهْلُ الدُّنْيَا، وَاتَّخَذُوا آيَاتِ
 اللّٰهِ هُزُوًا وَاسْتَكْبَرُوا عَنْهَا

“Amani iwe juu yenu enyi Maimamu wa uongofu! Amani iwe juu yenu enyi wenye uchamungu! Amani iwe juu yenu enyi mlio Hoja juu ya wakazi wa duniani! Amani iwe juu yenu enyi wasimamizi wa viumbe kwa uadilifu! Amani iwe juu yenu enyi wenye uteule! Amani iwe juu yenu enyi aali wa Mtume wa Mwenyezi Mungu! Amani iwe juu yenu enyi mnaohusika na maongezi ya siri! Nashahidilia kwamba hakika nyinyi mmefikisha, mmenasihi na mmefanya subira kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, mmekadhibishwa na kutendewa ubaya lakini mkasamehe. Nashahidilia kwamba hakika nyinyi ni Maimamu wema waongofu, na kwamba kuwatii nyinyi ni faradhi, na kwamba hakika kauli yenu ni ukweli, na hakika nyinyi mmeita lakini hamjajibiwa, mmeamrisha lakini hamjatiwa, na kwamba hakika nyinyi ni mihimili ya dini na nguzo za ardhi, mmeendelea kuwa katika usimamizi wa Mwenyezi Mungu akiwatoeni toka kwenye mifupa ya mgongo wa kila aliyetakaswa na akiwahamisha toka kwenye vizazi vya waliotakaswa, ujahilia wa majahili haujawachafua na wala fitina za matamano hazijashiriki kwenu.

“Ninyi ni wasafi na ni safi asili yenu, ninyi ni neema tuliyo neemeshwa na hakimu wa Siku ya Malipo, hivyo amewaweka katika nyumba ambazo Mwenyezi Mungu ameamrisha zitukuzwe, na humo litajwe jina Lake, na amefanya sala zetu juu yenu ni rehema kwetu na ni kafara

ya madhambi yetu, pale Mwenyezi Mungu alipowachagua kwa ajili yetu na akayaweka uzuri maumbo yetu kwa neema aliyotuneemesha ya mapenzi yetu kwenu, na tulikuwa Kwake tukiitwa kwa elimu yenu na tukijulikana kwa usadiki wetu kwenu, na hiki ni kisimamo cha mtu aliyefanya uharibifu, akakosea, akanyenyekea na akaungama makosa aliyotenda na akataraji uokovu kupitia kisimamo chake, na amuombe yule mwenye kuwaokoa wale walioangamia amuokoe toka kwenye maangamio kupitia kwenu, hivyo kuweni waombezi wangu, kwani nimefunga safari hadi kwenu pale wakazi wa dunia walipojitenga nanyi, na wakazifanyia mchezo alama za Mwenyezi Mungu na kuzifanyia kiburi.”

Inua kichwa chako na useme:

يَا مَنْ هُوَ قَائِمٌ لَا يَسْهُو، وَدَائِمٌ لَا يَلْهُو، وَمُحِيطٌ بِكُلِّ شَيْءٍ لَكَ
الْبُنُّ بِهَا وَقَفَّتْ نِي وَعَرَفْتَنِي بِهَا أَقْبَتَنِي عَلَيْهِ، إِذْ صَدَّ عَنْهُ
عِبَادُكَ، وَجَهَلُوا مَعْرِفَتَهُ، وَاسْتَحْفُوا بِحَقِّهِ، وَمَالُوا إِلَى سِوَاهُ،
فَكَانَتِ الْبَيْتَةُ مِنْكَ عَلَى مَعَ أَقْوَامٍ خَصَّصْتَهُمْ بِهَا خَصَّصْتَنِي بِهِ،
فَلَاكَ الْحَبْدُ إِذْ كُنْتُ عِنْدَكَ فِي مَقَامِي هَذَا مَذْكُورًا مَكْتُوبًا، فَلَا
تَحْرِمْنِي مَا رَجَوْتُ، وَلَا تُخَيِّبْنِي فِيهَا دَعَوْتُ، بِحُرْمَةِ مُحَمَّدٍ
وَآلِهِ الطَّاهِرِينَ، وَصَلَّى اللَّهُ عَلَى مُحَمَّدٍ وَآلِ مُحَمَّدٍ.

“Ewe Ambaye ni mwenye kusimamia mambo asiyesahau, wa kudumu asiyeghafilika, na mwenye ujuzi wa kila kitu! Neema ni Yako kwa lile uliloniafikisha na kunijulisha lile ulilonisimamisha kwa ajili yake, pale waja Wako walipolizuia na wakashindwa kulijua, wakadharau haki yake na wakaelemea kwenye lisilokuwa hilo, hivyo hiyo ikawa ni neema Yako juu yangu pamoja na wale watu uliowapa lile ulilonipa. Hivyo una sifa njema ninapokuwa ni mwenye kutajwa na kuandikwa Kwako katika kisimamo changu hiki, basi usininyime nililotaraji na usinirudishe bila kunipa nililokuomba, kwa utukufu wa Muhammad na aali zake watoharifu, na (ninamuomba) Mwenyezi Mungu amsalie Muhammad na aali Muhammad.”

Kisha jiombee utakalo, kisha Sali Sala ya Ziyara rakaa nane, yaani Sali rakaa mbili kwa ajili ya zawadi kwa kila Imam (a.s.), ni sawa hiyo iwe nyumbani kwako au ndani ya Msikiti wa Mtume (s.a.w.w.), kwa sababu hivi sasa ni vigumu kusalia ndani ya Baqii.

Ziyara ya pili ya Maimamu wa huko Baqii:

Nayo ni Ziyara mjumuisho, inatumika kuwazuru Maasumina wote (a.s.), ameitaja Shaikh Saduq katika kitabu *al-Fiqhi*, amesema: Ridha (a.s.) aliulizwa kuhusu kuliendea kaburi la Abu Hasan Musa, akasema: Salini kwenye misikiti inayolizunguka, na inatosheleza kuisoma katika sehemu zote (yaani katika makaburi yote ya Maimamu au makaburi yote ya Manabii na Maimamu, kama ilivyo dhahiri).

Kama alivyosema Shaikh Saduq baada ya kuitaja ziyara yenyewe: Hii inatosheleza katika ziara zote (yaani katika makaburi yote ya Manabii na Maimamu).

Inatosha kusema:

السَّلَامُ عَلَى أَوْلِيَاءِ اللَّهِ وَأَصْفِيَائِهِ، السَّلَامُ عَلَى أَمْنَاءِ اللَّهِ
وَأَحِبَّائِهِ، السَّلَامُ عَلَى أَنْصَارِ اللَّهِ وَخُلَفَائِهِ، السَّلَامُ عَلَى مَحَالِّ
مَعْرِفَةِ اللَّهِ، السَّلَامُ عَلَى مَسَاكِينِ ذِكْرِ اللَّهِ، السَّلَامُ عَلَى
مُظْهِرِي أَمْرِ اللَّهِ وَنَهْيِهِ، السَّلَامُ عَلَى الدُّعَاةِ إِلَى اللَّهِ، السَّلَامُ
عَلَى الْمُسْتَقْرِّينَ فِي مَرْضَاتِ اللَّهِ، السَّلَامُ عَلَى الْمُخْلِصِينَ فِي
طَاعَةِ اللَّهِ، السَّلَامُ عَلَى الْأَدْلَاءِ عَلَى اللَّهِ، السَّلَامُ عَلَى الَّذِينَ
مَنْ وَالَاهُمْ فَقَدْ وَالَى اللَّهُ، وَمَنْ عَادَاهُمْ فَقَدْ عَادَى اللَّهُ، وَمَنْ
عَرَفَهُمْ فَقَدْ عَرَفَ اللَّهُ، وَمَنْ جَهَلَهُمْ فَقَدْ جَهَلَ اللَّهُ، وَمَنْ
اعْتَصَمَ بِهِمْ فَقَدْ اعْتَصَمَ بِاللَّهِ، وَمَنْ تَخَلَّى مِنْهُمْ فَقَدْ تَخَلَّى مِنَ
اللَّهِ عَزَّوَجَلَّ،

وَأَشْهَدُ اللَّهُ أَنِّي سَلِمٌ لِمَنْ سَالَمْتُمْ، وَحَرْبٌ لِمَنْ حَارَبْتُمْ، مُؤْمِنٌ
بِسِرِّكُمْ وَعَلَانِيَتِكُمْ، مُغَوِّضٌ فِي ذَلِكَ كُلِّهِ إِلَيْكُمْ، لَعَنَ اللَّهُ عَدُوَّ

آلِ مُحَمَّدٍ مِنَ الْجِنِّ وَالْإِنْسِ وَأَبْرَأُ إِلَى اللَّهِ مِنْهُمْ، وَصَلَّى اللَّهُ
عَلَى مُحَمَّدٍ وَآلِهِ

“Amani iwe juu ya Mawalii wa Mwenyezi Mungu na wateule Wake! Amani iwe juu ya waaminifu wa Mwenyezi Mungu na vipenzi Vyake! Amani iwe juu ya wasaidizi wa Mwenyezi Mungu na makhalifa Wake! Amani iwe juu ya sehemu yalipokaa maarifa ya Mwenyezi Mungu! Amani iwe juu ya makazi ya utajo wa Mwenyezi Mungu! Amani iwe juu ya wadhihirishaji wa amri ya Mwenyezi Mungu na katazo Lake! Amani iwe juu ya waitaji kwa Mwenyezi Mungu! Amani iwe juu ya wenye kutulia katika radhi za Mwenyezi Mungu! “Amani iwe juu ya wenye ikhlasi katika kumtii Mwenyezi Mungu! Amani iwe juu ya wenye kuonyesha ni nani Mwenyezi Mungu! Amani iwe juu ya wale ambao mwenye kuwapena wao bila shaka amempenda Mwenyezi Mungu, mwenye kuwafanyia uadui wao bila shaka amemfanyia uadui Mwenyezi Mungu, mwenye kuwatambua wao bila shaka amemtambua Mwenyezi Mungu, asiyewatambua wao bila shaka hajamtambua Mwenyezi Mungu, mwenye kushikamana nao bila shaka ameshikamana na Mwenyezi Mungu, na mwenye kujitenga nao bila shaka amejitenga na Mwenyezi Mungu!

“Namshuhudilisha Mwenyezi Mungu kwamba hakika mimi ni mwenye amani kwa yule mliye na amani naye na ni mwenye kumpiga vita yule mnayempiga vita, ni mwenye kuamini siri yenu na dhahiri yenu, katika hilo nimeyaacha yote mikononi mwenu. (Ninamuomba) Mwenyezi Mungu amlaani adui waMuhammad miongoni

mwa majini na watu, na ninakimbilia kwa Mwenyezi Mungu kwa kujitenga nao. Na (ninamuomba) Mwenyezi Mungu amsalie Muhammad na aali zake.”

Kithirisha kumsalia Muhammad na aali Muhammad na kuwataja kwa majina mmoja baada ya mwingine na kutoa tamko la kujitenga na maadui zao, na kisha omba utakalo kwa ajili yako mwenyewe na kwa ajili ya waumini wa kiume na wa kike.

Kuwasalia Maimamu Hasan na Husein (a.s.):

Katika kuwasalia Maimamu Hasan na Husein (a.s.) sema:

اللَّهُمَّ صَلِّ عَلَى الْحَسَنِ وَالْحُسَيْنِ عَبْدَيْكَ وَوَلِيِّكَ، وَابْنِي
رَسُولِكَ، وَسِبْطِي الرَّحْمَةَ، وَسَيِّدِي شَبَابِ أَهْلِ الْجَنَّةِ، أَفْضَلَ
مَا صَلَّيْتَ عَلَى أَحَدٍ مِنْ أَوْلَادِ النَّبِيِّينَ وَالْمُرْسَلِينَ، اللَّهُمَّ صَلِّ
عَلَى الْحَسَنِ ابْنِ سَيِّدِ النَّبِيِّينَ وَوَصِيِّ أَمِيرِ الْمُؤْمِنِينَ، أَلَسَّلَامُ
عَلَيْكَ يَا بَنَ رَسُولِ اللَّهِ، أَلَسَّلَامُ عَلَيْكَ يَا ابْنَ سَيِّدِ الْوَصِيِّينَ،
أَشْهَدُ أَنَّكَ يَا ابْنَ أَمِيرِ الْمُؤْمِنِينَ أَمِيرُ اللَّهِ وَابْنُ أَمِينِهِ، عِشْتَ
مَظْلُوماً وَمَضَيْتَ شَهِيداً، وَأَشْهَدُ أَنَّكَ الْإِمَامُ الرَّزِيُّ الْهَادِي

الْبَهْدِيِّ، اللَّهُمَّ صَلِّ عَلَيْهِ وَبَدِّخْ رُوحَهُ وَجَسَدَهُ عَنِّي فِي هَذِهِ
السَّاعَةِ أَفْضَلَ التَّحِيَّةِ وَالسَّلَامِ،

اللَّهُمَّ صَلِّ عَلَى الْحُسَيْنِ بْنِ عَلِيٍّ الْبَطْلُومِ الشَّهِيدِ، قَتِيلِ
الْكَفْرَةِ وَطَرِيحِ الْفَجْرَةِ، السَّلَامُ عَلَيْكَ يَا أَبَا عَبْدِ اللَّهِ، السَّلَامُ
عَلَيْكَ يَا بْنَ رَسُولِ اللَّهِ، السَّلَامُ عَلَيْكَ يَا ابْنَ أَمِيرِ الْمُؤْمِنِينَ
أَشْهَدُ مَوْقِنًا أَنَّكَ أَمِينُ اللَّهِ وَابْنُ أَمِينِهِ، قُتِلْتَ مَظْلُومًا
وَمَضَيْتَ شَهِيدًا، وَأَشْهَدُ أَنَّ اللَّهَ تَعَالَى الطَّالِبُ بِشَارِكِ، وَمُنْجِرُ
مَا وَعَدَكَ مِنَ النَّصْرِ وَالتَّأْيِيدِ فِي هَلَاكِ عَدُوِّكَ وَإِظْهَارِ دَعْوَتِكَ،
وَأَشْهَدُ أَنَّكَ وَفَيْتَ بِعَهْدِ اللَّهِ، وَجَاهَدْتَ فِي سَبِيلِ اللَّهِ،
وَعَبَدْتَ اللَّهَ مُخْلِصًا حَتَّى أَتَاكَ الْيَقِينُ لَعَنَ اللَّهُ أُمَّةً قَتَلَتْكَ،
وَلَعَنَ اللَّهُ أُمَّةً خَدَلَتْكَ، وَلَعَنَ اللَّهُ أُمَّةً الْبَتُّ عَلَيْكَ، وَأَبْرَأُ إِلَى
اللَّهِ تَعَالَى مِمَّنْ أَكْذَبَكَ وَاسْتَخَفَّ بِحَقِّكَ وَاسْتَحَلَّ دَمَكَ،

يَا أَبَا عَبْدِ اللَّهِ لَعَنَ اللَّهُ قَاتِلَكَ، وَلَعَنَ اللَّهُ
 خَادِلَكَ، وَلَعَنَ اللَّهُ مَنْ سَبَعَ وَأَعَيْتَكَ فَلَمْ يُجِبْكَ وَلَمْ يُضْمِرْكَ،
 وَلَعَنَ اللَّهُ مَنْ سَبَا نِسَاءَكَ أَنَا إِلَى اللَّهِ مِنْهُمْ بَرِيٌّ وَمَسْنُ وَالَاهُمْ
 وَمَالَاهُمْ وَأَعَانَهُمْ عَلَيْهِ، وَأَشْهَدُ أَنَّكَ وَالْأَيُّمَةُ مِنْ وُلْدِكَ كَلِمَةُ
 التَّقْوَى وَبَابُ الْهُدَى وَالْعُرْوَةُ الْوُثْقَى وَالْحَبَّةُ عَلَى أَهْلِ الدُّنْيَا،
 وَأَشْهَدُ أَنِّي بِكُمْ مُؤْمِنٌ وَبِئَنْزَلْتَكُمْ مَوْقِنٌ، وَلَكُمْ تَابِعٌ بِذَاتِ
 نَفْسِي وَشَرَايِعِ دِينِي وَخَوَاتِيمِ عَمَلِي وَمُنْقَلَبِي فِي دُنْيَايَ وَآخِرَتِي.

“Ewe Mwenyezi Mungu! Msalie Hasan na Husein waja Wako wawili, mawalii Wako wawili, watoto wa Mtume Wako, vijana wa rehema na mabwana wa vijana wa Peponi, sala iliyo bora kushinda ile uliyomsalia yeyote miongoni mwa watoto wa Manabii na Mitume. Ewe Mwenyezi Mungu! Msalie Hasan mtoto wa mbora wa Manabii na Wasii wa Amirul-Muuminina. Amani iwe juu yako ewe mtoto wa Mtume wa Mwenyezi Mungu! Amani iwe juu yako ewe mtoto wa mbora wa Mawasii! Nashahidilia kwamba hakika wewe mtoto wa Amirul-Muuminina ni mwaminifu wa Mwenyezi Mungu na mwana wa mwaminifu Wake, umeishi katika hali ya kudhulumiwa na umeondaka na hali ni shahidi. Na nashahidilia kwamba hakika wewe ni Imam mtakasifu, kiongozi uliye mwongozo. Ewe Mwenyezi Mungu! Msalie na ifikishie

roho yake na mwili wake katika saa hii maamkizi bora mno na salamu kutoka kwangu.

“Ewe Mwenyezi Mungu! Msalie Husein bin Ali mdhulumiwa aliyekufa kishahidi, muuwaji wa makafiri na muondowaji wa waovu. Amani iwe juu yako ewe Abu Abdillah! Amani iwe juu yako ewe mtoto wa Mtume wa Mwenyezi Mungu! Amani iwe juu yako ewe mtoto wa Amirul-Muuminina! Nashahidilia kwa yakini kabisa kwamba hakika wewe ni mwaminifu wa Mwenyezi Mungu na mwana wa mwaminifu Wake, umeuawa katika hali ya kudhulumiwa na umeondaka na hali ni shahidi. Na nashahidilia kwamba hakika Mwenyezi Mungu atakulipizia kisasi na atakutimizia alichokuahidi ambacho ni kukupa ushindi na kukuunga mkono katika kumhilikisha adui yako na kudhihirisha wito wako. Na nashahidilia kwamba hakika wewe ulitekeleza ahadi ya Mwenyezi Mungu, Ukapigana jihadi katika njia ya Mwenyezi Mungu, na ukamwabudu Mwenyezi Mungu kwa ikhlasi mpaka kifo kilipokufika. Mwenyezi Mungu aulaani Ummah uliokuuwa, Mwenyezi Mungu aulaani Ummah uliokutelekeza, na Mwenyezi Mungu aulaani Ummah ulioitikia wito dhidi yako, nakimbilia kwa Mwenyezi Mungu dhidi ya yule aliyekukadhibisha, akadharau haki yako na akahalalisha damu yako.

“Kwa haki ya baba yangu, haki yako na haki ya mama yangu, ewe Abu Abdillah! Mwenyezi Mungu amlaani aliyekuuwa, Mwenyezi Mungu amlaani aliyekutelekeza, Mwenyezi Mungu amlaani aliyesikia wito wako lakini hakukuitikia na hakukusaidia, na Mwenyezi Mungu amlaani aliyewafanya mateka wanawake wako, mimi ni mwenye kukimbilia kwa Mwenyezi Mungu dhidi yao, dhidi ya vipenzi vyao, dhidi ya kundi lao na dhidi ya wale

waliowasaidia. Na nashahidilia kwamba hakika wewe na Maimamu toka katika kizazi chako ni neno la uchamungu, mlango wa uongofu, shikio madhubuti na ni hoja juu ya wakazi wa ardhini. Na nashahidilia kwamba hakika mimi ni mwenye kuwaamini nyinyi na ni mwenye yakini na cheo chenu, na ni mwenye kuwafuata nyinyi kwa mambo ya nafsi yangu, sheria ya dini yangu, hatma ya amali yangu na mgeuko wangu katika dunia yangu na akhera yangu.”

Kumsalia Imamu Zainul-Abidina (a.s.):

Katika kumsalia Imamu Zainul-Abidina (a.s.) sema:

اللَّهُمَّ صَلِّ عَلَى عَلِيِّ بْنِ الْحُسَيْنِ سَيِّدِ الْعَابِدِينَ الَّذِي
 اسْتَخْلَصْتَهُ لِنَفْسِكَ، وَجَعَلْتَ مِنْهُ أُمَّةً الْهُدَى الَّذِينَ يَهْدُونَ
 بِالْحَقِّ وَبِهِ يَعْدِلُونَ، اخْتَرْتَهُ لِنَفْسِكَ وَطَهَّرْتَهُ مِنَ الرَّجْسِ،
 وَأَصْطَفَيْتَهُ وَجَعَلْتَهُ هَادِيًا مَهْدِيًّا، اللَّهُمَّ فَصَلِّ عَلَيْهِ أَفْضَلَ مَا
 صَلَّيْتَ عَلَى أَحَدٍ مِنْ ذُرِّيَّةِ أَنْبِيَائِكَ حَتَّى تَبْدُغَ بِهِ مَا تَقَرُّ بِهِ
 عَيْنُهُ فِي الدُّنْيَا وَالْآخِرَةِ، إِنَّكَ عَزِيزٌ حَكِيمٌ

“Ewe Mwenyezi Mungu! Msalie Ali bin Husein bwana wa wafanya ibada ambaye umemteua kwa ajili Yako mwenyewe, na ukatoa toka kwake Maimamu wa uongofu ambao huongoza kwa haki na kwayo hufanya uadilifu, umemchagua kwa ajili Yako mwenyewe na umemtakasa na uchafu, na umemteua na kumfanya kiongozi aliye

mwongozo. Ewe Mwenyezi Mungu! Basi msalie yeye sala bora kushinda uliyomsalia yeyote toka katika kizazi cha Manabii Wako, mpaka kwa sala hiyo umfikishie kile kitakachotuliza macho yake duniani na akhera, hakika Wewe ni Mwenye nguvu Mwenye hikima.”

Kumsalia Imamu Muhammad al-Baqir (a.s.):

Katika kumsalia Imamu Muhammad al-Baqir (a.s.) sema:

اللَّهُمَّ صَلِّ عَلَى مُحَمَّدِ بْنِ عَلِيٍّ، بَاقِرِ الْعِلْمِ وَإِمَامِ الْهُدَى،
وَقَائِدِ أَهْلِ التَّقْوَى وَالْمُنْتَجِبِ مِنْ عِبَادِكَ، اللَّهُمَّ وَكَمَا
جَعَلْتَهُ عَلِيًّا لِعِبَادِكَ وَمَنَارًا لِبِلَادِكَ، وَمُسْتَوْدَعًا لِحِكْمَتِكَ
وَمُتَرَجِّبًا لِرُوحِيكَ، وَأَمَرْتَ بِطَاعَتِهِ وَحَدَّرْتَ مِنْ مَعْصِيَتِهِ،
فَصَلِّ عَلَيْهِ يَا رَبِّ أَفْضَلَ مَا صَلَّيْتَ عَلَى أَحَدٍ مِنْ ذُرِّيَّةِ أَنْبِيَائِكَ
وَأَصْفِيَاءِكَ وَرُسُلِكَ وَأَمَنَائِكَ يَا رَبَّ الْعَالَمِينَ

“Ewe Mwenyezi Mungu! Msalie Muhammad bin Ali, mpasuaji wa elimu na Imam wa uongofu, kiongozi wa wachamungu na mteule kati ya waja Wako. Ewe Mwenyezi Mungu! Kama ulivyomfanya alama ya waja Wako, mnara wa nchi Yako, hifadhi ya hikima Yako na mfafanuzi wa Wahyi Wako, na ukaamuru kumtii na ukahadharisha kumuasi, vilevile msalie ewe Mola Mlezi sala bora mno kushinda uliyomsalia yeyote toka katika

kizazi cha Manabii Wako, wateule Wako, Mitume Wako na waaminifu Wako, ewe Mola Mlezi wa viumbe wote.”

Kumsalia Imamu Ja’far as-Sadiq (a.s.):

Katika kumsalia Imamu Ja’far as-Sadiq (a.s.) sema:

اللَّهُمَّ صَلِّ عَلَى جَعْفَرِ بْنِ مُحَمَّدٍ الصَّادِقِ، خَازِنِ الْعِلْمِ،
الدَّاعِي إِلَيْكَ بِالْحَقِّ، الثَّوْرِ الْبُيَيْنِ، اللَّهُمَّ وَكَمَا جَعَلْتَهُ
مَعْدِنَ كَلَامِكَ وَوَحْيِكَ وَخَازِنَ عِلْمِكَ وَلِسَانَ تَوْحِيدِكَ، وَوَلِيَّ
أَمْرِكَ وَمُسْتَحْفَظَ دِينِكَ، فَصَلِّ عَلَيْهِ أَفْضَلَ مَا صَلَّيْتَ عَلَى أَحَدٍ
مِنْ أَصْفِيَاءِكَ وَحُجَجِكَ إِنَّكَ حَبِيدٌ مَجِيدٌ

“Ewe Mwenyezi Mungu! Msalie Ja’far bin Muhammad as-Sadiq, muhazini wa elimu, muitaji Kwako kwa haki na aliye nuru ya wazi. Ewe Mwenyezi Mungu! Kama ulivyomfanya kituo cha maneno Yako na wahyi Wako, mhazini wa elimu Yako na ulimi wa Tauhidi Yako, msimamizi wa jambo Lako na muhifadhi wa dini Yako, vilevile msalie sala bora kushinda ile uliyomsalia yeyote miongoni mwa wateule Wako na hoja Wako, hakika Wewe ni mhimidiwa msifika.”

**Namna ya kumzuru Sayyida Fatima binti Asadi,
mama mzazi wa Amirul-Muuminina Ali (a.s.):**

Simama kwenye kaburi lake lililopo pembezoni mwa makaburi ya Maimamu huko Baqii. Na baadhi wamesema kwamba kaburi lake lipo pembezoni mwa kaburi la Halima Sa'diyya, yaani nje ya Baqii. Sema:

اَلسَّلَامُ عَلٰى نَبِيِّ اللهِ،. اَلسَّلَامُ عَلٰى رَسُوْلِ اللهِ، اَلسَّلَامُ عَلٰى
مُحَمَّدٍ سَيِّدِ الْمُرْسَلِيْنَ، اَلسَّلَامُ عَلٰى مُحَمَّدٍ سَيِّدِ الْاَوْلِيَيْنِ،
اَلسَّلَامُ عَلٰى مُحَمَّدٍ سَيِّدِ الْاٰخِرِيْنَ، اَلسَّلَامُ عَلٰى مَنْ بَعَثَهُ اللهُ
رَحْمَةً لِّلْعَالَمِيْنَ، اَلسَّلَامُ عَلَيْكَ أَيُّهَا النَّبِيُّ وَرَحْمَةُ اللهِ وَبَرَكَاتُهُ،
اَلسَّلَامُ عَلٰى فَاطِمَةَ بِنْتِ اَسَدِ الْهَاشِمِيَّةِ، اَلسَّلَامُ عَلَيْكَ أَيَّتُهَا
الصِّدِّيقَةُ الْمَرْضِيَّةُ، اَلسَّلَامُ عَلَيْكَ أَيَّتُهَا التَّقِيَّةُ النَّقِيَّةُ،
اَلسَّلَامُ عَلَيْكَ أَيَّتُهَا الْكَرِيْمَةُ الرَّضِيَّةُ، اَلسَّلَامُ عَلَيْكَ يَا كَافِلَةَ
مُحَمَّدٍ خَاتِمِ النَّبِيِّيْنَ، اَلسَّلَامُ عَلَيْكَ يَا وَالِدَةَ سَيِّدِ الْوَصِيِّيْنَ،
اَلسَّلَامُ عَلَيْكَ يَا مَنْ ظَهَرَتْ شَفَقَتُهَا عَلٰى رَسُوْلِ اللهِ خَاتِمِ
النَّبِيِّيْنَ، اَلسَّلَامُ عَلَيْكَ يَا مَنْ تَرَبَّيْتُهَا لِوَلِيِّ اللهِ الْاَمِيْنِ،

السَّلَامُ عَلَيْكَ وَعَلَى رُوحِكَ وَبَدَنِكَ الطَّاهِرِ، السَّلَامُ عَلَيْكَ
وَعَلَى وَلَدِكَ وَرَحْبَةِ اللَّهِ وَبَرَكَاتِهِ،

أَشْهَدُ أَنَّكَ أَحْسَنْتِ الْكِفَالََةَ، وَأَدَيْتِ الْأَمَانَةَ، وَاجْتَهَدْتِ فِي
مَرْضَاتِ اللَّهِ، وَبَالِغْتِ فِي حِفْظِ رَسُولِ اللَّهِ، عَارِفَةً بِحَقِّهِ،
مُؤْمِنَةً بِصِدْقِهِ، مُعْتَرِفَةً بِنُبُوَّتِهِ، مُسْتَبْصِرَةً بِنِعْمَتِهِ، كَافِلَةً
بِتَرْبِيَّتِهِ، مُشْفِقَةً عَلَى نَفْسِهِ، وَاقِفَةً عَلَى خِدْمَتِهِ، مُخْتَارَةً
رِضَاهُ، وَأَشْهَدُ أَنَّكَ مَضَيْتِ عَلَى الْإِيَابِ وَالْتِمَسِكِ بِأَشْرَفِ
الْأُدْيَانِ، رَاضِيَةً مَرْضِيَّةً طَاهِرَةً زَكِيَّةً تَقِيَّةً نَقِيَّةً، فَرَضَى اللَّهُ
عَنْكَ وَأَرْضَاكَ، وَجَعَلَ الْجَنَّةَ مَنْزِلَكَ وَمَاوَاكِ اللَّهُمَّ صَلِّ عَلَى
مُحَمَّدٍ وَآلِ مُحَمَّدٍ وَانْفَعْنِي بِزِيَارَتِهَا، وَثَبِّتْنِي عَلَى مَحَبَّتِهَا،
وَلَا تَحْرِمْنِي شَفَاعَتَهَا، وَشَفَاعَةَ الْأَيْبَةِ مِنْ ذُرِّيَّتِهَا، وَارْتُقِنِي
مُرَافَقَتَهَا، وَاحْشُرْنِي مَعَهَا وَمَعَ أَوْلَادِهَا الطَّاهِرِينَ،

اللَّهُمَّ لَا تَجْعَلْهُ آخِرَ الْعَهْدِ مِنْ زِيَارَتِي إِيَّاهَا، وَارْمُرْنِي الْعُودَ
 إِلَيْهَا أَبَدًا مَا أَبْقَيْتَنِي، وَإِذَا تَوَفَّيْتَنِي فَاحْشُرْنِي فِي زُمْرَتِهَا،
 وَأَدْخِلْنِي فِي شَفَاعَتِهَا، بِرَحْمَتِكَ يَا أَرْحَمَ الرَّاحِمِينَ، اللَّهُمَّ
 بِحَقِّهَا عِنْدَكَ وَمَنْزِلَتِهَا لَدَيْكَ، اغْفِرْ لِي وَلِوَالِدَيَّ وَلِجَمِيعِ
 الْمُؤْمِنِينَ وَالْمُؤْمِنَاتِ، وَآتِنَا فِي الدُّنْيَا حَسَنَةً وَفِي الْآخِرَةِ
 حَسَنَةً وَقِنَا بِرَحْمَتِكَ عَذَابَ النَّارِ

“Amani iwe juu ya Nabii wa Mwenyezi Mungu! Amani iwe juu ya Mtume wa Mwenyezi Mungu! Amani iwe juu ya Muhammad mbora wa Mitume! Amani iwe juu ya Muhammad mbora wa wale wa mwanzo! Amani iwe juu ya Muhammad mbora wa wale wa mwisho! Amani iwe juu ya yule aliyetumwa na Mwenyezi Mungu awe rehema kwa walimwengu! Amani iwe juu yako ewe Nabii na pia rehema za Mwenyezi Mungu na Baraka Zake! Amani iwe juu yako Fatima binti Asadi mhashimiya! Amani iwe juu yako ewe mkweli mwenye kuridhiwa! Amani iwe juu yako ewe mchamungu msafi! Amani iwe juu yako ewe mkarimu mwenye kuridhia! Amani iwe juu yako ewe mlezi wa Muhammad mwisho wa Manabii! Amani iwe juu yako ewe mama mzazi wa bwana wa Mawasii! Amani iwe juu yako ewe ambaye ilidhihiri huruma yake kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu mwisho wa Manabii! Amani iwe juu yako ewe ambaye yalidhihiri malezi yake kwa Walii wa Mwenyezi Mungu aliye mwaminifu! Amani iwe juu yako

na juu ya roho yako na mwili wako ulio tohara! Amani iwe juu yako na juu ya mzazi wako pia rehome za Mwenyezi Mungu na Baraka Zake.

“Nashahidilia kwamba hakika wewe ulitoa malezi bora, ukatekeleza amana, ukajitolea kwa juhudi katika lile limridhishalo Mwenyezi Mungu na ukapindukia katika kumhifadhi Mtume wa Mwenyezi Mungu, na hali ni mwenye kutambua haki yake, mwenye kuamini ukweli wake, mwenye kukiri unabii wake, mwenye kuona neema yake, mwenye kusimamia malezi yake, mwenye kumhurumia, mwenye kumhudumia, mwenye kuchagua radhi yake (mwenye kumfadhilisha kuliko yeye mwenyewe). Na nashahidilia kwamba hakika wewe umepita juu ya imani na umeshikamana na dini tukufu mno, ilhali ni mwenye kuridhia mwenye kuridhiwa, uliyetoharika mtakasifu, mchamungu na msafi, Mwenyezi Mungu akawa radhi nawe na akakuridhisha, na akafanya Pepo ndio mashukio yako na mafikio yako. Ewe Mwenyezi Mungu! Msalie Muhammad na aali Muhammad na ninufaishe kwa kumzuru kwangu (Fatima) na nithibitisha katika mapenzi yake, na wala usininyime uombezi wake na uombezi wa Maimamu toka katika kizazi chake, na niruzuku urafiki wake na nikusanye pamoja naye na pamoja na wanae watakasifu.

“Ewe Mwenyezi Mungu! Usifanye hii kuwa ahadi yangu ya mwisho ya kumzuru yeye, niruzuku hali ya kurudi tena kwake muda wote utakaoniweka hai, na utakaponifisha unikusanye katika kundi lake, na uniingize katika uombezi wake kwa rehema Zako ewe Mwenye kurehemu kushinda wote wenye kurehemu. Ewe Mwenyezi Mungu! Kupitia haki yake iliyopo Kwako na cheo chake Kwako nighufirie mimi na wazazi wangu na waumini wote wa kiume na wa

kike, na utupe katika dunia mema na katika akhera mema na utukinge na adhabu ya moto kwa rehema Zako.” (Kisha Sali Sala ya Ziyara eneo linalofaa kwa nia ya kujibiwa.)

Namna ya kumzuru Ibrahim mtoto wa Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.):

Simama kwenye kaburi lake na useme:

اَلسَّلَامُ عَلٰى رَسُوْلِ اللهِ، اَلسَّلَامُ عَلٰى نَبِيِّ اللهِ، اَلسَّلَامُ عَلٰى
حَبِيبِ اللهِ، اَلسَّلَامُ عَلٰى صَفِيِّ اللهِ، اَلسَّلَامُ عَلٰى نَجِيِّ اللهِ،
اَلسَّلَامُ عَلٰى مُحَمَّدِ بْنِ عَبْدِاللهِ، سَيِّدِ الْاَنْبِيَاءِ وَخَاتَمِ
الرُّسُلَيْنِ، وَخَيْرَةِ اللهِ مِنْ خَلْقِهِ فِي اَرْضِهِ وَسَبَائِهِ، اَلسَّلَامُ عَلٰى
جَمِيعِ اَنْبِيَاءِ اللهِ وَرُسُلِهِ، اَلسَّلَامُ عَلٰى السُّعْدَاءِ وَ الشُّهَدَاءِ
وَ الصَّالِحِينَ، اَلسَّلَامُ عَلَيْنَا وَعَلَى عِبَادِ اللهِ الصَّالِحِينَ، اَلسَّلَامُ
عَلَيْكَ اَيَّتُهَا الرُّوْحُ الزَّكِيَّةُ، اَلسَّلَامُ عَلَيْكَ اَيَّتُهَا النَّفْسُ
الشَّرِيفَةُ، اَلسَّلَامُ عَلَيْكَ اَيَّتُهَا السُّلَالَةُ الطَّاهِرَةُ، اَلسَّلَامُ
عَلَيْكَ اَيَّتُهَا النَّسَبَةُ الزَّكِيَّةُ،

السَّلَامُ عَلَيْكَ يَا ابْنَ خَيْرِ الْوَرَى، السَّلَامُ عَلَيْكَ يَا ابْنَ النَّبِيِّ
الْمُحْتَبَى، السَّلَامُ عَلَيْكَ يَا ابْنَ الْمَبْعُوثِ إِلَى كَافَّةِ الْوَرَى،
السَّلَامُ عَلَيْكَ يَا ابْنَ الْبَشِيرِ النَّذِيرِ، السَّلَامُ عَلَيْكَ يَا ابْنَ
السَّمَاكِ الْهَنِيرِ، السَّلَامُ عَلَيْكَ يَا ابْنَ الْمُؤَيَّدِ بِالْقُرْآنِ، السَّلَامُ
عَلَيْكَ يَا ابْنَ الْمُرْسَلِ إِلَى الْإِنْسِ وَالْجَانِّ، السَّلَامُ عَلَيْكَ يَا ابْنَ
صَاحِبِ الرَّايَةِ وَالْعَلَامَةِ، السَّلَامُ عَلَيْكَ يَا ابْنَ الشَّفِيعِ يَوْمَ
الْقِيَامَةِ، السَّلَامُ عَلَيْكَ يَا ابْنَ مَنْ حَبَاهُ اللَّهُ بِالْكَرَامَةِ،
السَّلَامُ عَلَيْكَ وَرَحْمَةُ اللَّهِ وَبَرَكَاتُهُ،

أَشْهَدُ أَنَّكَ قَدْ اخْتَارَ اللَّهُ لَكَ دَارَ إِنْعَامِهِ قَبْلَ أَنْ يَكْتُبَ
عَلَيْكَ أَحْكَامَهُ، أَوْ يُكَلِّفَكَ حَلَالَهُ وَحَرَامَهُ، فَتَقْدَكَ إِلَيْهِ طَيْباً
زَاكِياً مَرْضِياً طَاهِراً مِنْ كُلِّ نَجَسٍ، مُقَدَّساً مِنْ كُلِّ دَنَسٍ،
وَبَوَّأَكَ جَنَّةَ الْمَأْوَى، وَرَفَعَكَ إِلَى الدَّرَجَاتِ الْعُلَى، وَصَلَّى اللَّهُ
عَلَيْكَ صَلَاةً تَقْرَأُ بِهَا عَيْنُ رَسُولِهِ، وَتُبَلِّغُهُ أَكْبَرَ مَأْمُورِهِ.

اللَّهُمَّ اجْعَلْ أَفْضَلَ صَلَوَاتِكَ وَأَزْكَاهَا، وَأَنْسَى بَرَكَاتِكَ وَأَوْفَاهَا،
عَلَى رَسُولِكَ وَنَبِيِّكَ وَخَيْرَتِكَ مِنْ خَلْقِكَ، مُحَمَّدَ خَاتَمِ
النَّبِيِّينَ، وَعَلَى مَنْ نَسَلَ مِنْ أَوْلَادِهِ الطَّيِّبِينَ، وَعَلَى مَا
خَلَّفَ مِنْ عَثَرَتِهِ الطَّاهِرِينَ، بِرَحْمَتِكَ يَا أَرْحَمَ الرَّاحِمِينَ. اللَّهُمَّ
إِنِّي أَسْأَلُكَ بِحَقِّ مُحَمَّدٍ صَفِيِّكَ، وَإِبْرَاهِيمَ نَجْلِ نَبِيِّكَ أَنْ
تَجْعَلَ سَعْيِي بِهِمْ مَشْكُوراً، وَذَنْبِي بِهِمْ مَغْفُوراً، وَحَيَاتِي بِهِمْ
سَعِيدَةً، وَعَاقِبَتِي بِهِمْ حَسِيدَةً، وَحَوَائِجِي بِهِمْ مَقْضِيَّةً، وَأَفْعَالِي
بِهِمْ مَرْضِيَّةً، وَأُمُورِي بِهِمْ مَسْعُودَةً، وَشُؤُونِي بِهِمْ مَحْشُودَةً.

اللَّهُمَّ وَأَحْسِنْ لِي التَّوْفِيقَ، وَنَفِّسْ عَنِّي كُلَّ هَمٍّ وَضِيقٍ. اللَّهُمَّ
جَنِّبْنِي عِقَابَكَ، وَامْنَحْنِي ثَوَابَكَ، وَأَسْكِنْنِي جَنَّاتَكَ، وَادْمُرْ قِنِي
رِضْوَانَكَ وَأَمَانَكَ، وَأَشْرِكْ لِي فِي صَالِحِ دُعَائِي وَالِدَيْي وَوُلْدِي
وَجَبِيحِ الْهُؤُمِنِينَ وَالْمُؤْمِنَاتِ، الْأَحْيَاءِ مِنْهُمْ وَالْأَمْوَاتِ، إِنَّكَ
وَلِيُّ الْبَاقِيَاتِ الصَّالِحَاتِ، آمِينَ رَبَّ الْعَالَمِينَ

“Amani iwe juu ya Mtume wa Mwenyezi Mungu! Amani iwe juu ya Nabii wa Mwenyezi Mungu! Amani iwe juu ya hababi wa Mwenyezi Mungu! Amani iwe juu ya mteule wa Mwenyezi Mungu! Amani iwe juu ya msema siri na Mwenyezi Mungu! Amani iwe juu ya Muhammad bin Abdullah mbora wa Manabii, mwisho wa Mitume na chaguo la Mwenyezi Mungu toka katika viumbe Vyake ardhini na mbinguni! Amani iwe juu ya Manabii Wake wote na Mitume Wake! Amani iwe juu ya Mashahidi wote, wema na waswalihina! Amani iwe juu yetu na juu ya waja wema wa Mwenyezi Mungu! Amani iwe juu yako ewe roho takasifu! Amani iwe juu yako ewe nafsi tukufu! Amani iwe juu yako ewe asili takasifu! Amani iwe juu yako ewe nafsi takasifu!

“Amani iwe juu yako ewe mtoto wa mbora wa viumbe! Amani iwe juu yako ewe mtoto wa Nabii mteule! Amani iwe juu yako ewe mtoto wa aliyetumwa kwa viumbe wote! Amani iwe juu yako ewe mtoto wa mtoa habari njema na mwonyaji! Amani iwe juu yako ewe mtoto wa taa itoayo nuru! Amani iwe juu yako ewe mtoto wa aliyepewa nguvu kwa Qur’an! Amani iwe juu yako ewe mtoto wa aliyetumwa kwa wanadamu na majini! Amani iwe juu yako ewe mtoto wa mwenye bendera na alama! Amani iwe juu yako ewe mtoto wa mwombezi wa Siku ya Kiyama! Amani iwe juu yako ewe mtoto wa aliyetunukiwa heshima na Mwenyezi Mungu! Amani iwe juu yako na pia rehema za Mwenyezi Mungu na Baraka Zake!

“Nashahidilia kwamba hakika Mwenyezi Mungu amekuchagulia nyumba ya kukunemeshea kabla hajafaradhisha juu yako hukumu Zake au kukuwajibisha kwa halili Yake na haramu Yake, hivyo akakuhamishia Kwake na hali wewe ni mwema, mtakasifu, mwenye

kuridhiwa, msafi dhidi ya kila najisi na mtakaswa dhidi ya kila uchafu. Akakupa makazi katika pepo uliyofikia na akakunyanyua mpaka kwenye daraja za juu. Mwenyezi Mungu akusalie sala itakayotuliza macho ya Mtume Wake na kumfikishia lile kubwa mno analolitumaini.

“Ewe Mwenyezi Mungu! Jaalia Sala Yako iliyo bora kushinda zote, tukufu kushinda zote, na baraka Yako yenye kuongezeka kushinda zote na yenye kutimia kushinda zote, ziwe juu ya Mtume Wako, Nabii Wako na chaguo Lako toka katika viumbe Vyako Muhammad mwisho wa Manabii, na ziwe juu ya kizazi toka katika watoto wake wema, na ziwe juu ya aliyowaacha toka katika kizazi chake kitakasifu, kwa rehema Zako ewe Mwenye kurehemu kushinda wote wenye kurehemu. Ewe Mwenyezi Mungu! Hakika mimi nakuomba kwa haki ya Muhammad mteule Wako na Ibrahim mtoto wa Nabii Wako, ufanye mwendo wangu uwe wenye kuthaminiwa kupitia kwao, dhambi zangu ziwe zenye kughufiriwa kupitia kwao, uhai wangu uwe wenye mafanikio kupitia kwao, hatima yangu iwe njema kupitia kwao, haja zangu ziwe zenye kukidhiwa kupitia kwao, vitendo vyangu viwe vyenye kuridhiwa kupitia kwao, mambo yangu yawe yenye mafanikio kupitia kwao na mambo yangu yawe yenye kusifika kupitia kwao.

“Ewe Mwenyezi Mungu! Niwafikishe vizuri na niondolee kila tabu na dhiki. Ewe Mwenyezi Mungu! Niepushe na adhabu Yako na nitunukie thawabu Zako, nipe makazi ndani ya pepo Yako na niruzuku ridhaa Yako na amani Yako, na kwa ajili yangu mshirikishe katika dua yangu njema mzazi wangu, kizazi changu na waumini wote wa kike na wa kiume walio hai miongoni mwao na walio wafu, hakika Wewe ndiye msimamizi wa yale yenye

kudumu yaliyo mema. Amina ewe Mola Mlezi wa walimwengu.”

(Omba haja yako na Sali sehemu ifaayo Sala ya Ziyara.)

Namna ya kuwazuru mabinti wa Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.):

Simama kwenye makaburi yao na sema katika kuwazuru:

اَلسَّلَامُ عَلَیْكَ يَا رَسُوْلَ رَبِّ الْعَالَمِیْنَ، اَلسَّلَامُ عَلَیْكَ يَا صَفْوَةَ
جَمِیْعِ الْاَنْبِیَاءِ وَالْمُرْسَلِیْنَ، اَلسَّلَامُ عَلَیْكَ يَا مَنْ اَخْتَارَهُ اللهُ
عَلَى الْخَلْقِ اَجْمَعِیْنَ، وَرَحْمَةَ اللهِ وَبَرَكَاتَهُ، اَلسَّلَامُ عَلَیْ بَنَاتِ
السَّیِّدِ الْمُصْطَفِیِّ، اَلسَّلَامُ عَلَیْ بَنَاتِ النَّبِیِّ الْمُحْتَبِیِّ، اَلسَّلَامُ
عَلَى بَنَاتِ مَنْ اصْطَفِیَهُ اللهُ فِی السَّمَاءِ، وَفَضَّلَهُ عَلَیْ جَمِیْعِ
الْبَرِیَّةِ وَالْوَرَى، اَلسَّلَامُ عَلَیْ ذُرِّیَّةِ السَّیِّدِ الْجَلِیْلِ، مِنْ نَسْلِ
اِسْمَاعِیْلِ، وَسُلَالَةِ اِبْرَاهِیْمَ الْخَلِیْلِ،

اَلسَّلَامُ عَلَیْ بَنَاتِ النَّبِیِّ الرَّسُوْلِ، اَلسَّلَامُ عَلَیْ اَخْوَاتِ فَاطِمَةَ
الرُّهْرَاءِ الْبَتُوْلِ، اَلسَّلَامُ عَلَیْ الذَّرِیَّةِ الطَّیِّبَةِ الطَّاهِرَةِ وَالْعَتْرَةِ

الزاكية الزاهرة بنات خاتم النبيين وسيد الأنبياء والبرسدين
 وخيرة رسول الله أجمعين. أَسَلَامُ عَلَى الذَّرِيَّةِ الطَّاهِرَةِ
 الزاكية والعترة البصطفوية أَسَلَامُ عَلَى زَيْنَبَ وَأُمِّ كَلْثُومَ
 وَرُقَيْيَةَ، أَسَلَامُ عَلَى الشَّرِيفَاتِ الْأَحْسَابِ، وَالطَّاهِرَاتِ
 الْأَنْسَابِ، أَسَلَامُ عَلَى بَنَاتِ الْأَبَاءِ الْأَعَاظِمِ، وَسُلَالَةِ الْأَجْدَادِ
 الْأَكَارِمِ الْأَفَاخِمِ، عَبْدِ الْمُطَلِّبِ وَعَبْدِ مَنْفٍ وَهَاشِمِ، وَرَحْمَةُ
 اللَّهِ وَبَرَكَاتُهُ

“Amani iwe juu yako ewe Mtume wa Mola Mlezi wa
 walimwengu! Amani iwe juu yako ewe chaguo bora kati ya
 Manabii wote na Mitume wote! Amani iwe juu yako ewe
 ambaye Mwenyezi Mungu alimchagua juu ya viumbe
 wote, na pia rehemu Zake na Baraka Zake viwe juu yako!
 Amani iwe juu ya mabinti wa bwana mteule! Amani iwe
 juu ya mabinti wa Nabii mteule! Amani iwe juu ya mabinti
 wa ambaye Mwenyezi Mungu alimteua mbinguni na
 akamfadhilisha kushinda viumbe wote! Amani iwe juu ya
 kizazi cha bwana mtukufu toka katika kizazi cha Ismail na
 asili ya Ibrahim khalili!

“Amani iwe juu ya mabinti wa Nabii aliye Mtume! Amani
 iwe juu ya ndugu wa kike wa Fatima Zahrau al-Batul!
 Amani iwe juu ya kizazi chema na safi na kizazi kitakasifu
 chenye kutoa nuru, mabinti wa mwisho wa Manabii na

mbora wa Manabii na Mitume na chaguo bora kati ya Mitume wote wa Mwenyezi Mungu! Amani iwe juu ya kizazi safi kitakasifu na kizazi cha mteule! Amani iwe juu ya Zainab, Ummu Kulthum na Ruqayyah! Amani iwe juu ya wenye nasaba tukufu na nasaba takasifu! Amani iwe juu ya mabinti wa mababa watukufu na asili ya mababu watukufu waheshimiwa Abdul-Muttalib, Abdu Manaf na Hashim, na pia rehema za Mwenyezi Mungu na Baraka Zake viwe juu yao.”

**Namna ya kuwazuru shangazi wawili wa Mtume:
Swafiyyah na Atiqah:**

السَّلَامُ عَلَيْكَ يَا عَمَّتِي رَسُولِ اللَّهِ، السَّلَامُ عَلَيْكَ يَا عَمَّتِي نَبِيِّ
اللَّهِ، السَّلَامُ عَلَيْكَ يَا عَمَّتِي حَبِيبِ اللَّهِ، السَّلَامُ عَلَيْكَ يَا
عَمَّتِي الْمُصْطَفَى، رَضِيَ اللَّهُ تَعَالَى عَنْكَ وَجَعَلَ الْجَنَّةَ مَنْزِلَكَ
وَرَحْمَةً اللَّهِ وَبَرَكَاتُهُ

“Amani iwe juu yenu enyi mashangazi wa Mtume wa Mwenyezi Mungu! Amani iwe juu yenu enyi mashangazi wa Nabii wa Mwenyezi Mungu! Amani iwe juu yenu enyi mashangazi wa hababi wa Mwenyezi Mungu! Amani iwe juu yenu enyi mashangazi wa mteule! Mwenyezi Mungu awe radhi nanyi na afanye Pepo kuwa makazi yenu, na pia rehema za Mwenyezi Mungu na baraka Zake viwe juu yenu.

Namna ya kumzuru Bibi Fatima Ummul-Banina

mama mzazi wa Abul-Fadhli Abbas:

Katika kumzuru Ummul-Banina (a.s.) utasema:

السَّلَامُ عَلَيْكَ يَا زَوْجَةَ وَلِيِّ اللَّهِ، السَّلَامُ عَلَيْكَ يَا زَوْجَةَ
أَمِيرِ الْمُؤْمِنِينَ، السَّلَامُ عَلَيْكَ يَا أُمَّ الْبَنِينَ، السَّلَامُ عَلَيْكَ يَا
أُمَّ الْعَبَّاسِ بْنِ أَمِيرِ الْمُؤْمِنِينَ عَلِيِّ بْنِ أَبِي طَالِبٍ، رَضِيَ اللَّهُ
تَعَالَى عَنْكَ، وَجَعَلَ الْجَنَّةَ مَنْزِلَكَ وَمَأْوِيكَ، وَرَحْمَةَ اللَّهِ
وَبَرَكَاتُهُ

“Amani iwe juu yako ewe mke wa Walii wa Mwenyezi Mungu! Amani iwe juu yako ewe mke wa Amirul-Muuminina! Amani iwe juu yako ewe mama wa watoto wa kiume! Amani iwe juu yako ewe mama yake Abbasi mtoto wa Amirul-Muuminina Ali bin Abu Talib! Mwenyezi Mungu awe radhi nawe na afanye Pepo kuwa makazi yako na mafikio yako, na pia rehema za Mwenyezi Mungu na baraka Zake viwe juu yako.”

Namna ya kumzuru Bwana wetu Aqil naBwana wetu Abdullah bin Ja’far Tayyar (a.s.):

السَّلَامُ عَلَيْكَ يَا سَيِّدَنَا يَا عَقِيلَ بْنَ أَبِي طَالِبٍ، السَّلَامُ عَلَيْكَ يَا
ابْنَ عَمِّ رَسُولِ اللَّهِ، السَّلَامُ عَلَيْكَ يَا ابْنَ عَمِّ نَبِيِّ اللَّهِ، السَّلَامُ

عَلَيْكَ يَا ابْنَ عَمِّ حَبِيبِ اللَّهِ، السَّلَامُ عَلَيْكَ يَا ابْنَ عَمِّ الْهُصَافِيِّ،
السَّلَامُ عَلَيْكَ يَا أَخَا عَلِيٍّ الْهَرْتَمِيِّ، السَّلَامُ عَلَى عَبْدِ اللَّهِ بْنِ
جَعْفَرِ الطَّيْبَارِيِّ الْجِنَانِ، وَعَلَى مَنْ حَوْلَكُمَا مِنْ أَصْحَابِ رَسُولِ
اللَّهِ رَضِيَ اللَّهُ تَعَالَى عَنْكُمَا وَأَرْضَاكُمَا أَحْسَنَ الرِّضَا، وَجَعَلَ
الْجَنَّةَ مَنْزِلِكُمَا وَ مَسْكَنِكُمَا وَ مَحَلَّكُمَا وَمَأْوِيَكُمَا، السَّلَامُ
عَلَيْكُمَا وَرَحْمَةُ اللَّهِ وَبَرَكَاتُهُ

“Amani iwe juu yako ewe Bwana wetu ewe Aqiil bin Abi Talib! Amani iwe juu yako ewe mtoto wa ami yake Mtume wa Mwenyezi Mungu! Amani iwe juu yako ewe mtoto wa ami yake Nabii wa Mwenyezi Mungu! Amani iwe juu yako ewe mtoto wa ami yake hababi wa Mwenyezi Mungu! Amani iwe juu yako ewe mtoto wa ami yake mteule! Amani iwe juu yako ewe ndugu yake Ali al-Murtadha! Amani iwe juu ya Abdullah bin Ja’far mwenye kupaa Peponi, na iwe juu ya wale walio pembezoni mwenu miongoni mwa masahaba wa Mtume wa Mwenyezi Mungu! Mwenyezi Mungu awe radhi nanyi na awaridhishe kwa ridhaa bora kabisa, na aifanye Pepo kuwa mashukio yenu, makazi yenu, mahali penu na mafikio yenu. Amani iwe juu yenu na pia rehema za Mwenyezi Mungu na Baraka Zake.”

Namna ya kuwazuru wahanga:

Katika kuzuru makaburi ya wahanga wa tukio la Hura na wahanga wa Vita vya Uhudi, sema:

السَّلَامُ عَلَيْكُمْ يَا شُهَدَاءُ يَا سُعْدَاءُ يَا نُجَبَاءُ يَا نُقَبَاءُ يَا أَهْلَ
الصِّدْقِ وَالْوَفَاءِ، السَّلَامُ عَلَيْكُمْ يَا مُجَاهِدُونَ فِي سَبِيلِ اللَّهِ
حَقَّ جِهَادِهِ، السَّلَامُ عَلَيْكُمْ بِمَا صَبَرْتُمْ فَنِعْمَ عُقْبَى الدَّارِ،
السَّلَامُ عَلَيْكُمْ يَا شُهَدَاءَ كَافَّةٍ عَامَّةً وَرَحْمَةً اللَّهُ وَبَرَكَاتُهُ

“Amani iwe juu yenu enyi wahanga, enyi wema, enyi waheshimiwa, enyi viongozi wa makabila, enyi wakweli na watekeleza ahadi! Amani iwe juu yenu enyi mliopigana jihadi katika njia ya Mwenyezi Mungu jihadi ya kweli! Amani iwe juu yenu kwa ile subira mliyofanya, basi ni mema yaliyoje matokeo ya nyumba ya Akhera! Amani iwe juu yenu enyi wahanga wote, na pia rehema za Mwenyezi Mungu na Baraka Zake ziwe juu yenu.”

Namna ya kumzuru Bibi Halima Sa'diyya aliyemnyonyesha Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.):

السَّلَامُ عَلَيْكَ يَا أُمَّ رَسُولِ اللَّهِ، السَّلَامُ عَلَيْكَ يَا أُمَّ صَفِيٍّ اللَّهُ،
السَّلَامُ عَلَيْكَ يَا أُمَّ حَبِيبِ اللَّهِ، السَّلَامُ عَلَيْكَ يَا أُمَّ الْبُصْطَفَى،

السَّلَامُ عَلَيْكَ يَا مَرْضِعَةَ رَسُولِ اللَّهِ، السَّلَامُ عَلَيْكَ يَا حَلِيبَةَ
السَّعْدِيَّةِ، فَرَضِيَ اللَّهُ تَعَالَى عَنْكَ وَأَرْضَاكَ، وَجَعَلَ الْجَنَّةَ
مَنْزِلَكَ وَمَأْوَاكَ، وَرَحِمَهُ اللَّهُ وَبَرَكَاتُهُ

“Amani iwe juu yako ewe mama yake Mtume wa Mwenyezi Mungu! Amani iwe juu yako ewe mama yake chaguo bora la Mwenyezi Mungu! Amani iwe juu yako ewe mama yake hababi wa Mwenyezi Mungu! Amani iwe juu yako ewe mama wa mteule wa Mwenyezi Mungu! Amani iwe juu yako ewe uliyemnyonyesha Mtume wa Mwenyezi Mungu! Amani iwe juu yako ewe Halima Sa’diyah! Mwenyezi Mungu awe radhi nawe na akuridhishe, na aifanye pepo kuwa mashukio yako na mafikio yako, na pia rehema za Mwenyezi Mungu na Baraka Zake ziwe juu yako.”

Namna ya kuwazuru walio makaburini:

السَّلَامُ عَلَى أَهْلِ لَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ، مِنْ أَهْلِ لَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ، يَا أَهْلَ لَا
إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ، بِحَقِّ لَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ، كَيْفَ وَجَدْتُمْ قَوْلَ لَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ،
مِنْ لَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ، يَا لَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ، بِحَقِّ لَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ، إِغْفِرْ لِسُنِّ

قَالَ لَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ، وَاحْشُرْنَا فِي زُمْرَةٍ مَّنْ قَالَ لَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ،

مُحَمَّدٌ رَسُولُ اللَّهِ عَلَيَّ وَالْيُومُ الْيَوْمِ

“Amani iwe juu ya watu wa tamko ‘Hapana mungu ila Allah’ kutoka kwa watu wa tamko ‘Hapana mungu ila Allah’! Enyi watu wa ‘Hapana mungu ila Allah’ kwa haki ya ‘Hapana mungu ila Allah’ mmeikutaje kauli ‘Hapana mungu ila Allah’ toka kwa ‘Hapana mungu ila Allah’! Ewe Ambaye ‘Hapana mungu ila Allah’ kwa haki ya ‘Hapana mungu ila Allah’ mghufirie aliyesema ‘Hapana mungu ila Allah’ na utikusanye katika kundi la waliosema ‘Hapana mungu ila Allah, Muhammad ni Mtume wa Mwenyezi Mungu na Ali ni Walii wa Mwenyezi Mungu.”

Kutoka kwa Ali Amirul-Muuminina (a.s.): “Atakayeingia makaburini na akasoma ziyara Mwenyezi Mungu atampa thawabu za ibada ya miaka hamsini, na atamfutia madhambi yake na ya wazazi wake ya miaka hamsini.”

Na kutoka kwa Mtume (s.a.w.w.): “Atakayesoma Surat al-Qadri mara saba kwenye kaburi la muumini Mwenyezi Mungu atamtumia malaika atakayekuwa akimwabudu Mwenyezi Mungu kwenye kaburi lake, na thawabu za matendo ya huyo malaika atamwandikia maiti huyo, hivyo Mwenyezi Mungu atakapomfufua toka kaburini kwake hatopita kwenye msukosuko ila Mwenyezi Mungu atamwondolea msukosuko huo kwa amali hizo mpaka aingie Peponi.”

Ni Sunna baada ya kusoma Sura al-Qadri mara saba usome Alhamdu na Sura Nasi na Sura al-Falaqi, na Sura Ikhlas na

Ayati Kursiyyu, kila moja mara tatu. Na katika riwaya ni kwamba asome hayo na hali akiwa ameelekea Kibla.

Namna ya kumzuru Bwana wetu Ismail mtoto wa Imam Ja'far as-Sadiq (a.s.):

اَلسَّلَامُ عَلٰى جَدِّكَ اَلْمُصْطَفٰى، اَلسَّلَامُ عَلٰى اَبِيكَ اَلْمُرْتَضٰى
الرِّضَا، اَلسَّلَامُ عَلٰى السَّيِّدِيْنِ اَلْحَسَنِ وَ اَلْحُسَيْنِ، اَلسَّلَامُ عَلٰى
خَدِيْجَةَ اُمِّ الْمُؤْمِنِيْنَ اُمِّ سَيِّدَةِ نِسَاءِ الْعَالَمِيْنَ، اَلسَّلَامُ عَلٰى
فاطمة اُمِّ الْاَيْمَةِ الطَّاهِرِيْنَ، اَلسَّلَامُ عَلٰى التُّفُوْسِ الْفَاخِرَةِ،
بُحُوْرِ الْعُلُوْمِ الزَّاخِرَةِ، شُفْعَاىِ فِي الْاٰخِرَةِ، وَ اَوْلِيَاىِ عِنْدَ عَوْدِ
الرُّوْحِ اِلَى الْعِظَامِ النَّخِرَةِ، اُنْبِيَّةِ الْخَلْقِ وَ وِلَاةِ الْحَقِّ، اَلسَّلَامُ
عَلَيْكَ اَيُّهَا الشَّخْصُ الشَّرِيْفُ، اِسْمَاعِيْلُ بْنُ مَوْلَانَا جَعْفَرُ بْنُ
مُحَمَّدِ الصَّادِقِ الطَّاهِرِ الْكَرِيْمِ، اَشْهَدُ اَنْ لَا اِلَهَ اِلَّا اللهُ، وَاَنْ
مُحَمَّدًا عَبْدُهُ وَ مُصْطَفِيْهِ، وَاَنْ عَلِيًّا وَلِيُّهُ وَ مُجْتَبَاُهُ، وَاَنْ
الْاِمَامَةَ فِيْ وُلْدِهِ اِلَى يَوْمِ الدِّيْنِ، نَعَلَمَ ذَلِكَ عَلِمَ الْيَقِيْنِ، وَ نَحْنُ
لِذَلِكَ مُعْتَقِدُوْنَ، وَ فِيْ نَصْرِهِمْ مُجْتَهَدُوْنَ

“Amani iwe juu ya babu yako al-Mustafa! Amani iwe juu ya baba yako al-Murtadha! Amani iwe juu ya mabwana wawili Hasan na Husain! Amani iwe juu ya Khadija mama wa waumini mama yake na mbora wa wanawake wote wa ulimwengu! Amani iwe juu ya Fatima mama wa Maimamu watakasifu! Amani iwe juu ya nafsi bora, bahari za elimu zenye kujaa, waombezi wangu huko akhera na viongozi wangu pindi roho itakaporejea kwenye mifupa iliyoharibika, Maimamu wa viumbe na viongozi wa haki! Amani iwe juu yako ewe mtu sharifu Ismail mtoto wa maulana Ja’far bin Muhammad as-Sadiq (a.s.) mtakasifu aliye mkarimu. Nashahidilia kwamba hapana mungu ila Allah na hakika Muhammad ni mja Wake na ndiye aliyemteua, na hakika Ali ni Walii Wake na mteule Wake, na hakika Uimamu ni katika kizazi chake mpaka siku ya hukumu, tunayajua hayo kwa elimu ya yakini na sisi ni wenye kuyaitakidi hayo na ni wenye kutoa juhudi katika kuwasaidia wao.”

Namna ya kumzuru Bwana wetu Abdullah bin Abdul-Muttalib baba mzazi wa Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.):

Alifariki alipokuwa akirudi toka Sham, na ilikuwa ni kabla ya kuzaliwa Mtume (s.a.w.w.). Kaburi lake lipo karibu na soko. Na kwa hivi sasa kuwa katika eneo la kusalia na hali umeelekea Mlango wa Salamu (Babus-Salam) na useme:

السَّلَامُ عَلَيْكَ يَا وَلِيَّ اللَّهِ، السَّلَامُ عَلَيْكَ يَا أَمِينَ اللَّهِ، السَّلَامُ عَلَيْكَ يَا نُورَ اللَّهِ، السَّلَامُ عَلَيْكَ يَا مُسْتَوْدَعَ نُورِ رَسُولِ اللَّهِ،

السَّلَامُ عَلَيْكَ يَا وَالدَّ خَاتِمَ الْأَنْبِيَاءِ، السَّلَامُ عَلَيْكَ يَا مَنْ
 اتَّهَى إِلَيْهِ الْوَدِيعَةُ وَالْأَمَانَةُ الْبَنِيْعَةُ، السَّلَامُ عَلَيْكَ يَا مَنْ
 أَوْدَعَ اللَّهُ فِي صُلْبِهِ الطَّيِّبِ الطَّاهِرِ الْبَكِيْنِ نُورَ رَسُوْلِ اللَّهِ الصَّادِقِ
 الْأَمِيْنِ، السَّلَامُ عَلَيْكَ يَا وَالدَّ سَيِّدِ الْأَنْبِيَاءِ وَالْمُرْسَلِيْنَ،

أَشْهَدُ أَنَّكَ قَدْ حَفِظْتَ الْوَصِيَّةَ، وَأَدَيْتَ الْأَمَانَةَ عَنْ رَبِّ
 الْعَالَمِيْنَ فِي رَسُوْلِهِ، وَكُنْتَ فِي دِيْنِكَ عَلَى يَقِيْنٍ، وَأَشْهَدُ أَنَّكَ
 اتَّبَعْتَ دِيْنَ اللَّهِ عَلَى مِنْهَاجِ جَدِّكَ إِبْرَاهِيْمَ حَمِيْلِ اللَّهِ فِي حَيَاتِكَ
 وَبَعْدَ وَفَاتِكَ، عَلَى مَرْضَاتِ اللَّهِ فِي رَسُوْلِهِ، وَأَقْرَرْتَ وَصَدَّقْتَ
 بِنُبُوَّةِ رَسُوْلِ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ، وَوَلَايَةِ أَمِيْرِ الْمُؤْمِنِيْنَ
 عَلَيْهِ السَّلَامُ، وَالْأَيْمَةِ الطَّاهِرِيْنَ عَلَيْهِمُ السَّلَامُ، فَصَلَّى اللَّهُ
 عَلَيْكَ حَيًّا وَمَيِّتًا، وَرَحْمَةً اللَّهُ وَبَرَكَاتُهُ

“Amani iwe juu yako ewe Walii wa Mwenyezi Mungu!
 Amani iwe juu yako ewe mwaminifu wa Mwenyezi
 Mungu! Amani iwe juu yako ewe nuru ya Mwenyezi
 Mungu! Amani iwe juu yako ewe hifadhi ya nuru ya
 Mtume wa Mwenyezi Mungu! Amani iwe juu yako ewe

mzazi wa mwisho wa Manabii! Amani iwe juu yako ewe ambaye kwake imekomea amana nzito! Amani iwe juu yako ewe ambaye Mwenyezi Mungu aliweka katika mifupa ya mgongo wake safi mtakasifu na uliohifadhika nuru ya Mtume wa Mwenyezi Mungu msema kweli mwaminifu! Amani iwe juu yako ewe mzazi wa mbora wa Manabii na Mitume!

“Nashahidilia kwamba hakika wewe ulihifadhi wosia na ukatekeleza amana kutoka kwa Mola Mlezi wa walimwengu kuhusu Mtume Wake, na ulikuwa katika yakini na dini yako. Na nashahidilia kwamba hakika wewe ulifuata dini ya Mwenyezi Mungu katika uhai wako na baada ya kufa kwako kwa kufuata nyayo za babu yako Ibrahim Khalili wa Mwenyezi Mungu, na kwa kufuata yale aliyomridhia Mwenyezi Mungu Mtume Wake. Ulikiri na kusadikisha unabii wa Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) na uongozi wa Amirul-Muuminina (a.s.) na wa Maimamu watakasifu (a.s.), hivyo Mwenyezi Mungu akusalie uwapo hai na uwapo maiti, na pia rehema za Mwenyezi Mungu na Baraka Zake ziwe juu yako.”

Ziyara ya pili:

السَّلَامُ عَلَيْكَ يَا صَاحِبَ الْبَجْدِ الْاَثِيْلِ، السَّلَامُ عَلَيْكَ يَا خَيْرَةَ
فَرْعٍ مِنْ دَوْحَةِ الْخَلِيْلِ، السَّلَامُ عَلَيْكَ يَا ابْنَ الدِّيْبِ
اِسْمَاعِيْلَ، السَّلَامُ عَلَيْكَ يَا سُلَالَةَ الْاَبْرَارِ، السَّلَامُ عَلَيْكَ يَا اَبَا
النَّبِيِّ الْبُخْتَارِ، وَعَمَّ الْوَصِيَّ الْكَرَّارِ، وَوَالِدَ الْاَنْبِيَّةِ الْاَطْهَارِ،

أَسْلَامُ عَلَيْكَ يَا مَنْ أَضَاءَتْ بِنُورِ جَبِينِهِ عِنْدَ وِلَادَتِهِ أَطْرَافُ
 السَّمَاءِ، أَسْلَامُ عَلَيْكَ يَا يُوسُفَ آلِ عَبْدِ مَنَافٍ، أَسْلَامُ
 عَلَيْكَ يَا مَنْ سَلَكَ مَسْلَكَ جَدِّهِ إِسْمَاعِيلَ، فَاسْأَلْهُ لِأَبِيهِ
 لِيَذُبَّ عَنْهُ، أَسْلَامُ عَلَيْكَ يَا مَنْ فَدَاكَ اللهُ بِمَا فَدَاكَ، فَتَقَبَّلَهُ
 فَأَعْطَاكَ اللهُ وَأَبَاكَ، أَسْلَامُ عَلَيْكَ يَا حَامِلَ نُورِ النُّبُوَّةِ، أَسْلَامُ
 عَلَيْكَ يَا أَشْرَفَ النَّاسِ فِي الْأَبُوَّةِ وَالْبُنُوَّةِ، أَسْلَامُ عَلَيْكَ يَا وَالِدَ
 خَاتِمِ النَّبِيِّينَ، أَسْلَامُ عَلَيْكَ يَا أَبَا الطَّاهِرِينَ بَعْدَ الطَّاهِرِينَ،
 وَابْنَ الطَّاهِرِينَ، وَرَحْمَةَ اللهِ وَبَرَكَاتُهُ

“Amani iwe juu yako ewe mwenye utukufu wa asili!
 Amani iwe juu yako ewe tawi bora toka katika mti wa
 Khalili! Amani iwe juu yako ewe mtoto wa dhabihu Ismail!
 Amani iwe juu yako ewe asili ya watu wema! Amani iwe
 juu yako ewe baba yake na Nabii mteule, ami yake Wasii
 imara na mzazi wa Maimamu watakasifu! Amani iwe juu
 yako ewe ambaye aliziangaza pande za mbingu kwa nuru
 ya paji lake wakati wa kuzaliwa kwake! Amani iwe juu
 yako ewe Yusufu wa aali Abdu Manafi! Amani iwe juu
 yako ewe ambaye alifuata mwenendo wa babu yake
 Ismail, akajisalimisha kwa baba yake ili amchinje! Amani
 iwe juu yako ewe ambaye Mwenyezi Mungu alimfidia kwa
 fidia Yake akaikubali, Mwenyezi Mungu akampa yeye na

baba yake! Amani iwe juu yako ewe uliyebeba nuru ya unabii! Amani iwe juu yako ewe uliye mbora kushinda watu wote katika ubaba na utoto! Amani iwe juu yako ewe mzazi wa mwisho wa Manabii! Amani iwe juu yako ewe baba wa watakasifu baada ya watakasifu na mtoto wa watakasifu! Pia rehema za Mwenyezi Mungu na Baraka Zake ziwe juu yako.”

Namna ya kumuaga Mtume (s.a.w.w.):

Ewe mheshimiwa hujaji! Utakapotaka kusafiri toka Madina maliza haja zako zote, oga na vaa nguo safi mno kati ya zile ulizonazo, na kisha nenda kumzuru Mtume (s.a.w.w.), mzuru kwa kusoma zile ziyara zilizotangulia na kisha muage kwa kumwambia:

اَلسَّلَامُ عَلَیْكَ يَا رَسُوْلَ اللهِ، اَلسَّلَامُ عَلَیْكَ اَیُّهَا الْبَشِيْرُ
 النَّذِيْرُ، اَلسَّلَامُ عَلَیْكَ اَیُّهَا السِّرَاجُ الْبُنِيْرُ، اَلسَّلَامُ عَلَیْكَ اَیُّهَا
 السَّفِيْرُ بَيْنَ اللهِ وَبَيْنَ خَلْقِهِ، اَشْهَدُ يَا رَسُوْلَ اللهِ اَنَّكَ كُنْتَ نُوْرًا
 فِي الْاَصْلَابِ الشَّامِخَةِ، وَالْاَرْحَامِ الْبَطْهَرَةِ، لَمْ تُنَجِّسْكَ
 الْجَاهِلِيَّةُ بِاَنْجَاسِهَا، وَلَمْ تُلْبَسْكَ مِنْ مُدْلَهَاتِ ثِيَابِهَا،
 وَاَشْهَدُ يَا رَسُوْلَ اللهِ اَنَّيْ مُؤْمِنٌ بِكَ وَبِالْاَيْتَةِ مِنْ اَهْلِ بَيْتِكَ
 مُوقِنٌ بِجَمِيْعِ مَا اَتَيْتَ بِهِ رَاضٍ مُؤْمِنٌ، وَاَشْهَدُ اَنَّ الْاَيْتَةَ مِنْ

أَهْلِ بَيْتِكَ أَعْلَامُ الْهُدَى، وَالْعُرْوَةُ الْوُثْقَى، وَالْحُجَّةُ عَلَى أَهْلِ
 الدُّنْيَا، اللَّهُمَّ لَا تَجْعَلْهُ آخِرَ الْعَهْدِ مِنْ زِيَارَةِ نَبِيِّكَ عَلَيْهِ
 وَآلِهِ السَّلَامُ، وَإِنْ تَوَقَّيْتَنِي فَإِنِّي أَشْهَدُ فِي مَبَاتِي عَلَى مَا أَشْهَدُ
 عَلَيْهِ فِي حَيَاتِي أَنَّكَ أَنْتَ اللَّهُ لَا إِلَهَ إِلَّا أَنْتَ وَحْدَكَ لَا شَرِيكَ لَكَ،
 وَأَنَّ مُحَمَّدًا عَبْدُكَ وَرَسُولُكَ، وَأَنَّ الْأَيْمَةَ مِنْ أَهْلِ بَيْتِهِ
 أَوْلِيَاؤُكَ وَأَنْصَارُكَ وَحُجَجُكَ عَلَى خَلْقِكَ، وَخُلَفَاؤُكَ فِي
 عِبَادِكَ، وَأَعْلَامُكَ فِي بِلَادِكَ، وَخُزَّانُ عِلْمِكَ، وَحَفَظَةُ سِرِّكَ،
 وَتَرَاجِمَةُ وَحْيِكَ، اللَّهُمَّ صَلِّ عَلَى مُحَمَّدٍ وَآلِ مُحَمَّدٍ، وَبَدِّعْ
 رُوحَ نَبِيِّكَ مُحَمَّدٍ وَآلِهِ فِي سَاعَتِي هَذِهِ وَفِي كُلِّ سَاعَةٍ تَحِيَّةً مِنِّي
 وَسَلَامًا، وَالسَّلَامُ عَلَيْكَ يَا رَسُولَ اللَّهِ وَرَحْمَةُ اللَّهِ وَبَرَكَاتُهُ، وَلَا
 جَعَلَهُ اللَّهُ آخِرَ تَسْلِيمِي عَلَيْكَ

“Amani iwe juu yako ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu!
 Amani iwe juu yako ewe mtoa habari njema na mwonyaji!
 Amani iwe juu yako ewe taa itoayo nuru! Amani iwe juu
 yako ewe balozi baina ya Mwenyezi Mungu na viumbe
 Wake! Nashahidilia ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu
 kwamba hakika wewe ulikuwa nuru katika mifupa ya

migongo mitukufu na vizazi vitakasifu, ujahiliya haujakuchafua kwa uchafu wake wala giza halijakuvisha vazi lake. Nakiri ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu kwamba hakika mimi ni mwenye kukuamini wewe na Maimamu toka katika watu wa nyumba yako. Na ni mwenye yakini na yote uliyoleta, na ni mwenye kuridhia na kuamini. Na ninakiri kwamba hakika maimamu toka katika watu wa nyumba yako ni bendera za uongofu, shikio madhubuti na hoja juu ya wakazi wa duniani.

“Ewe Mwenyezi Mungu! Usiifanye hii kuwa ndio ahadi yangu ya mwisho ya kumzuru Nabii Wako (a.s.), na kama utanifisha basi hakika mimi nashahidilia katika mauti yangu yale ninayoshahidilia katika uhai wangu, kwamba hakika Wewe ni Allah hapana mungu ila Wewe peke Yako hauna mshirika, na kwamba hakika Muhammad ni mja Wako na Mtume Wako, na kwamba hakika Maimamu toka katika watu wa nyumba yake ni vipenzi Vyako, wasaidizi Wako na hoja Wako juu ya viumbe Vyako, ni makhalfi Wako kwa waja Wako, bendera Zako katika nchi Yako, wahazini wa elimu Yako, hifadhi ya siri Yako na wafafanuzi wa Wahyi Wako.

“Ewe Mwenyezi Mungu! Msalie Muhammad na aali Muhammad na ifikishie roho ya Nabii Wako Muhammad na za aali zake maamkizi na salamu kutoka kwangu, katika saa yangu hii na katika kila saa. Amani iwe juu yako ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu, na pia rehema za Mwenyezi Mungu na Baraka Zake ziwe juu yako. Mwenyezi Mungu asifanye kuwa ndio mwisho wa mimi kukutolea salamu.”

Kisha sema:

اللَّهُمَّ لَا تَجْعَلْهُ آخِرَ الْعَهْدِ مِنْ زِيَارَةِ قَبْرِ نَبِيِّكَ، فَإِنْ تَوَقَّيْتَنِي
 قَبْلَ ذَلِكَ، فَإِنِّي أَشْهَدُ فِي مَبَاتِي عَلَى مَا أَشْهَدُ عَلَيْهِ فِي حَيَاتِي،
 أَنْ لَا إِلَهَ إِلَّا أَنْتَ، وَأَنْ مُحَمَّدًا عَبْدُكَ وَرَسُولُكَ، وَأَنَّكَ قَدْ
 اخْتَرْتَهُ مِنْ خَلْقِكَ، ثُمَّ اخْتَرْتَ مِنْ أَهْلِ بَيْتِهِ الْأَيْمَّةَ الطَّاهِرِينَ،
 الَّذِينَ أَذْهَبْتَ عَنْهُمْ الرِّجْسَ وَطَهَّرْتَهُمْ تَطْهِيرًا، فَاحْشُرْنَا مَعَهُمْ،
 وَفِي رُؤْمَرْتِهِمْ وَتَحْتَ لَوَائِهِمْ، وَلَا تُفَرِّقْ بَيْنَنَا وَبَيْنَهُمْ فِي الدُّنْيَا
 وَالْآخِرَةِ، يَا أَرْحَمَ الرَّاحِمِينَ السَّلَامُ عَلَيْكَ لَا جَعَلَهُ اللَّهُ آخِرَ
 تسليبي عليك.

“Ewe Mwenyezi Mungu! Usiifanye kuwa ni ahadi yangu
 ya mwisho ya kulizuru kaburi la Nabii Wako, kwani iwapo
 utanifisha kabla ya hilo (kulizuru tena) basi mimi
 nashahidilia katika mauti yangu yale ninayoshahidilia
 katika uhai wangu, kwamba hapana mungu ila Wewe, na
 kwamba hakika Muhammad ni mja Wako na Mtume
 Wako, na kwamba hakika Wewe umemchagua toka katika
 viumbe Wako, kisha ukachagua toka katika watu wa
 nyumba yake Maimamu watakasifu ambao uliwaondolea
 uchafu na ukawatakasa sanasana, hivyo tukusanye pamoja
 nao na katika kundi lao na chini ya bendera yao, na wala
 usitutenganishe sisi na wao duniani na akhera, ewe
 Mwenye kurehemu kushinda wote wenye kurehemu.

Amani iwe juu yako na Mwenyezi Mungu asifanye kuwa ndio mwisho wa mimi kukutolea salamu.”

Ziyara ya kuwaaga Maimamu huko Baqii:

Ewe mheshimiwa hujaji! Baada ya kulizuru kaburi la Mtukufu Mtume wako (s.a.w.w.) na kumuaga kwa ziyara iliyotangulia, sasa elekea Baqii ili ukawaage Maimamu wako wanne (a.s.) na wazuru kwa ziyara zao zilizotangulia, kisha waage. Sheikh na Sayyid bin Tawuus amesema: Katika kuwaaga sema:

السَّلَامُ عَلَيْكُمْ أَيُّهَا الْهُدَى وَرَحْمَةُ اللَّهِ وَبَرَكَاتُهُ، اسْتَوْدِعُكُمْ اللَّهُ
وَأَقْرَأُ عَلَيْكُمْ السَّلَامَ، أَمَّا بِاللَّهِ وَبِالرَّسُولِ، وَبِهَا جِئْتُمْ بِهِ
وَدَلَّيْتُمْ عَلَيْهِ، اللَّهُمَّ فَاكْتُبْنَا مَعَ الشَّاهِدِينَ وَلَا تَجْعَلْهُ آخِرَ
العهد من زيارتهم والسلام عليهم ورحمة الله وبركاته.

“Amani iwe juu yenu enyi Maimamu wa uongofu na pia rehema za Mwenyezi Mungu na baraka Zake! Nawaacha nyinyi kwa Mwenyezi Mungu na ninawasomea salamu. Tumemwamini Mwenyezi Mungu, Mtume na yale mliyokuja nayo na kutujulisha. Ewe Mwenyezi Mungu tuandike pamoja na mashahidi. Na wala usiifanye kuwa ndio ahadi ya mwisho ya mimi kuwazuru. Amani iwe juu yenu na rehema za Mwenyezi Mungu na Baraka Zake.”

NAMNA YA KUWAZURU MAASUMINA KUMI NA WANNE KATIKA SIKU SABA ZA JUMA

Ziyara ya Mtume wa Mwenyezi Mungu siku ya Jumamosi:

Imetajwa kwamba katika kumzuru Mtume wa Mwenyezi
Mungu siku ya Jumamosi sema:

أَشْهَدُ أَنْ لَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ وَحْدَهُ لَا شَرِيكَ لَهُ وَأَشْهَدُ أَنَّكَ رَسُولُهُ
وَأَنَّكَ مُحَمَّدُ بْنُ عَبْدِ اللَّهِ وَأَشْهَدُ أَنَّكَ قَدْ بَلَغْتَ رِسَالَاتِ رَبِّكَ
وَنَصَحْتَ لِأُمَّتِكَ وَجَاهَدْتَ فِي سَبِيلِ اللَّهِ بِالْحِكْمَةِ وَالْمَوْعِظَةِ
الْحَسَنَةِ وَأَدَيْتَ الَّذِي عَلَيْكَ مِنَ الْحَقِّ وَأَنَّكَ قَدْ رُوِّفْتَ
بِالْبُؤْمِنِينَ وَغَلَطْتَ عَلَى الْكَافِرِينَ وَعَبَدْتَ اللَّهَ مُخْلِصًا حَتَّى
أَتَاكَ الْيَقِينُ فَبَدَّخَ اللَّهُ بِكَ أَشْرَفَ مَحَلِّ الْبُكْرَمِيِّينَ

الْحَمْدُ لِلَّهِ الَّذِي اسْتَنْقَذَنَا بِكَ مِنَ الشِّرْكِ وَالضَّلَالِ اللَّهُمَّ
صَلِّ عَلَى مُحَمَّدٍ وَآلِهِ وَاجْعَلْ صَلَوَاتِكَ وَصَلَوَاتِ مَلَائِكَتِكَ
الْبُقَرَّاءِ وَأَنْبِيَاءِكَ الْمُرْسَلِينَ وَعِبَادِكَ الصَّالِحِينَ وَأَهْلِي

السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضِينَ وَمَنْ سَبَّحَ لَكَ يَا رَبَّ الْعَالَمِينَ مِنْ
الْأُولَى وَالْآخِرِينَ عَلَى مُحَمَّدٍ عَبْدِكَ وَرَسُولِكَ وَنَبِيِّكَ
وَأَمِينِكَ وَنَجِيبِكَ وَحَبِيبِكَ وَصَفِيِّكَ وَصَفْوَتِكَ وَخَاصَّتِكَ
وَخَالِصَّتِكَ وَخَيْرَتِكَ مِنْ خَلْقِكَ وَأَعْطِهِ الْفُضْلَ وَالْفَضِيلَةَ
وَالْوَسِيلَةَ وَالذَّرَجَةَ الرَّفِيعَةَ وَالْبَعْثَهُ مَقَاماً مَحْمُوداً يَغْبِطُهُ بِهِ
الْأَوْلُونَ وَالْآخِرُونَ

اللَّهُمَّ إِنَّكَ قُلْتَ وَلَوْ أَنَّهُمْ إِذْ ظَلَمُوا أَنفُسَهُمْ جَاءُوكَ فَاسْتَغْفَرُوا
اللَّهَ وَاسْتَغْفَرَ لَهُمُ الرَّسُولُ لَوَجَدُوا اللَّهَ تَوَّاباً رَحِيماً. إلهي فَقَدْ
أَتَيْتُ نَبِيَّكَ مُسْتَغْفِراً تَائِباً مِنْ ذُنُوبِي فَصَلِّ عَلَيَّ مُحَمَّدَ وَآلِهِ وَ
أَغْفِرْهَا لِي، يَا سَيِّدَنَا أَتَوَجَّهُ بِكَ وَبِأَهْلِ بَيْتِكَ إِلَى اللَّهِ تَعَالَى
رَبِّكَ وَرَبِّي لِيَغْفِرَ لِي إِنَّ اللَّهَ وَإِنَّا إِلَيْهِ رَاجِعُونَ إِنَّ اللَّهَ وَإِنَّا إِلَيْهِ
رَاجِعُونَ إِنَّ اللَّهَ وَإِنَّا إِلَيْهِ رَاجِعُونَ

أُصِبْنَا بِكَ يَا حَبِيبَ قُلُوبِنَا فَمَا أَعْظَمَ الْبُصِيْبَةَ بِكَ حَيْثُ انْقَطَعَ
 عَنَّا الْوَحْيُ وَحَيْثُ فَقَدْنَاكَ فَإِنَّ اللَّهَ وَإِنَّا إِلَيْهِ رَاجِعُونَ يَا سَيِّدَنَا يَا
 رَسُولَ اللَّهِ صَلَوَاتُ اللَّهِ عَلَيْكَ وَعَلَى آلِ بَيْتِكَ الطَّاهِرِينَ هَذَا
 يَوْمُ السَّبْتِ وَهُوَ يَوْمُكَ وَأَنَا فِيهِ ضَيْفُكَ وَجَارُكَ فَأَضِيفْنِي وَاجْرِنِي
 فَإِنَّكَ كَرِيمٌ تُحِبُّ الضِّيَافَةَ وَمَأْمُورٌ بِالْإِجَارَةِ فَأَضِيفْنِي وَأَحْسِنْ
 ضِيَافَتِي وَاجْرِنَا وَأَحْسِنْ إِجَارَتَنَا بِمَنْزِلَةِ اللَّهِ عِنْدَكَ وَعِنْدَ آلِ
 بَيْتِكَ وَبِمَنْزِلَتِهِمْ عِنْدَهُ وَبِمَا اسْتَوْدَعَكُمْ مِنْ عِلْمِهِ فَإِنَّهُ أَكْرَمُ
 الْأَكْرَمِينَ

“Nashahidilia kwamba hapana mungu ila Allah peke Yake hana mshirika. Na nashahidilia kwamba hakika wewe ni Mtume Wake na hakika wewe ni Muhammad bin Abdullah. Na nashahidilia kwamba hakika wewe umefikisha ujumbe wote wa Mola Wako Mlezi, umeunasihi Ummah wako, umejitolea katika njia ya Mwenyezi Mungu kwa hekima na mawaidha mazuri, na umefikisha haki iliyokuwa wajibu juu yako. Na hakika wewe umekuwa na huruma kwa waumini na mkali kwa makafiri, umemwabudu Mwenyezi Mungu kwa ikhlasi mpaka kifo kilipokufika, hivyo Mwenyezi Mungu akakufikisha kwenye kilele cha ubora wa sehemu ya wale waliotukuzwa.

“Kila sifa njema ni ya Mwenyezi Mungu aliyetuepusha na Shiriki na upotovu kupitia Kwako. Ewe Mwenyezi Mungu! Msalie Muhammad na aali zake na weka sala Zako na sala za malaika Wako, za Manabii Wako waliotumwa, za waja Wako wema, za wakazi wa mbinguni na ardhini, na za kila aliyekutakasa ewe Mola Mlezi wa viumbe wote kuanzia za wale waliotangulia mpaka za wale watakaofuatia, juu ya Muhammad mja Wako, Mtume Wako, Nabii Wako, mwaminifu Wako, msiri Wako, kipenzi Chako, mteule Wako, chaguo Lako bora, muhtasi Wako, makhsusi Wako na chaguo Lako miongoni mwa viumbe Wako. Mpe ubora na fadhila, wasila na daraja la juu, na muinue cheo kinachosifika, chenye kutamaniwa na waliotangulia na watakaokuja.

“Ewe Mwenyezi Mungu! Hakika Wewe umesema: **“Na lau wangelikujia walipojidhulumu nafsi zao wakaomba msamaha kwa Mwenyezi Mungu, na Mtume akawaombea msamaha, bila shaka wangemkuta Mwenyezi Mungu, Mwenye kupokea toba, Mwenye kurehemu.”** Ilahi! Nami nimemjia Nabii Wako na hali ni mwenye kuomba maghfira na mwenye kutubia dhambi zangu, basi msalie Muhammad na aali zake na nighufirie dhambi zangu. Ewe bwana wetu! kupitia kwako na kwa watu wa nyumba yako naelekea kwa Mwenyezi Mungu Mola Wako Mlezi na Mola Wangu Mlezi ili anighufirie. Hakika sisi sote ni wa Mwenyezi Mungu na Kwake tutarejea. Hakika sisi sote ni wa Mwenyezi Mungu na Kwake tutarejea. Hakika sisi sote ni wa Mwenyezi Mungu na Kwake tutarejea.

“Tumepatwa na msiba wako ewe kipenzi cha nyoyo zetu, ni msiba mkubwa ulioje msiba wako! kwani tumekatikiwa na wahyi na tumekupoteza, hakika sisi sote ni wa

Mwenyezi Mungu na Kwake Yeye tutarejea. Ewe bwana wetu! Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu! Sala za Mwenyezi Mungu ziwe juu yako na juu ya watu wa nyumba yako wema watakasifu. Hii ni siku ya Jumamosi nayo ndio siku yako na mimi ni mgeni Wako humo na jirani yako, hivyo upokee ugeni wangu na niweke jirani, kwani hakika wewe ni mkarimu unapenda ugeni na umeamrisha kukubali ujirani, upokee ugeni wangu na uenzi vilivyo ugeni wangu, tufanye majirani na uenzi vilivyo ujirani wetu kwa cheo cha Mwenyezi Mungu ulicho nacho na kilichopo kwa watu wa nyumba yako, na kwa cheo chao Kwake, na kwa elimu Yake aliyoiweka kwenu, kwani hakika Yeye ni mkarimu kushinda wakarimu wote.”

Ziyara ya Amirul-Muuminina siku ya Jumapili:

Alishuhudiwa Sahibuz-Zaman al-Mahdi (a.s.) katika ziyara ya kumzuru (a.s.) siku ya Jumapili akisema:

السَّلَامُ عَلَى الشَّجَرَةِ النَّبَوِيَّةِ وَالِدَّوْحَةِ الْهَاشِيَّةِ الْبُضِيَّةِ
 الْبُشَيْرَةِ بِالنَّبَوَّةِ الْمُنْقَذَةِ بِالإِمَامَةِ وَعَلَى ضَجِيعِكَ أَدَمَ وَنُوحَ
 عَلَيْهِمَا السَّلَامُ، السَّلَامُ عَلَيْكَ وَعَلَى أَهْلِ بَيْتِكَ الطَّيِّبِينَ
 الطَّاهِرِينَ، السَّلَامُ عَلَيْكَ وَعَلَى الْمَلَائِكَةِ الْمُحَدِّقِينَ بِكَ
 وَالْحَاقِّينَ بِقَبْرِكَ يَا مَوْلَايَ يَا أَمِيرَ الْمُؤْمِنِينَ هَذَا يَوْمُ الْأَحَدِ وَهُوَ

يَوْمَكَ وَبِاسْمِكَ وَأَنَا صَيِّفُكَ فِيهِ وَ جَارُكَ فَأَضْفُنِي يَا مَوْلَايَ
وَأَجِرْنِي فَإِنَّكَ كَرِيمٌ تُحِبُّ الضِّيَافَةَ وَمَأْمُورٌ بِالْإِجَارَةِ فَافْعَلْ مَا
رَغِبْتُ إِلَيْكَ فِيهِ وَرَجَوْتُهُ مِنْكَ بِمَنْزِلَتِكَ وَ آلِ بَيْتِكَ عِنْدَ اللَّهِ
وَمَنْزِلَتِهِ عِنْدَكُمْ وَبِحَقِّ ابْنِ عَبَّكَ رَسُولِ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ
وَأَلِهِ وَسَلَّمَ وَعَلَيْهِمْ أَجْمَعِينَ

“Amani iwe juu ya mti wa unabii, mti wa Kihashimiya, wenye kuangaza, wenye kutoa matunda kupitia unabii, yaliyowiva kupitia uimamu, na iwe juu ya mbavu zako mbili Adam na Nuh (a.s.)! Amani iwe juu yako na juu ya watu wa nyumba yako wema watakasifu! Amani iwe juu yako na juu ya Malaika waliokuzunguka waliojaa na kulizunguka kaburi lako! Ewe kiongozi wangu! Ewe Amirul-Muuminina! Hii ni siku ya Jumapili nayo ndio siku yako na ya jina lako na mimi ni mgeni wako humu na jirani yako, hivyo upokee ugeni wangu ewe kiongozi wangu na niweke jirani, kwani hakika wewe ni mkarimu unapenda ugeni na umeamrisha kukubali ujirani, tenda yale niliyotamani kwako humu na niliyoyataraji toka kwako, kwa cheo ulichonacho na walicho nacho watu wa nyumba yako kwa Mwenyezi Mungu, na kwa cheo Chake alichonacho kwenu, na kwa haki ya binamu yako Mtume wa Mwenyezi Mungu sala na salamu za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake na juu ya aali zake, ziwe juu yao na juu yenu nyote.”

Ziyara ya Zahra (a.s.):

Ameitaja Allama al-Majlisiy katika mlango wa ziyara za katika siku saba za juma:

السَّلَامُ عَلَيْكَ يَا مُتَّحِنَةً اُمْتَحَنَكَ الَّذِي خَلَقَكَ فَوَجَدَكَ لَهَا
اُمْتَحَنَكَ صَابِرَةً اَنَا لِكَ مُصَدِّقٌ صَابِرٌ عَلَى مَا آتَى بِهِ اَبُوكِ
وَوَصِيَّهُ صَلَوَاتُ اللّٰهِ عَلَيْهَا. وَاَنَا اَسْأَلُكَ اِنْ كُنْتُ صَدَّقْتُكَ اِلَّا
اَلْحَقَّتَنِي بِتَصَدِيقِي لَهَا لِتَسَّرَ نَفْسِي فَاَشْهَدِي اَنِّي ظَاهِرٌ
بِوَلَايَتِكَ وَوَلَايَةِ آلِ بَيْتِكَ صَلَوَاتُ اللّٰهِ عَلَيْهِمْ اَجْمَعِينَ

“Amani iwe juu yako ewe mtahiniwa ambaye amekutahini Yule aliyekuumba, akakukuta ni mwenye subira kwa yale aliyokutahini! Mimi ni mwenye kukusadiki wewe na ni mwenye subira juu ya yale aliyoyaleta baba yako na Wasii wake sala za Mwenyezi Mungu ziwe juu yao. Na mimi nakuomba ikiwa kweli nimekusadikisha basi unikutanishe na usadiki wangu kwao ili nafsi yangu ifurahi, hivyo shuhudilia kwamba hakika mimi ni msafi kupitia mapenzi yako na mapenzi ya aali wa Nabii wako Muhammad sala za Mwenyezi Mungu ziwe juu yao wote.

Amesema al-Majlisiy: Katika ziyara hii nilikuta nyongeza kupitia riwaya nyingine, nayo ni:

اَلسَّلَامُ عَلَیْكَ يَا مُتَّحِنَةً اِمْتَحَنَكَ الَّذِی خَلَقَ قَبْلَ اَنْ
 یَخْلُقَ وَكُنْتَ لَهَا اِمْتَحَنًا بِه صَابِرَةً وَنَحْنُ لَكَ اَوْلِیَاءُ
 مُصَدِّقُونَ وَلِكُلِّ مَا اَتَى بِه اَبُوکِ صَلَّى اللهُ عَلَیْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ وَآتَى
 بِه وَصِیُّهُ عَلَیْهِ السَّلَامُ مُسَلِّمُونَ وَنَحْنُ نَسْأَلُكَ اَللّٰهُمَّ اِذْ كُنَّا
 مُصَدِّقِیْنَ لَهُمْ اَنْ تُلْحِقْنَا بِتَصَدِیْقِنَا بِالذَّرَجَةِ الْعَالِیَةِ لِنبَشِّرَ
 اَنْفُسَنَا بِاَنَّهَا قَدْ طَهَّرْنَا بِوَلَایَتِهِمْ عَلَیْهِمُ السَّلَامُ

“Amani iwe juu yako ewe mtahiniwa! Mwenyezi Mungu aliyekuumba alikutahini kabla hajakuumba, na ulikuwa ni mwenye subira kwa yale aliyokutahini, na sisi ni vipenzi vyako wenye kukusadikisha wewe, na ni wenye kukubali kila alilotuletea baba yako (s.a.w.w.) na kila alilotuletea Wasii wake, na sisi tunakuomba ewe Mwenyezi Mungu ikiwa kweli tumewasadikisha utukutanishe na daraja la juu kupitia usadiki wetu ili tuzipe habari njema nafsi zetu kwamba tumetakasika kupitia mapenzi yetu kwako.”

Ziyara ya Imam Hasan (a.s.) siku ya Jumatatu:

اَلسَّلَامُ عَلَیْكَ يَا بَنَیْ رَسُوْلِ رَبِّ الْعَالَمِیْنَ. اَلسَّلَامُ عَلَیْكَ يَا بَنَیْ
 اَمِیْرِ الْمُؤْمِنِیْنَ اَلسَّلَامُ عَلَیْكَ يَا بَنَیْ فَاطِمَةَ الزُّهْرَاءِ اَلسَّلَامُ

عَلَيْكَ يَا حَبِيبَ اللَّهِ السَّلَامُ عَلَيْكَ يَا صَفْوَةَ اللَّهِ السَّلَامُ عَلَيْكَ يَا
أَمِينَ اللَّهِ السَّلَامُ عَلَيْكَ يَا حُجَّةَ اللَّهِ السَّلَامُ عَلَيْكَ يَا نُورَ اللَّهِ
السَّلَامُ عَلَيْكَ يَا صِرَاطَ اللَّهِ السَّلَامُ عَلَيْكَ يَا بَيَانَ حُكْمِ اللَّهِ

السَّلَامُ عَلَيْكَ يَا نَاصِرَ دِينِ اللَّهِ السَّلَامُ عَلَيْكَ أَيُّهَا السَّيِّدُ الرَّزِيُّ
السَّلَامُ عَلَيْكَ أَيُّهَا الْبُرُّ الْوَفِيُّ السَّلَامُ عَلَيْكَ أَيُّهَا الْغَائِمُ الْأَمِينُ
السَّلَامُ عَلَيْكَ أَيُّهَا الْعَالِمُ بِالتَّأْوِيلِ السَّلَامُ عَلَيْكَ أَيُّهَا الطَّاهِرُ
الرَّزِيُّ السَّلَامُ عَلَيْكَ أَيُّهَا التَّعِيُّ التَّعِيُّ السَّلَامُ عَلَيْكَ أَيُّهَا الْحَقُّ
الْحَقِيقُ السَّلَامُ عَلَيْكَ أَيُّهَا الشَّهِيدُ الصِّدِّيقُ السَّلَامُ عَلَيْكَ يَا
أَبَا مُحَمَّدٍ الْحَسَنَ بْنَ عَلِيٍّ وَرَحْمَةَ اللَّهِ وَبَرَكَاتَهُ

“Amani iwe juu yako ewe mtoto wa Mtume wa Mola
Mlezi wa walimwengu! Amani iwe juu yako ewe mtoto wa
Amirul-Muuminina! Amani iwe juu yako ewe mtoto wa
Fatima Zahra! Amani iwe juu yako ewe hababi wa
Mwenyezi Mungu! Amani iwe juu yako ewe chaguo bora
la Mwenyezi Mungu! Amani iwe juu yako ewe mwaminifu
wa Mwenyezi Mungu! Amani iwe juu yako ewe hoja wa
Mwenyezi Mungu! Amani iwe juu yako ewe nuru ya
Mwenyezi Mungu! Amani iwe juu yako ewe njia ya

Mwenyezi Mungu! Amani iwe juu yako ewe mbainishajiwa hukmu ya Mwenyezi Mungu!

“Amani iwe juu yako ewe mwenye kuinusuru dini ya Mwenyezi Mungu! Amani iwe juu yako ewe bwana mtakasifu! Amani iwe juu yako ewe mwema mtekelezaji! Amani iwe juu yako ewe mwenye kusimamia mwaminifu! Amani iwe juu yako ewe mjuzi wa taawili! Amani iwe juu yako ewe kiongozi uliye mwongozo! Amani iwe juu yako ewe msafi mtakasifu! Amani iwe juu yako ewe mchamungu msafi! Amani iwe juu yako ewe uliye haki kweli! Amani iwe juu yako ewe shahidi msema kweli! Amani iwe juu yako ewe Abu Muhammad Hasan bin Ali na pia rehema za Mwenyezi Mungu na Baraka Zake ziwe juu yako.”

Ziyara ya Imam Husain (a.s.) siku ya Jumatatu:

السَّلَامُ عَلَيْكَ يَا بَنَ رَسُولِ اللَّهِ السَّلَامُ عَلَيْكَ يَا بَنَ أَمِيرِ
الْمُؤْمِنِينَ. السَّلَامُ عَلَيْكَ يَا بَنَ سَيِّدَةِ نِسَاءِ الْعَالَمِينَ أَشْهَدُ
أَنَّكَ أَقْبَتَ الصَّلَاةَ وَآتَيْتَ الزَّكَاةَ وَأَمَرْتَ بِالْمَعْرُوفِ وَنَهَيْتَ
عَنِ الْمُنْكَرِ وَعَبَدْتَ اللَّهَ مُخْلِصًا وَجَاهَدْتَ فِي اللَّهِ حَقَّ جِهَادِهِ
حَتَّى أَتَاكَ الْيَقِينُ فَعَلَيْكَ السَّلَامُ مِنِّي مَا بَقِيَتْ وَبَقِيَ الدَّلِيلُ
وَالنَّهَارُ وَعَلَى آلِ بَيْتِكَ الطَّيِّبِينَ الطَّاهِرِينَ، أَنَا يَا مَوْلَايَ مَوْلَى

لَكَ وَلَا لِي بَيْتِكَ سَلَّمَ لِمَنْ سَأَلَكَمْ وَحَرْبٌ لِمَنْ حَارَبَكُمْ مُؤْمِنٌ
بِسِرِّكُمْ وَجَهْرُكُمْ وَظَاهِرُكُمْ وَبَاطِنُكُمْ لَعَنَ اللَّهُ أَعْدَاءَكُمْ مِنْ
الْأُولَئِينَ وَالْآخِرِينَ وَأَنَا أَبْرَأُ إِلَى اللَّهِ تَعَالَى مِنْهُمْ

يَا مَوْلَايَ يَا أَبَا مُحَمَّدٍ يَا مَوْلَايَ يَا أَبَا عَبْدِ اللَّهِ هَذَا يَوْمُ الْاِثْنَيْنِ
وَهُوَ يَوْمُكُمْ وَبِاسِبِكُمْ وَأَنَا فِيهِ ضَيْفُكُمْ فَأَضِيفَانِي وَأَحْسِنَا
ضِيافَتِي فَنِعْمَ مَنِ اسْتَضَيْفَ بِهِ أَتُّبَا وَأَنَا فِيهِ مِنْ جَوَارِكُمَا
فَأَجِيرَانِي فَإِنَّكُمَا مَأْمُورَانِ بِالضِّيَافَةِ وَالْإِجَارَةِ فَصَلَّى اللَّهُ
عَلَيْكُمْ وَأَلِكُمَا الطَّيِّبِينَ

“Amani iwe juu yako ewe mtoto wa Mtume wa Mwenyezi Mungu! Amani iwe juu yako ewe mtoto wa Amirul-Muuminina! Amani iwe juu yako ewe mtoto wa mbora wa wanawake wote wa ulimwenguni! Nashahidilia kwamba hakika wewe umesimamisha Sala, umetoa Zaka, umeamrisha mema, umekataza maovu, na umemwabudu Mwenyezi Mungu kwa ikhlasi na umepigana katika njia ya Mwenyezi Mungu mpaka kifo kilipokufika, hivyo ikufikie salamu toka kwangu muda wote nitakaokuwa hai na muda wote utakaobaki usiku na mchana, na pia iwafikie watu wa nyumba yako wema watakasifu. Mimi ewe kiongozi wangu ni mwenye mapenzi nawe na watu wa nyumba yako, nina

amani na yule mwenye amani nanyi na ni mwenye kumpiga vita yule mwenye kuwapiga vita, ni mwenye kuamini siri yenu na dhahiri yenu, nje yenu na ndani yenu. Mwenyezi Mungu awalaani maadui zenu kuanzia wale wa mwanzo hadi wale wa mwisho, na mimi nakimbilia kwa Mwenyezi Mungu dhidi yao.

“Ewe kiongozi wangu! Ewe Abu Muhammad! Ewe kiongozi wangu! Ewe Abu Abdillah! Hii ni siku ya Jumatatu nayo ndio siku yenu na ya jina lenu na mimi humu ni mgeni wenu naomba mpokee ugeni wangu na muenzi vilivyo ugeni wangu, kwani ni uzuri ulioje kwa yule atakayepokewa nanyi katika ugeni. Na mimi humu ni jirani yenu hivyo kubalini ujirani wangu kwani hakika nyinyi mmeamrisha kupokea ugeni na kukubali ujirani, Mwenyezi Mungu awasalie nyinyi na aali zenu wema.”

Ziyara ya Imam Zainul-Abidina, Imam Muhammad al-Baqir na Imam Ja’far as-Sadiq (a.s.) siku ya Jumanne:

السَّلَامُ عَلَيْكُمْ يَا خُزَّانَ عِلْمِ اللَّهِ السَّلَامُ عَلَيْكُمْ يَا تَرَاجِمَةَ وَحْيِ
 اللَّهِ السَّلَامُ عَلَيْكُمْ يَا آئِمَّةَ الْهُدَى السَّلَامُ عَلَيْكُمْ يَا أَعْلَامَ الشُّقَى
 السَّلَامُ عَلَيْكُمْ يَا أَوْلَادَ رَسُولِ اللَّهِ أَنَا عَارِفٌ بِحَقِّكُمْ مُسْتَبْصِرٌ
 بِشَأْنِكُمْ مُعَادِلٌ لِأَعْدَائِكُمْ مُوَالٍ لِأَوْلِيَائِكُمْ بِأَبِي أَنْتُمْ وَأُمِّي صَلَوَاتُ
 اللَّهِ عَلَيْكُمْ اللَّهُمَّ إِنِّي أَتَوَالِي آخِرَهُمْ كَمَا تَوَالَيْتُ أَوْلَاهُمْ وَأَبْرَأُ مِنْ

كُلِّ وَلِيَجَةَ دُونَهُمْ وَأَكْفُرُ بِالْحَبِيبِ وَالطَّاغُوتِ وَاللَّاتِ وَالْعُزَّى
صَلَوَاتُ اللَّهِ عَلَيْكُمْ يَا مَوَالِيَّ وَرَحْمَةُ اللَّهِ وَبَرَكَاتُهُ

السَّلَامُ عَلَيْكَ يَا سَيِّدَ الْعَابِدِينَ وَسُلَاةَ الْوَصِيِّينَ السَّلَامُ
عَلَيْكَ يَا بَاقِرَ عِلْمِ النَّبِيِّينَ السَّلَامُ عَلَيْكَ يَا صَادِقًا مُصَدِّقًا فِي
الْقَوْلِ وَالْفِعْلِ يَا مَوَالِيَّ هَذَا يَوْمُكُمْ وَهُوَ يَوْمُ الثَّلَاثَاءِ وَأَنَا فِيهِ
ضَيْفٌ لَكُمْ وَمُسْتَجِيرٌ بِكُمْ فَأَضِيفُونِي وَأَجِيرُونِي بِمَنْزِلَةِ اللَّهِ
عِنْدَكُمْ وَآلِ بَيْتِكُمُ الطَّيِّبِينَ الطَّاهِرِينَ

“Amani iwe juu yenu enyi wahazini wa elimu ya Mwenyezi Mungu! Amani iwe juu yenu enyi wafasiri wa wahyi wa Mwenyezi Mungu! Amani iwe juu yenu enyi Maimamu wa uongofu! Amani iwe juu yenu enyi bendera za uchamungu! Amani iwe juu yenu enyi watoto wa Mtume wa Mwenyezi Mungu! Naapa kwa baba yangu, kwenu na mama yangu kwamba mimi ni mwenye kutambua haki yenu, mwenye kuona hadhi yenu, mwenye uadui na maadui zenu na mwenye mapenzi na vipenzi vyenu ninyi, sala za Mwenyezi Mungu ziwe juu yenu. Ewe Mwenyezi Mungu! Hakika mimi namtawalisha wa mwisho wao kama nilivyomtawalisha wa mwanzo wao, na ninajitenga na kila aliyekwenda kombo nao, na ninayakufuru masanamu, shetani, Lata na Uzza. Sala za

Mwenyezi Mungu ziwe juu yenu enyi viongozi wangu na pia rehema za Mwenyezi Mungu na Baraka Zake.

“Amani iwe juu yako ewe bwana wa wafanya ibada na asili ya mawasii! Amani iwe juu yako ewe mpasuaji wa elimu ya Manabii! Amani iwe juu yako ewe mkweli msadikishaji katika kauli na kitendo! Enyi viongozi wangu! Hii ni siku yenu nayo ni siku ya Jumanne, nami humu ni mgeni wenu na ni mwenye kutaka ujirani wenu basi pokeeni ugeni wangu na niwekeni jirani, kwa haki ya cheo cha Mwenyezi Mungu alichonacho kwenu na kwa watu wa nyumba yenu wema watakasifu.”

Ziyara ya Imam Musa al-Kadhim, Imam Ali Ridha, Imam Muhammad Jawwad na Imam Ali al-Hadi (a.s.) siku ya Jumatano:

السَّلَامُ عَلَيْكُمْ يَا أَوْلِيَاءَ اللَّهِ السَّلَامُ عَلَيْكُمْ يَا حُجَجَ اللَّهِ السَّلَامُ
عَلَيْكُمْ يَا نُورَ اللَّهِ فِي ظُلُمَاتِ الْأَرْضِ السَّلَامُ عَلَيْكُمْ صَلَوَاتُ اللَّهِ
عَلَيْكُمْ وَعَلَى آلِ بَيْتِكُمُ الطَّيِّبِينَ الطَّاهِرِينَ بِأَبِي أَنْتُمْ وَأُمِّي لَقَدْ
عَبَدْتُمْ اللَّهَ مُخْلِصِينَ وَجَاهَدْتُمْ فِي اللَّهِ حَقَّ جِهَادِهِ حَتَّى أَتَاكُمْ
الْيَقِينَ فَلَغَنَ اللَّهُ أَعْدَاءَكُمْ مِنَ الْجِنَّ وَالْإِنْسِ أَجْمَعِينَ وَأَنَا أَكْبَرُ
إِلَى اللَّهِ وَإِلَيْكُمْ مِنْهُمْ،

يَا مَوْلَايَ يَا أَبَا إِبْرَاهِيمَ مُوسَى بَنَ جَعْفَرَ يَا مَوْلَايَ يَا أَبَا الْحَسَنِ
 عَلِيَّ بَنَ مُوسَى يَا مَوْلَايَ يَا أَبَا جَعْفَرَ مُحَمَّدَ بَنَ عَلِيٍّ يَا مَوْلَايَ يَا
 أَبَا الْحَسَنِ عَلِيَّ بَنَ مُحَمَّدٍ أَنَا مَوْلَى لَكُمْ مَوْمِنٌ بِسِرِّكُمْ وَجَهْرِكُمْ
 مُتَضَيِّفٌ بِكُمْ فِي يَوْمِكُمْ هَذَا وَهُوَ يَوْمُ الْأَرْبَعَاءِ وَمُسْتَجِيرٌ بِكُمْ
 فَأَضِيفُونِي وَأَجِيرُونِي بِأَلِ بَيْتِكُمُ الطَّيِّبِينَ الطَّاهِرِينَ

“Amani iwe juu yenu enyi mawalii wa Mwenyezi Mungu!
 Amani iwe juu yenu enyi hoja wa Mwenyezi Mungu!
 Amani iwe juu yenu enyi nuru ya Mwenyezi Mungu katika
 giza la ardhini! Amani iwe juu yenu enyi ambao sala za
 Mwenyezi Mungu ziwe juu yenu na juu ya watu wa
 nyumba yenu wema watakasifu! Kwa haki ya baba yangu,
 yenu na ya mama yangu hakika mmemwabudu Mwenyezi
 Mungu kwa ikhlasi na mmepigana katika njia ya
 Mwenyezi Mungu jihadi ya kweli mpaka yakini
 ilipowafika. Mwenyezi Mungu awalaani maadui zenu wote
 miongoni mwa majini na watu, na mimi nakimbilia kwa
 Mwenyezi Mungu na kwenu dhidi yao.

“Ewe kiongozi wangu! Ewe Abu Ibrahim Musa bin Ja’far!
 Ewe kiongozi wangu! Ewe Abu Hasan Ali bin Musa
 Ridha! Ewe kiongozi wangu! Ewe Abu Ja’far Muhammad
 bin Ali! Ewe kiongozi wangu! Ewe Abu Hasan Ali bin
 Muhammad! Mimi ni mwenye mapenzi nanyi, mwenye
 kuamini siri yenu na dhahiri yenu, mwenye kutaka ugeni
 kwenu katika siku yenu hii nayo ni siku ya Jumatano, na ni
 mwenye kuomba ujirani wenu basi pokeeni ugeni wangu

na niwekeni jirani, kwa haki ya watu wa nyumba yenu wema watakasifu.”

Ziyara ya Imam Hasan al-Askari (a.s.) siku ya Alhamisi:

السَّلَامُ عَلَيْكَ يَا وَلِيَّ اللَّهِ السَّلَامُ عَلَيْكَ يَا حُجَّةَ اللَّهِ وَخَالِصَتَهُ،
السَّلَامُ عَلَيْكَ يَا إِمَامَ الْمُؤْمِنِينَ وَوَارِثَ الْبُرْسَدِينَ وَحُجَّةَ رَبِّ
الْعَالَمِينَ، . صَلَّى اللَّهُ عَلَيْكَ وَعَلَى آلِ بَيْتِكَ الطَّيِّبِينَ
الطَّاهِرِينَ، يَا مَوْلَايَ يَا أَبَا مُحَمَّدٍ الْحَسَنَ بْنَ عَلِيٍّ أَنَا مَوْلَى لَكَ
وَلِإِلِ بَيْتِكَ وَهَذَا يَوْمُكَ وَهُوَ يَوْمُ الْخَبِيسِ وَأَنَا ضَيْفُكَ فِيهِ
وَمُسْتَجِيرُكَ فِيهِ فَأَحْسِنْ ضِيَافَتِي وَاجَارِقْ بِحَقِّ آلِ بَيْتِكَ
الطَّيِّبِينَ الطَّاهِرِينَ

“Amani iwe juu yako ewe Walii wa Mwenyezi Mungu!
Amani iwe juu yako ewe hoja wa Mwenyezi Mungu na
chaguo lake makhsusi! Amani iwe juu yako ewe Imam wa
waumini, mrithi wa Mitume na hoja wa Mola Mlezi wa
walimwengu! Mwenyezi Mungu akusalie wewe na watu
wa nyumba yako wema watakasifu. Ewe kiongozi wangu!
Ewe Abu Muhammad Hasan bin Ali! Mimi ni mwenye
mapenzi nawe na watu wa nyumba yako, na hii ni siku
yako nayo ni siku ya Alhamisi, na mimi ni mgeni wako
humu na ni mwenye kuomba ujirani wako, basi uenzi

vilivyo ugeni wangu na ujirani wangu, kwa haki ya watu wa nyumba yako wema watakasifu.”

Ziyara ya Imamu wa zama hizi (a.s.) siku ya Ijumaa:

Siku ya Ijumaa ni makhsusi kwa ajili ya Hujja mtoto wa Hasan al-Askari, nayo ndio siku atakayodhihiri:

السَّلَامُ عَلَيْكَ يَا حُجَّةَ اللَّهِ فِي أَرْضِهِ، السَّلَامُ عَلَيْكَ يَا عَيْنَ اللَّهِ فِي
خَلْقِهِ، السَّلَامُ عَلَيْكَ يَا نُورَ اللَّهِ الَّذِي يَهْتَدِي بِهِ الْمُهْتَدُونَ
وَيُفَرِّجُ بِهِ عَنِ الْمُؤْمِنِينَ، السَّلَامُ عَلَيْكَ أَيُّهَا الْمُهْتَدِبُ
الْخَائِفُ، السَّلَامُ عَلَيْكَ أَيُّهَا الْوَلِيُّ النَّاصِحُ، السَّلَامُ عَلَيْكَ يَا
سَفِينَةَ النَّجَاةِ، السَّلَامُ عَلَيْكَ يَا عَيْنَ الْحَيَاةِ، السَّلَامُ عَلَيْكَ
صَلَّى اللَّهُ عَلَيْكَ وَعَلَى آلِ بَيْتِكَ الطَّيِّبِينَ الطَّاهِرِينَ، السَّلَامُ
عَلَيْكَ عَجَلِ اللَّهِ لَكَ مَا وَعَدَكَ مِنَ النَّصْرِ وَظُهُورِ الْأُمْرِ،

السَّلَامُ عَلَيْكَ يَا مَوْلَايَ أَنَا مَوْلَاكَ عَارِفٌ بِأَوْلَاكَ وَأُخْرَاكَ،
اتَّقَرَّبُ إِلَى اللَّهِ تَعَالَى بِكَ وَبِآلِ بَيْتِكَ، وَأَتَنْتَظِرُ ظُهُورَكَ وَظُهُورَ

الْحَقِّ عَلَى يَدَيْكَ وَأَسْأَلُ اللَّهَ أَنْ يُصَلِّيَ عَلَيَّ مُحَمَّدًا وَعَلَى آلِ مُحَمَّدٍ
وَأَنْ يَجْعَلَ لِي مِنَ الْمُتَتَابِعِينَ لَكَ وَالتَّابِعِينَ وَالتَّابِعِينَ لَكَ
عَلَى أَعْدَائِكَ وَالْمُسْتَشْهَدِينَ بَيْنَ يَدَيْكَ فِي جُمْلَةِ أَوْلِيَائِكَ،

يَا مَوْلَايَ يَا صَاحِبَ الزَّمَانِ صَلَوَاتُ اللَّهِ عَلَيْكَ وَعَلَى آلِ بَيْتِكَ
هَذَا يَوْمَ الْجُمُعَةِ وَهُوَ يَوْمُكَ الْمَتَوَقَّعُ فِيهِ ظُهُورُكَ وَالْفَرَجُ فِيهِ
لِلْمُؤْمِنِينَ عَلَى يَدَيْكَ وَقَتْلُ الْكَافِرِينَ بِسَيْفِكَ وَأَنَا يَا مَوْلَايَ
فِيهِ صَيْفُكَ وَجَارُكَ وَأَنْتَ يَا مَوْلَايَ كَرِيمٌ مِنْ أَوْلَادِ الْكِرَامِ
وَمَأْمُورٌ بِالضِّيَافَةِ وَالْإِجَارَةِ فَأَضِغْنِي وَأَجِرْنِي صَلَوَاتُ اللَّهِ
عَلَيْكَ وَعَلَى أَهْلِ بَيْتِكَ الطَّاهِرِينَ

“Amani iwe juu yako ewe Hoja wa Mwenyezi Mungu katika ardhi Yake! Amani iwe juu yako ewe jicho la Mwenyezi Mungu kwa viumbe Wake! Amani iwe juu yako ewe nuru ya Mwenyezi Mungu ambayo kwayo wenye kutaka kuongoka huongoka na kwayo waumini hufarijika! Amani iwe juu yako ewe uliyefunzwa maadili mema na uliye na hofu! Amani iwe juu yako ewe kiongozi mnasihi! Amani iwe juu yako ewe safina ya uokovu! Amani iwe juu yako ewe chemchemu ya uhai! Amani iwe juu yako ewe ambaye Mwenyezi Mungu hukusalie wewe na watu wa

nyumba yako wema watakasifu! Amani iwe juu yako ewe ambaye Mwenyezi Mungu akuharakishie yale aliyokuahidi ambayo ni ushindi na kudhihiri jambo!

“Amani iwe juu yako ewe kiongozi wangu! Mimi ni mwenye kukutawalisha wewe na mwenye kutambua mwanzo wako na mwisho wako, najikurubisha kwa Mwenyezi Mungu kupitia kwako na watu wa nyumba yako, na ninangojea kudhihiri kwako na kudhihiri kwa haki mikononi mwako, na ninamuomba Mwenyezi Mungu amsalie Muhammad na aali Muhammad na anijaalie niwe miongoni mwa wenye kukungojea wewe, wenye kukufuata, wenye kukusaidia wewe dhidi ya maadui zako, na wenye kufa kishahidi mikononi mwako katika kundi la hao.

“Ewe kiongozi wangu! Ewe mhusika wa zama hizi, sala za Mwenyezi Mungu ziwe juu yako na juu ya watu wa nyumba yako, hii ni siku ya Ijumaa nayo ndio siku yako unayotarajiwa kudhihiri humo na waumini kupata faraja mikononi mwako na kuwauwa makafiri kwa upanga wako, na mimi humu ewe kiongozi wangu ni mgeni wako na jirani yako, na wewe ewe kiongozi wangu ni mkarimu mtoto wa wakarimu na ni mwenye kuamrisha kupokea ugeni na ujirani hivyo poka ugeni wangu na niweke jirani, sala za Mwenyezi Mungu ziwe juu yako na juu ya watu wa nyumba yako watakasifu.”

Namna ya kuwazuru Maasumina kumi na nne (a.s.) kwa mbali:

Sayyid Ibnu Tawuusi amesema katika kitabu *al-Iqbali*: Tambua kwamba hakika mimi nimekuta katika riwaya mbalimbali kutoka kwa waaminifu kwamba kila siku miongoni mwa siku za juma yupo anayekinga hatari zake

na anamkaribisha mwanadamu humo katika meza ya mema yake. Jumamosi ni siku ya Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.). Jumapili ni ya maulana Ali (a.s.). Jumatatu ni ya Hasan na Husain (a.s.). Jumanne ni ya Ali bin Husain na Muhammad al-Baqir na Ja'far as-Sadiq (a.s.). Jumatano ni ya Musa al-Kadhim, Ali Ridha, Muhammad Jawwad na Ali al-Hadi (a.s.). Alhamisi ni ya Hasan al-Askari (a.s.). Na Ijumaa ni ya al-Mahdi (a.s.).

Imepokewa kutoka kwa as-Sadiq Ja'far bin Muhammad (a.s.) kwamba alisema: “Atakayetaka kulizuru kaburi la Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.), kaburi la Amirul-Muuminina, Fatima, Hasan, Husein na kaburi la hoja wa Mwenyezi Mungu (a.s.) na hali akiwa nchini kwake basi akoge siku ya Ijumaa na avae nguo mbili safi na aende kwenye ardhi isiyoyana mimea kisha asali rakaa nne, asome katika rakaa hizo chochote awezacho miongoni mwa Qur'an, atakapotoa tashahudi na salamu asimame akiwa ameelekea Kibla na aseme:

السَّلَامُ عَلَيْكَ أَيُّهَا النَّبِيُّ وَرَحْمَةُ اللَّهِ وَبَرَكَاتُهُ، السَّلَامُ عَلَيْكَ
 أَيُّهَا النَّبِيُّ الْمُرْسَلُ، وَالْوَصِيُّ الْمُرْتَضَى، وَالسَّيِّدَةُ الْكُبْرَى،
 وَالسَّيِّدَةُ الزَّهْرَاءُ، وَالسَّبْطَانِ الْمُنْتَجَبَانِ، وَالْأَوْلَادُ الْأَعْلَامُ،
 وَالْأَمْنَاءُ الْمُنْتَجَبُونَ، جِئْتُ انْقِطَاعاً إِلَيْكُمْ وَإِلَى آبَائِكُمْ وَوَلَدِكُمْ
 الْخَلْفِ، عَلَى بَرَكَةِ الْحَقِّ، فَقَلْبِي لَكُمْ مُسَلِّمٌ وَنُصْرَتِي لَكُمْ

مُعَدَّةً، حَتَّى يَحْكُمَ اللَّهُ بِدِينِهِ، فَبِعَظْمِ مَعَكُمْ لَمْ يَمَعَّ عَدُوَّكُمْ، إِنِّي
 لِبَنِ الْقَائِلِينَ بِفَضْلِكُمْ، مُقَرَّرٌ بِرَجْعَتِكُمْ، لَا أُكْرَهُ لِلَّهِ قُدْرَةً وَلَا
 أَرْعَمُ إِلَّا مَا شَاءَ اللَّهُ سُبْحَانَ اللَّهِ ذِي الْبُلْكِ وَالْبَلْكَوتِ، يُسَبِّحُ
 اللَّهَ بِأَسْمَائِهِ جَمِيعُ خَلْقِهِ، وَالسَّلَامُ عَلَى أَرْوَاحِكُمْ وَأَجْسَادِكُمْ،
 وَالسَّلَامُ عَلَيْكُمْ وَرَحْمَةُ اللَّهِ وَبَرَكَاتُهُ

“Amani iwe juu yako ewe Nabii na pia rehema za Mwenyezi Mungu na Baraka Zake! Amani iwe juu yako ewe Nabii uliyetumwa, na ewe Wasii uliyeridhiwa, na ewe bi Khadija na ewe Bi Zahara, na enyi wajukuu wawili wateule, na enyi watoto wajuzi, waaminifu na wateule, nimekuja na hali ni mwenye kujielekeza kwenu, kwa baba zenu na kwa mtoto wenu aliyeachwa kwa ajili ya Baraka za viumbe. Moyo wangu ni wenye kusalimishwa kwenu na usaidizi wangu kwenu ni wenye kuandaliwa, mpaka Mwenyezi Mungu ahukumu mbele yake, nipo pamoja nanyi, nipo pamoja nanyi na si pamoja na maadui zenu, hakika mimi ni miongoni mwa wenye kutamka ubora wenu na ni mwenye kukiri kurejea kwenu, sikanushi kwa Mwenyezi Mungu uwezo wowote na wala sidai ila yale ayatakayo Mwenyezi Mungu, ametakasika Mwenyezi Mungu na kila sifa njema ni ya Mwenyezi Mungu mwenye umiliki na ufalme, viumbe Vyake vyote humsabihi Yeye Mwenyezi Mungu kupitia majina Yake. Na amani iwe juu ya roho zenu na miili yenu! Amani iwe juu yenu na pia rehema za Mwenyezi Mungu na Baraka Zake.”

Na katika riwaya nyingine: Fanya hayo ukiwa juu ya paa ya nyumba yako.

Dua baada ya ziara:

Sayyid Ibnu Tawuus amesema: “Ni Sunna kuomba dua hii baada ya ziara hizo za Maimamu (a.s.) huko kwenye makaburi yao matukufu:

اللَّهُمَّ إِنْ كَانَتْ ذُنُوبِي قَدْ أَخْلَقْتُ وَجْهِي عِنْدَكَ وَحَجَبْتَ دُعَائِي
عَنْكَ وَحَالَتْ بَيْنِي وَبَيْنَكَ فَأَسْأَلُكَ أَنْ تُقْبَلَ عَلَيَّ بِوَجْهِكَ
الْكَرِيمِ وَتَنْشُرَ عَلَيَّ رَحْمَتَكَ وَتُنزِلَ عَلَيَّ بَرَكَاتِكَ وَإِنْ كَانَتْ قَدْ
مَنَعَتْ أَنْ تَرْفَعَنِي إِلَيْكَ صَوْتاً أَوْ تَغْفِرَ لِي ذَنْباً أَوْ تَتَجَاوَزَ عَنِّي
خَطِيئَةَ مُهْلِكَةٍ فَهَا أَنَا إِذَا مُسْتَجِيبٌ بِكَرَمِ وَجْهِكَ وَعِزِّ جَلَالِكَ
مُتَوَسِّلٌ إِلَيْكَ مُتَقَرِّبٌ إِلَيْكَ بِأَحَبِّ خَلْقِكَ إِلَيْكَ وَأَكْرَمِهِمْ
عَلَيْكَ وَأَوْلَاهُمْ بِكَ وَأَطْوَعِهِمْ لَكَ وَأَعْظَمِهِمْ مَنزِلَةً وَمَكَاناً
عِنْدَكَ مُحَمَّدٍ وَبِعْتَرْتِهِ الطَّاهِرِينَ الْأَيْتَةَ الْهُدَاةَ الْمُهْدِيَيْنِ
الَّذِينَ فَرَضْتَ عَلَى خَلْقِكَ طَاعَتَهُمْ وَأَمَرْتَ بِسُودَتِهِمْ وَجَعَلْتَهُمْ
وُلَاةَ الْأُمُورِ مِنْ بَعْدِ رَسُولِكَ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ يَا مُدِلَّ كُلِّ

جَبَّارٍ عَنِيدٍ يَا مُعِزُّ الْمُؤْمِنِينَ بَدَّخْ مَجْهُودِي فَهَبْ لِي نَفْسِي
السَّاعَةَ وَرَحْمَةً مِنْكَ تَبْنِي بِهَا عَلَيَّ يَا أَرْحَمَ الرَّاحِمِينَ

“Ewe Mwenyezi Mungu! Ikiwa dhambi zangu zimeuchakaza uso wangu Kwako, na zimezuia maombi yangu Kwako, na zimeweka kizuizi kati yangu na Wewe, basi nakuomba unielekee kwa heshima Yako tukufu na ueneze juu yangu rehema Zako na unishushie Baraka Zako. Na kama zimezuia sauti yangu isifike Kwako, au usinighufirie dhambi zangu au kunisamehe makosa yangu yenye kuangamiza, basi ni mimi hapa nakuomba ujirani kupitia heshima ya utukufu Wako na nguvu za utukufu Wako, ni mwenye kutawassali Kwako na kujikurubisha Kwako kupitia kiumbe ukipendacho mno kushinda vingine, kitukufu mno Kwako kushinda vingine, kilicho bora mno Kwako kushinda vingine, chenye utii Kwako kushinda vingine, na chenye cheo na nafasi tukufu mno Kwako kushinda vingine, Muhammad (s.a.w.w.), na kupitia kizazi chake kitakasifu Maimamu wa uongofu walio mwongozo, ambao umewawajibisha viumbe Wako kuwatii wao, ukaamuru kuwapenda wao na ukawafanya viongozi wa jambo (Uislamu) baada ya Mtume Wako (s.a.w.w.). Ewe mwenye kumdhalilisha kila jabari mkaidi! Na ewe mwenye kuwapa heshima waumini! Juhudi zangu zimekomea hapa hivyo ipe nafsi yangu wasaa na rehema kutoka Kwako ambayo itakuwa ni neema kwangu, ewe Mwenye kurehemu kushinda wote wenye kureheme.

Kisha sema:

اللهم إن هذا مشهد لا يرجو من فاتته فيه رحمتك ، أن ينالها
 في غيره ، وَلَا أَحَدٌ أَشَقَى مِنْ أَمْرِ قَصْدَكَ مُؤَمَّلًا فَابَ عَنْهُ خَائِبًا
 اللَّهُمَّ إِنِّي أَعُوذُ بِكَ مِنْ شَرِّ الْإِيَابِ وَخَيْبَةِ الْبُنْتَلَبِ وَالْمُنَاقَشَةِ
 عِنْدَ الْحِسَابِ وَحَاشَاكَ يَا رَبِّ أَنْ تَقْرَنَ طَاعَةَ وَبَيْتِكَ بِطَاعَتِكَ
 وَمُؤَالَاتِهِ بِمُؤَالَاتِكَ وَمَعْصِيَتَهُ بِمَعْصِيَتِكَ ثُمَّ تُوَيْسَ زَائِرُهُ
 وَالْمُتَحَبِّلَ مِنْ بَعْدِ الْبِلَادِ إِلَى قَبْرِهِ وَعِزَّتِكَ يَا رَبِّ لَا يَنْعَقِدُ عَلَى
 ذَلِكَ ضَبِيرِي إِذْ كَانَتْ الْقُلُوبُ إِلَيْكَ بِالْجَبِيلِ تَشِيرُ

“Ewe Mwenyezi Mungu! Hakika hili ni kaburi ambalo yule atakayepitwa na rehema Zako hapa hataraji kuzipata kwingine, na wala hakuna yeyote aliye muovu kushinda mtu mwenye kulikusudia huku akiwa ni mwenye matarajio kisha arudi mikono mitupu. Ewe Mwenyezi Mungu! Hakika mimi najikinga Kwako dhidi ya shari za safari ya kurudi, kufeli wakati wa mgeuko, na mahojiano wakati wa hesabu. Uko mbali ewe Mola Mlezi na kitendo cha kuambatanisha utii wa Walii Wako na utii Wako, uongozi wake na uongozi Wako, uasi dhidi yake na uasi dhidi Yako, kisha umkatishe tamaa mwenye kumzuru na mwenye kujifungasha toka mji wa mbali mpaka kwenye kaburi lake. Naapa kwa utukufu Wako ewe Mola Mlezi dhamira yangu haiamini hilo kwani nyoyo zinaashiria mazuri Kwako.”

Sheikh Mufid naye kaitaja dua hii, lakini yeye kaongeza kipande hiki:

يَا وَلِيَّ اللَّهِ إِنَّ بَيْنِي وَبَيْنَ اللَّهِ عَزَّوَجَلَّ ذُنُوبًا لَا يَأْتِي عَلَيْهَا إِلَّا
رِضَاكَ، فَبِحَقِّ مَنْ ائْتَمَنَكَ عَلَى سِرِّهِ، وَاسْتَرْعَاكَ أَمْرَ خَلْقِهِ،
وَقَرَنَ طَاعَتَكَ بِطَاعَتِهِ، وَمُؤَالَاتِكَ بِمُؤَالَاتِهِ، تَوَلَّ صَلَاحَ حَالِي
مَعَ اللَّهِ عَزَّوَجَلَّ، وَاجْعَلْ حَظِّي مِنْ زِيَارَتِكَ تَخْلِيطِي بِخَالِصِي
رُؤَاكِ الَّذِينَ تَسْأَلُ اللَّهُ عَزَّوَجَلَّ فِي عِتْقِ رِقَابِهِمْ، وَتَرْغَبُ إِلَيْهِ
فِي حُسْنِ ثَوَابِهِمْ، وَهَا أَنَا الْيَوْمَ بِقَبْرِكَ لِائْتِدٍ، وَبِحُسْنِ دِفَاعِكَ
عَنِّي عَائِدٍ، فَتَلَفَنِي يَا مَوْلَايَ وَأَدْرِكْنِي وَأَسْأَلُ اللَّهَ عَزَّوَجَلَّ فِي
أَمْرِي، فَإِنَّ لَكَ عِنْدَ اللَّهِ مَقَامًا كَرِيمًا وَجَاهًا عَظِيمًا صَلَّى اللَّهُ
عَلَيْكَ وَسَلَّمَ تَسْلِيمًا

“Ewe Walii wa Mwenyezi Mungu! Hakika baina yangu na Mwenyezi Mungu Mtukufu kuna dhambi hakuna wa kuzifunika ila ridhaa Yako, hivyo kwa haki ya Yule aliyekuamini kwa kukupa siri Yake, akakupa jukumu la kuwachunga viumbe Wake, akaambatanisha utii wako na utii Wake na uongozi wako na uongozi Wake, simamia ubadilishaji wa hali yangu pamoja na Mwenyezi Mungu Mtukufu, na fanya fungu langu toka katika kukuzuru wewe

liwe ni kunichanga mimi na wale wenye kukuzuru wewe kwa ikhlasi, ambao unamuomba Mwenyezi Mungu aziache huru shingo zao (dhidi ya moto) na unawaombea Kwake malipo mema. Na mimi ni huyu hapa leo hii nakimbilia kwenye kaburi lako na ninajikinga kwa utetezi wako mwema, hivyo nilaki ewe kiongozi wangu na nidiriki, na muombe Mwenyezi Mungu Mtukufu kuhusu jambo langu kwani hakika una cheo kitukufu kwa Mwenyezi Mungu na heshima adhimu. Sala na salamu za Mwenyezi Mungu ziwe juu yako.”

Dua ya kumwomba Hujjah (a.s.):

Ni bora kwa mwenye kufanya ziara akitaka kuomba kwenye kaburi lolote miongoni mwa makaburi matukufu, bali ni bora kwa mwenye kuomba popote atakapokuwa na kwa haja yoyote ile aanze kwa kuomba dua ya kumuomba afya njema al-Hujjah Imam wa Zama hizi, maamkizi mema na salamu viwe juu yake na juu ya baba zake. Na hili ni jambo muhimu sana na ni lenye faida nyingi. Na muhtasari wake ni aseme:

اَللّٰهُمَّ كُنْ لِيْوَلِيَّكَ الْحُجَّةِ بْنِ الْحَسَنِ، صَلَوَاتِكَ عَلَيْهِ وَعَلَى
اَبَائِهِ، فِيْ هَذِهِ السَّاعَةِ وَفِيْ كُلِّ سَاعَةٍ، وَلِيًّا وَحَافِظًا وَقَائِدًا
وَناَصِرًا وَدَلِيْلًا وَعَيْنًا، حَتَّى تُسَكِّنَهُ اَرْضَكَ طَوْعًا، وَتُبَتِّعَهُ فِيْهَا
طَوِيْلًا

“Ewe Mwenyezi Mungu! Kuwa msimamizi, muhifadhi, kiongozi, msaidizi, dalili (mwelekezi) na mlinzi kwa walii

Wako Hujjah mtoto wa al-Hasan sala Zako ziwe juu yake na juu ya baba zake katika saa hii na katika kila saa, mpaka umpe makazi ardhini Kwako kwa utiifu, na umstareheshe humo muda mrefu.”

Sala ya Ja’far Tayyar:

Imepokewa kwamba atakayemzuru Imam Ridha (a.s.) au mmoja kati ya Maimamu (a.s.) na akasali hapo Sala ya Ja’far Tayyar (a.s.) basi ataandikiwa kwa kila rakaa moja malipo ya mtu aliyehiji Hijja elfu moja na aliyekwenda Umra mara elfu moja, akawapa uhuru katika njia ya Mwenyezi Mungu watumwa elfu moja, na akasimama kidete katika Jihadi mara elfu moja safu moja na Nabii aliyetumwa. Na atapata kwa kila hatua aliyopiga malipo ya Hijja elfu moja, Umra elfu moja na kuwapa uhuru katika njia ya Mwenyezi Mungu watumwa elfu moja. Na ataandikiwa mema mia moja na atafutiwa madhambi mia moja.

Kuna riwaya imepatikana inayozungumzia fadhila adhimu ilizonayo Sala ya Ja’far Tayyar (a.s.) kwa njia bora kabisa. Na fadhila muhimu iliyonayo ni kufutiwa dhambi kubwa. Na wakati wake bora ni mwanzoni mwa mchana wa siku ya Ijumaa. Nayo ni rakaa nne kwa Tashahudi mbili na Salamu mbili, katika kila rakaa baada ya Alhamdu na Sura nyingine na kabla ya rukuu atasoma mara kumi na tano:

«سُبْحَانَ اللَّهِ وَالْحَمْدُ لِلَّهِ وَلَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ وَاللَّهُ أَكْبَرُ»

“Mwenyezi Mungu ametakasika. Na kila sifa njema ni ya Mwenyezi Mungu. Na hapana mungu ila Allah. Na Mwenyezi Mungu ni mkubwa mno.”

Na atasema hayo mara kumi katika rukuu yake baada ya dhikri. Na atakaponyooka toka katika rukuu akiwa amesimama atasema hayo mara kumi. Atakaposujudu atayasema mara kumi. Atakapokaa baina ya sijda mbili atayasema mara kumi. Atakaposujudu sijda ya pili atayasema mara kumi. Atakapokaa kupumzika ili asimame atayasema mara kumi kabla hajasimama. Atafanya hivyo katika rakaa zote nne, hivyo jumla ya idadi yake itakuwa ni tasbihi mia tatu. Si sharti katika Sala hiyo Sura makhsusi, lakini bora ni asome katika rakaa ya kwanza baada ya Alhamdu Sura Zilzala, katika rakaa ya pili baada ya Alhamdu Sura Al'adiyati, katika rakaa ya tatu Sura Nasru, na katika rakaa ya nne Sura Ikhlas.

Kama ambavyo ni Sunna baada ya kumaliza Tasbihati katika sijda ya pili katika rakaa ya nne asome:

سُبْحَانَ مَنْ لَبِسَ الْعِزَّ وَالْوَقَارَ، سُبْحَانَ مَنْ تَعَطَّفَ بِالْبَجْدِ
 وَتَكَرَّمَ بِهِ، سُبْحَانَ مَنْ لَا يَنْبَغِي التَّسْبِيحُ إِلَّا لَهُ، سُبْحَانَ مَنْ
 أَحْصَى كُلَّ شَيْءٍ عَلَيْهِ، سُبْحَانَ ذِي الْبَنِّ وَالنِّعَمِ، سُبْحَانَ
 ذِي الْقُدْرَةِ وَالْكَرَمِ. اللَّهُمَّ إِنِّي أَسْأَلُكَ بِعَاقِدِ الْعِزِّ مِنْ
 عَرْشِكَ، وَمُنْتَهَى الرَّحْمَةِ مِنْ كِتَابِكَ، وَأَسْأَلُكَ الْأَعْظَمِ،
 وَكَلِمَاتِكَ الثَّامَّةِ الَّتِي تَبَّتْ صِدْقًا وَعَدْلًا، صَلِّ عَلَى مُحَمَّدٍ
 وَأَهْلِ بَيْتِهِ وَافْعَلْ بِي كَذَا وَكَذَا

“Ametakasika Ambaye amevaa utukufu na heshima! Ametakasika Ambaye amejifunika utukufu na amepata heshima kwao! Ametakasika Ambaye haipasi kufanya Tasbihi ila kwa ajili Yake! Ametakasika Ambaye elimu yake imekihisabu kila kitu! Ametakasika mwenye ihsani na neema! Ametakasika mwenye uwezo na heshima! Ewe Mwenyezi Mungu! Ewe Mwenyezi Mungu! Hakika mimi nakuomba kupitia vifungo vya utukufu toka katika Arshi Yako na kilele cha rehema toka katika Kitabu Chako, jina Lako adhimu mno na maneno Yako timilifu ambayo yametimia kwa ukweli na uadilifu, umsalie Muhammad na watu wa nyumba yake na unifanyie mimi kadha wa kadha.” (Utaomba haja yako badala ya maneno kadha wa kadha.)”

Ni Sunna kwamba baada ya kumaliza Sala baada ya rakaa ya nne ainue mikono yake na aseme:

يَا رَبِّ يَا رَبِّ

يَا رَبَّاهُ يَا رَبَّاهُ

يَا اللَّهُ يَا اللَّهُ

يَا حَيُّ يَا حَيُّ

يَا رَحِيمُ يَا رَحِيمُ

يَا رَحْمَانُ يَا رَحْمَانُ

يَا أَرْحَمَ الرَّاحِمِينَ يَا أَرْحَمَ الرَّاحِمِينَ

“Ewe Mola Mlezi! Ewe Mola Mlezi!” mpaka hapa pumzi iishe.

“Ewe Mola wangu Mlezi! Ewe Mola wangu Mlezi!” mpaka hapa pumzi iishe

“Ewe Allah! Ewe Allah!” mpaka hapa pumzi iishe.

“Ewe Uliye hai! Ewe Uliye hai!” mpaka hapa pumzi iishe.

“Ewe Rahimu! Ewe Rahimu!” mpaka hapa pumzi iishe.

“Ewe Rahmani! Ewe Rahmani!” mara saba.

“Ewe Mwenye kurehemu kushinda wote wenye kurehemu!
Ewe Mwenye kurehemu kushinda wote wenye kurehemu!”
mara saba.

Kisha aseme:

اللَّهُمَّ إِنِّي أَفْتَتِحُ الْقَوْلَ بِحَمْدِكَ، وَأَنْطِقُ بِالشَّيْءِ عَلَيْكَ،
وَأُمَجِّدُكَ وَلَا غَايَةَ لِدَحِّكَ، وَأُثْنِي عَلَيْكَ، وَمَنْ يَبْدُغْ غَايَةَ
شَائِكَ، وَأَمَدَ مَجْدِكَ وَأَنِّي لَخَلِيقَتِكَ كُنْتُ مَعْرِفَةَ مَجْدِكَ وَأَمِّي

زَمَنْ لَمْ تَكُنْ مَبْدُوحاً بِفَضْلِكَ، مَوْصُوفاً بِسَجْدِكَ، عَوَاداً عَلَى
 الْهُدُنِيِّينَ بِحِلْبِكَ تَخَلَّفَ سُكَّانُ أَرْضِكَ عَنْ طَاعَتِكَ، فَكُنْتَ
 عَلَيْهِمْ عَطُوفاً بِجُودِكَ، جَوَاداً بِفَضْلِكَ، عَوَاداً بِكَرَمِكَ، يَا إِلَهَ
 إِلَّا أَنْتَ الْبَنَّانُ ذُو الْجَلَالِ وَالْإِكْرَامِ

“Ewe Mwenyezi Mungu! Hakika mimi ninaanza kauli kwa kukuhimidi Wewe, ninatamka kwa kukusifu Wewe, na ninakutukuza Wewe na hali hakuna kikomo cha sifa Zako, na ninakusifu na ni nani anayefikia kikomo cha sifa Zako na umbali wa utukufu Wako. Na umewafikia viumbe Wako wakati wa kuzijua sifa Zako, na ni wakati upi haukuwa msifiwa kwa fadhila Zako, Mtukuzwa kwa sifa Zako na mwenye kuwarudia wenye dhambi kwa uvumilivu Wako. Wakazi wa ardhi Yako wamejitenga na utii Wako lakini umekuwa mpole kwao kwa ukarimu Wako, Mkarimu kwa fadhila Zako na mwenye kuwarudia kwa ukarimu Wako, ewe Ambaye hapana mungu ila Wewe, Mpaji Mwenye utukufu na ukarimu.”

FASLU YA YA SITA

KUMZURU BWANA WETU HAMZA

Utasema katika kumzuru Hamza Bwana wa wahanga (r.a.):

اَسْلَامُ عَلَيْكَ يَا عَمَّ رَسُوْلِ اللهِ صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ، اَسْلَامُ
عَلَيْكَ يَا خَيْرَ الشُّهَدَاءِ، اَسْلَامُ عَلَيْكَ يَا اَسَدَ اللهِ وَاسَدَ
رَسُوْلِهِ، اَشْهَدُ اَنَّكَ قَدْ جَاهَدْتَ فِي اللهِ عَزَّوَجَلَّ، وَجَدْتَ
بِنَفْسِكَ، وَنَصَحْتَ رَسُوْلَ اللهِ صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ، وَكُنْتَ
فِي سَاعِدَةِ اللهِ سُبْحَانَهُ رَاغِبًا، بَابِي اَنْتَ وَاُمِّي اَتَيْتِكَ مُتَقَرِّبًا اِلَى
اللهِ بِزِيَارَتِكَ وَ مُتَقَرِّبًا اِلَى رَسُوْلِ اللهِ صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ
بِذَلِكَ رَاغِبًا اِلَيْكَ فِي الشَّفَاعَةِ، اَبْتَغِي بِزِيَارَتِكَ خَلَاصَ نَفْسِي،
مُتَعَوِّذًا بِكَ مِنْ نَارِ اسْتَحَقَّهَا مِثْلِي بِهَا جَنَيْتُ عَلَى نَفْسِي،
هَارِبًا مِنْ ذُنُوْبِي الَّتِي احْتَطَبْتُهَا عَلَى ظَهْرِي، فَزِعًا اِلَيْكَ رَجَاءً
رَحْمَةً رَبِّي،

أَتَيْتُكَ مِنْ شُقَّةٍ بَعِيدَةٍ طَالِباً فَكَأَنَّكَ رَقَبْتِي مِنَ النَّارِ، وَقَدْ
 أَوْفَرْتُ ظَهْرِي ذُنُوبٍ، وَأَتَيْتُ مَا أَسْخَطَ رَبِّي، وَلَمْ أَجِدْ أَحَدًا أَفْزَعُ
 إِلَيْهِ خَيْرًا لِي مِنْكُمْ أَهْلَ بَيْتِ الرَّحْمَةِ، فَكُنْ لِي شَفِيعاً يَوْمَ فَقْرِي
 وَحَاجَتِي، فَقَدْ سَرْتُ إِلَيْكَ مَحْزُونًا، وَأَتَيْتُكَ مَكْرُوبًا، وَسَكَبْتُ
 عَبْرَتِي عِنْدَكَ بَاكِيًا، وَصَرْتُ إِلَيْكَ مُفْرَدًا، وَأَنْتَ مَسْنُ أَمْرِي اللَّهُ
 بِصَلَّتِهِ، وَحَثَّنِي عَلَى بِرِّهِ، وَدَلَّنِي عَلَى فَضْلِهِ، وَهَدَانِي لِحُبِّهِ،
 وَرَعَّبَنِي فِي الْوِفَادَةِ إِلَيْهِ، وَالْهَمَّنِي طَلَبَ الْحَوَائِجِ عِنْدَكَ، أَنْتُمْ
 أَهْلُ بَيْتٍ لَا يَشْتَقِي مَنْ تَوَلَّاهُمْ، وَلَا يَخِيبُ مَنْ آتَاهُمْ، وَلَا يَخْسِرُ
 مَنْ يَهْوَاهُمْ وَلَا يَسْعَدُ مَنْ عَادَاهُمْ

“Amani iwe juu yako ewe ami yake Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.)! Amani iwe juu yako ewe mbora wa mashahidi! Amani iwe juu yako ewe simba wa Mwenyezi Mungu na simba wa Mtume Wake! Nashahidilia kwamba hakika wewe ulipigana jihadi katika njia ya Mwenyezi Mungu Mtukufu na ulijituma, ulimshauri Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) na ulikuwa ni mwenye hamu na yale yaliyopo kwa Mwenyezi Mungu, kwa haki ya baba yangu, yako na ya mama yangu, nimekujia na hali ni mwenye kujikurubisha kwa Mwenyezi Mungu kwa kukuzuru wewe, na ni mwenye kujikurubisha kwa Mtume

wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) kwa kufanya hivyo, ni mwenye hamu ya kupata uombezi wako, natafuta kupitia ziara yangu kwako uokovu wa nafsi yangu, ni mwenye kujikinga kupitia kwako na moto anaostahili mtu mfano wangu kutokana na makosa niliyoitendea nafsi yangu, ni mwenye kuyakimbia madhambi yangu ambayo nimeyageuza kuni juu ya mgongo wangu, ni mwenye kukimbilia Kwako nikitaraji rehema za Mola Wangu Mlezi.

“Nimekuja kwako toka sehemu ya mbali nikiwa ni mwenye kutafuta kukombolewa na wewe dhidi ya moto, na bila shaka dhambi zimeuelemea mgongo wangu na nimetenda yanayomchukiza Mola wangu Mlezi, na sijapata yeyote wa kumkimbilia aliye kheri kwangu kushinda nyinyi watu wa nyumba ya rehema, hivyo kuwa mwombezi wangu siku ya ufakiri wangu na haja yangu, nimetembea kuja kwako nikiwa ni mwenye kuhuzunishwa, na nimekuja nikiwa ni mwenye kutatizwa, nimemwaga machozi yangu kwako hali ni mwenye kulia na nimekuwa kwako mpweke, na wewe ni miongoni mwa yule ambaye Mwenyezi Mungu aliniamuru na akanihimiza kumtendea wema, na akanionyesha fadhila zake na akaniongoza kumpenda, akanipa shauku ya kumfungia safari na akanipa ilhamu ya kuomba haja kwake. Enyi watu wa nyumba ya Mtume! Hahangaiki yule mwenye kuwatawalisha nyinyi, hatoki mikono mitupu yule mwenye kuwajia, hapati hasara yule mwenye kuwapenda na wala hafanikiwi yule mwenye uadui nanyi.”

Kisha nenda kwenye Msikiti wa Uhud, nao ni ule msikiti uliyo karibu, Sali humo rakaa mbili ukiongezea na sala ya maamkizi ya msikiti, kisha nenda kwenye eneo la kaburi na sema:

اللَّهُمَّ صَلِّ عَلَى مُحَمَّدٍ وَآلِ مُحَمَّدٍ، اللَّهُمَّ إِنِّي تَعَرَّضْتُ
 لِرَحْمَتِكَ بِلُزُومِي لِقَبْرِ عَمِّ نَبِيِّكَ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ لِيُجِيرَنِي مِنْ
 نِقْمَتِكَ وَسَخَطِكَ وَمَقْتِكَ فِي يَوْمِ تَكْثُرُ فِيهِ الْأَصْوَاتُ، وَتَشْغَلُ
 كُلُّ نَفْسٍ بِمَا قَدَّمَتْ، وَتُجَادِلُ عَنْ نَفْسِهَا، فَإِنْ تَرَحَّصَنِي الْيَوْمَ
 فَلَا خَوْفَ عَلَيَّ وَلَا حُزْنَ، وَإِنْ تَعَاقَبُ فَبُولِي لَهُ الْقُدْرَةُ عَلَى
 عِبَادِهِ، وَلَا تُخَيِّبْنِي بَعْدَ الْيَوْمِ، وَلَا تَصْرِفْنِي بِغَيْرِ حَاجَتِي،
 فَقَدْ لَصِقْتُ بِقَبْرِ عَمِّ نَبِيِّكَ، وَتَقَرَّبْتُ بِهِ إِلَيْكَ ابْتِغَاءَ
 مَرْضَاتِكَ، وَرَجَاءِ رَحْمَتِكَ فَتَقَبَّلْ مِنِّي، وَعُدْ بِحِلْمِكَ عَلَيَّ
 جَهْلِي، وَبِرَأْفَتِكَ عَلَيَّ جِنَايَةَ نَفْسِي، فَقَدْ عَظُمَ جُرْمِي، وَمَا أَخَافُ
 أَنْ تَظْلِمَنِي وَلَكِنْ أَخَافُ سُوءَ الْحِسَابِ، فَانظُرِ الْيَوْمَ تَقَلُّبِي عَلَى
 قَبْرِ عَمِّ نَبِيِّكَ، فَبِهَا فُكِّنِي مِنَ النَّارِ وَلَا تُخَيِّبْ سَعْيِي، وَلَا
 يَهُونَنَّ عَلَيْكَ ابْتِهَالِي، وَلَا تَحْجِبَنَّ عَنْكَ صَوْتِي، وَلَا تَقْلِبْنِي بِغَيْرِ
 حَوَائِجِي،

يَا غِيَاثَ كُلِّ مَكْرُوبٍ وَمَحْزُونٍ، وَيَا مُفْرَجاً عَنِ الْمَلْهُوفِ
الْحَيْرَانَ الْغَرِيقِ الْبُشْرِفِ عَلَى الْهَلَكَةِ، فَصَلِّ عَلَى مُحَمَّدٍ وَآلِ
مُحَمَّدٍ، وَاَنْظُرْ إِلَى نَظْرَةً لَا أَشْتَى بَعْدَهَا أَبَداً، وَارْحَمْ تَضَرُّعِي
وَعَبْرَتِي وَانْفِرَادِي، فَقَدْ رَجَوْتُ رِضَاكَ، وَتَحَرَّيْتُ الْخَيْرَ الَّذِي
لَا يُعْطِيهِ أَحَدٌ سِوَاكَ، فَلَا تَرُدَّ أَمَلِي،

اللَّهُمَّ إِنَّ تَعَاقِبُ فَبَوْلٍ لَهُ الْقُدْرَةُ عَلَى عِبَادِهِ، وَجَزَائِهِ بِسُوءِ
فِعْلِهِ، فَلَا أَخِيْبَنَّ الْيَوْمَ، وَلَا تَضَرِّفْنِي بِغَيْرِ حَاجَتِي، وَلَا تَخَيِّبَنَّ
شُخُوصِي وَوَفَادَتِي، فَقَدْ أَنْفَدْتُ نَفَقَتِي، وَأَتَعَبْتُ بَدَنِي، وَقَطَعْتُ
الْبَفَازَاتِ، وَخَلَّفْتُ الْأَهْلَ وَالْبَالَ وَمَا خَوَّلْتَنِي، وَأَثَرْتُ مَا
عِنْدَكَ عَلَى نَفْسِي، وَلُذْتُ بِقَبْرِ عَمِّ نَبِيِّكَ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ،
وَتَقَرَّرْتُ بِهِ ابْتِغَاءَ مَرْضَاتِكَ، فَعُدْ بِحَبْلِكَ عَلَى جَهْلِي،
وَبِرَأْفَتِكَ عَلَى ذَنْبِي، فَقَدْ عَظَمَ جُرْمِي بِرَحْمَتِكَ يَا كَرِيمُ يَا كَرِيمُ

“Ewe Mwenyezi Mungu! Msalie Muhammad na aali
Muhammad! Ewe Mwenyezi Mungu! Hakika mimi

nimezitifuta rehema Zako kwa kuliandama kaburi la ami ya Nabii Wako (s.a.w.w.) ili aniepushe na adhabu Yako, ghadhabu Yako na hasira Zako siku ambayo sauti humo zitakithiri na kila nafsi itajishughulisha na yale iliyoyatanguliza na kujijadili yenyewe, hivyo ikiwa leo utanirehemu basi sintakuwa na hofu wala huzuni, na kama utaniadhibu ni kwa sababu bwana ana uwezo juu ya mtumwa wake, na wala usinirudishe mikono mitupu baada ya leo, na wala usiniondoe bila haja yangu, bila shaka nimejiambatanisha na kaburi la ammi ya Nabii Wako na nimejikurubisha Kwako kupitia kwake kwa ajili ya kutafuta radhi Zako na nikitaraji rehema Zako, hivyo pokea toka kwangu na urudie ujinga wangu kwa upole Wako, na makosa ya nafsi yangu kwa huruma Yako, kwani makosa yangu ni makubwa na hofu yangu si kwamba utanidhulumu lakini ninalohofu ni hesabu yangu mbaya. Utazame leo kwa huruma ugeukaji wangu juu ya kaburi la ami ya Nabii Wako (a.s.) na kwa kupitia kwao nikomboe dhidi ya moto, na wala usiurudishe mwendo wangu bila kitu, na wala unyenyekevu wangu usiwe mwepesi Kwako, na wala usiizuie sauti yangu na Wewe, na wala usinigeuze bila haja zangu.

“Ewe Uliye msaada wa kila mwenye kutatizwa mwenye kuhuzunishwa! Na ewe mfariji wa kila aliyedhikika, mwenye kufadhaika, mwenye kuzama na mwenye kufikwa na maangamio! Msalie Muhammad na aali Muhammad na unitazame mtazamo ambao sintahangaika baada yake abadani, na urehemu unyenyekevu wangu na kilio changu na upweke wangu, kwani bila shaka nimetaraji ridhaa Zako na nimechagua kheri ambayo haitoi yeyote isipokuwa Wewe, hivyo usiyarudishe matarajio yangu.

“Ewe Mwenyezi Mungu! Ukiniadhibu hiyo ni kwa sababu bwana ana uwezo juu ya mtumwa wake na ni kwa sababu ya malipo ya ubaya wa vitendo vyake, hivyo usinitoe mikono mitupu leo na wala usiniondoe bila haja yangu, na wala usinirudishe mikono mitupu utengano wangu na ugeni wangu, kwani bila shaka nimemaliza masurufu yangu, nimeuchosha mwili wangu, nimekata masafa, nimeiacha familia na mali na uliyonitunuku, na nimetanguliza kilichopo Kwako kabla ya nafsi yangu, nimekimbilika kwenye kaburi la ammi ya Nabii Wako (s.a.w.w.) na nimejikurubisha kwake nikitafuta radhi Zako, hivyo urudie ujinga wangu kwa upole Wako, na dhambi zangu kwa huruma Yako, kwani hakika kosa langu ni kubwa, kwa rehema Zako ewe Mkarimu, ewe Mkarimu.

Namna ya kuwazuru wahanga huko Uhud:

Sema katika Ziyara yao:

اَلسَّلَامُ عَلٰى رَسُوْلِ اللّٰهِ، اَلسَّلَامُ عَلٰى نَبِيِّ اللّٰهِ، اَلسَّلَامُ عَلٰى
 مُحَمَّدِ بْنِ عَبْدِ اللّٰهِ، اَلسَّلَامُ عَلٰى اَهْلِ بَيْتِهِ الطّٰهَرِيْنَ، اَلسَّلَامُ
 عَلَيْكُمْ اَيُّهَا الشُّهَدَاءُ الْبُؤْمُنُونَ، اَلسَّلَامُ عَلَيْكُمْ يَا اَهْلَ بَيْتِ
 الْاَيْمَانِ وَالتَّوْحِيدِ، اَلسَّلَامُ عَلَيْكُمْ يَا اَنْصَارَ دِيْنِ اللّٰهِ وَاَنْصَارَ
 رَسُوْلِهِ عَلَيْهِ وَاٰلِهِ السَّلَامُ، سَلَامٌ عَلَيْكُمْ بِمَا صَبَرْتُمْ فَنِعْمَ عُقْبَى
 الدَّارِ،

أَشْهَدُ أَنَّ اللَّهَ اخْتَارَكُمْ لِدِينِهِ، وَأَصْطَفَاكُمْ لِرَسُولِهِ، وَأَشْهَدُ
 أَنَّكُمْ قَدْ جَاهَدْتُمْ فِي اللَّهِ حَقَّ جِهَادِهِ، وَذَبَبْتُمْ عَنْ دِينِ اللَّهِ وَعَنْ
 نَبِيِّهِ، وَجُدْتُمْ بِأَنْفُسِكُمْ دُونَهُ، وَأَشْهَدُ أَنَّكُمْ قُتِلْتُمْ عَلَى مِنْهَاجِ
 رَسُولِ اللَّهِ، فَجَزَاكُمْ اللَّهُ عَنْ نَبِيِّهِ وَعَنِ الْإِسْلَامِ وَأَهْلِهِ أَفْضَلَ
 الْجَزَاءِ، وَعَرَّفْنَا وُجُوهَكُمْ فِي مَحَلِّ رِضْوَانِهِ، وَمَوْضِعِ إِكْرَامِهِ،
 مَعَ النَّبِيِّينَ وَالصَّادِقِينَ وَالشُّهَدَاءِ وَالصَّالِحِينَ وَحَسَنَ أَوْلِيكَ
 رَفِيقًا، أَشْهَدُ أَنَّكُمْ حِزْبُ اللَّهِ، وَأَنَّ مَنْ حَارَبَكُمْ فَقَدْ حَارَبَ اللَّهَ،
 وَأَنَّكُمْ لِبَنِّ الْبُقَرَّيْنِ الْفَائِزِينَ الَّذِينَ هُمْ أَحْيَاءٌ عِنْدَ رَبِّهِمْ
 يُرْزَقُونَ، فَعَلَى مَنْ قَتَلَكُمْ لَعْنَةُ اللَّهِ وَالْبَلَايَةُ وَالنَّاسِ
 أَجْمَعِينَ،

أَتَيْتُكُمْ يَا أَهْلَ التَّوْحِيدِ زَائِرًا، وَبِحَقِّكُمْ عَارِفًا، وَبِزِيَارَتِكُمْ إِلَى
 اللَّهِ مُتَقَرِّبًا، وَبِهَا سَبَقَ مِنْ شَرِيفِ الْأَعْمَالِ وَمَرْضِيِّ الْأَفْعَالِ
 عَالِبًا، فَعَلَيْكُمْ سَلَامُ اللَّهِ وَرَحْمَتُهُ وَبَرَكَاتُهُ، وَعَلَى مَنْ قَتَلَكُمْ

لَعْنَةُ اللَّهِ وَغَضَبُهُ وَسَخَطُهُ، اللَّهُمَّ انْفَعْنِي بِزِيَارَتِهِمْ، وَثَبِّتْنِي
 عَلَى قَصْدِهِمْ، وَتَوَقَّنِي عَلَى مَا تَوَقَّيْتَهُمْ عَلَيْهِ، وَاجْمَعْ بَيْنِي
 وَبَيْنَهُمْ فِي مُسْتَقَرِّ دَارِ رَحْمَتِكَ، أَشْهَدُ أَنْكُمْ لَنَا فَرْطٌ وَنَحْنُ بِكُمْ
 لَاحِقُونَ

“Amani iwe juu ya Mtume wa Mwenyezi Mungu! Amani iwe juu ya Nabii wa Mwenyezi Mungu! Amani iwe juu ya Muhammad bin Abdillah! Amani iwe juu ya watu wa nyumba yake watakasifu! Amani iwe juu yenu enyi wahanga waumini! Amani iwe juu yenu enyi watu wa nyumba ya imani na Tauhidi! Amani iwe juu yenu enyi watetezi wa dini ya Mwenyezi Mungu na watetezi wa Mtume wake! Amani iwe juu yake na juu ya aali zake! Amani iwe juu yenu kwa subira mliyofanya, ni nzuri iliyoje nyumba ya baadaye.

“Nashahidilia kwamba hakika Mwenyezi Mungu amewachagua kwa ajili ya dini Yake na amewateua kwa ajili ya Mtume Wake. Na nashahidilia kwamba hakika nyinyi mmepigana jihadi kwa ajili ya Mwenyezi Mungu jihadi ya kweli, mmejitoa kwa ajili ya dini ya Mwenyezi Mungu na Nabii Wake, na mmejitema kwa kumtetea Yeye. Na nashahidilia kwamba hakika nyinyi mmeuwawa katika njia ya Mtume wa Mwenyezi Mungu, hivyo naomba Mwenyezi Mungu awalipe kwa ajili ya Nabii Wake, Uislamu na watu wake malipo bora. Na atatambulisha nyuso zenu mahali pa ridhaa Yake na sehemu ya ukarimu Wake pamoja na Manabii, Masidiki, Mashahidi na

Wasalihina, na hao wana urafiki mzuri. Nashahidilia kwamba hakika nyinyi ni kundi la Mwenyezi Mungu na kwamba mwenye kuwapiga vita nyinyi amempiga vita Mwenyezi Mungu, na kwamba hakika nyinyi ni miongoni mwa waliokurubishwa wenye kufuzu, ambao wao wako hai kwa Mola wao Mlezi wakiruzukiwa, hivyo laana ya Mwenyezi Mungu, Malaika na watu wote iwe juu ya wale waliokuuweni.

“Nimekujieni enyi wanatauhidi hali ni mwenye kuwazuru na ni mwenye kutambua haki zenu, na ni mwenye kujikurubisha kwa Mwenyezi Mungu kwa ziara yenu, na ni mwenye kujua amali njema zilizotangulia na vitendo vya kuridhiwa, hivyo amani ya Mwenyezi Mungu iwe juu yenu, na pia rehema Zake na Baraka Zake. Na laana ya Mwenyezi Mungu, ghadhabu Zake na hasira Yake viwe juu ya wale waliokuuweni. Ewe Mwenyezi Mungu! Ninufaishe kwa ziara yao na nithibitisha juu ya kusudio lao, na nifishe katika yale uliyowafisha wao, na nikusanye mimi na wao pamoja katika nyumba ya kudumu ya rehema Zako. Nashahidilia hakika nyinyi ni wenye kututangulia nasi ni wenye kuwakuta.

Kisha soma Sura al-Qadri kiasi uwezavyo, kisha nenda kwenye msikiti uliyopo karibu na Sali humo rakaa mbili kwa ajili ya ziyara.

Namna ya kumzuru Abu Dharr al-Ghaffariy:

Ni Sunna kumzuru Abu Dharr (r.a.) huko Rabadha, na kwa mujibu wa kitabu *Bihar* katika mlango unaohusu ziara ni kwamba Rabadha ni karibu na Safrau kuliani mwa njia itokayo Makka kuelekea Madina, na kwa hivi sasa inaitwa al-Wasitu (kiunganishi). Mwandishi wa kitabu *Miftahul-Janati* ametaja ziyara hii kwa ajili yake:

أَسْلَامُ عَلَيْكَ يَا أَبَا ذَرٍّ الْغِفَارِيُّ، أَسْلَامُ عَلَيْكَ يَا صَاحِبَ
 رَسُولِ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ، وَرَحْمَةُ اللَّهِ وَبَرَكَاتُهُ، أَسْلَامُ
 عَلَيْكَ يَا مَنْ قَالَ فِي حَقِّهِ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ : مَا
 أَقَلَّتِ الْغُبْرَاءُ وَلَا أَظَلَّتِ الْخَضْرَاءُ عَلَى ذِي لَهْجَةٍ أَصْدَقَ مِنْ أَبِي
 ذَرٍّ، أَسْلَامُ عَلَيْكَ يَا مَنْ نَطَقَ بِالْحَقِّ، وَلَمْ يَخَفْ فِي اللَّهِ لَوْمَةً
 لَائِمًا، وَلَا ظُلْمًا ظَالِمًا، أَتَيْتُكَ زَائِرًا شَاكِرًا لِبِلَاتِكَ فِي الْإِسْلَامِ،
 فَاسْأَلُ اللَّهَ الَّذِي خَصَّكَ بِصِدْقِ اللَّهْجَةِ وَالْخُشُونَةِ فِي ذَاتِ اللَّهِ
 وَمُتَابَعَةِ الْخَيْرِينَ الْفَاضِلِينَ أَنْ يُحْيِيَنِي حَيَاتِكَ، وَيُيَسِّرَ لِي
 مَبَاتِكَ، وَيَحْشُرَنِي مَحْشَرَكَ، عَلَى إِنْكَارِ مَا أَنْكَرْتَ، وَمُنَابَذَةِ
 مَنْ نَابَذْتَ، جَمَعَ اللَّهُ بَيْنَنَا وَبَيْنَكَ وَبَيْنَ رَسُولِهِ وَآلِهِ صَلَّى
 اللَّهُ عَلَيْهِ وَعَلَيْهِمْ فِي مُسْتَقَرِّ رَحْمَتِهِ، وَالسَّلَامُ عَلَيْكَ وَرَحْمَةُ
 اللَّهِ وَبَرَكَاتُهُ

“Amani iwe juu yako ewe Abu Dharr al-Ghaffariy! Amani
 iwe juu yako ewe sahaba wa Mtume wa Mwenyezi Mungu,
 na pia rehema za Mwenyezi Mungu na baraka Zake!

Amani iwe juu yako ewe ambaye Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) alisema kuhusu haki yake: “Mbingu haijamfunika wala ardhi haijambeba mtu mkweli kuliko Abu Dharri!” Amani iwe juu yako ewe ambaye alitamka haki na hajaogopa katika jambo la Mwenyezi Mungu lawama ya mwenye kulaumu wala dhulma ya mwenye kudhulumu! Nimekujia na hali ni mwenye kukuzuru mwenye kushukuru mtihani wako katika Uislamu, hivyo namuomba Mwenyezi Mungu ambaye aliyekuhusisha na ulimi wa kweli, kujinyima (utawa) kwa ajili ya Mwenyezi Mungu na kuwafuata wabora, anihuishe maisha yako, anifishe kifo chako na anikusanye pamoja nawe kwa kuyakanusha yale uliyokanusha na kuyatupilia mbali yale uliyoyatupilia mbali. Namuomba Mwenyezi Mungu atokusanye sisi na wewe na Mtume Wake na aali zake (s.a.w.w.) kwenye makazi ya rehema Zake. Amani ziwe juu yako na rehema za Mwenyezi Mungu na baraka Zake.”

FADHILA ZA KUMZURU HAMZA BWANA WA WAHANGA, NA WAHANGA WENGINE HUKO UHUD

Fakhrul-Muhaqiqina ametaja katika kitabu *Risalatul-Fakhriyyah* kwamba: “Ni Sunna kumzuru Hamza na wahanga wengine huko Uhud. Imepokewa kutoka kwa Mtume (s.a.w.w.) kwamba alisema: “Atakayenizuru mimi bila kumzuru ammi yangu Hamza bila shaka atakuwa ameninyanyapaa.”

Sheikh al-Mufid amesema: “Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) alikuwa ameamuru kulizuru kaburi la Hamza (a.s.), na alikuwa akimtilia manani yeye na wahanga, na Fatima (a.s.) baada ya kifo chake (s.a.w.w.) aliendelea kwenda mara kwa mara kwenye kaburi lake (a.s.). Na ilikuwa ni sera ya kawaida kwa waislamu zama zake (s.a.w.w.) kumzuru Hamza (a.s.) na kulitilia manani kaburi lake.

Katika Hadithi imesemwa kwamba: Fatima (a.s.) baada ya baba yake aliishi siku sabini na tano bila kuonekana akiwa na furaha wala kucheka, huku akiyajia makaburi ya wahanga kila siku ya Ijumaa mara mbili, na siku ya Jumatatu na Alhamisi na akisema: Hapa ndipo Mtume wa Mwenyezi Mungu alipokuwepo, na hapa ndipo mushrikina walipokuwepo. Na katika nukuu nyingine ni kwamba alikuwa akisali hapo na kuomba dua. Wahanga wa Uhud ni takribani sabini, nao ni Hamza (a.s.), Abdullah bin Jahshi, Mus’ab bin Umayri, Ammarat bin Ziyad, Shimas bin Uthman na wengineo radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yao.

FASLU YA SABA

**INAHUSU MISIKITI NA MAENEO
YALIYOBARIKIWA HUKO MADINA NA
PEMBEZONI MWAKE**

Kwanza: Msikiti wa Mtume (s.a.w.w.):

Kabla hatujagusia hilo ni lazima utambue kwamba Madina ina eneo maalumu lililo tukufu kama Makka. Mipaka yake ni kuanzia Airu mpaka Iru, na kila mmoja ni mlima unaoizunguka Madina, mmoja ni kutokea Mashariki na mwingine ni kutokea Magharibi. Hiyo ndio mipaka ya eneo tukufu la Madina, na ijapokuwa si wajibu kuhirimia ndani ya eneo hilo kama ilivyo wajibu kwa eneo tukufu la Makka tukufu lakini inapasa kuliheshimu kwa ajili ya wale wanaoishi eneo hilo.

Ama mambo yaliyo Sunna humo ni:

1. Josho (Ghusli) kwa ajili ya kuingia Madina, kuingia Msikitini na kumzuru Mtume (s.a.w.w.). Inaruhusiwa kuoga josho moja kwa nia ya mambo yote matatu.
2. Wakati wa kuingia Msikitini usali rakaa mbili Sala ya maamkizi, kama ilivyotangulia.
3. Kusali Sala tano za wajibu Msikitini. Na thawabu za kusalia humo kwa mujibu wa baadhi ya riwaya ni sawa na thawabu na malipo ya Sala elfu kumi zinazosaliwa eneo lingine. Na sehemu bora kabisa humo Msikitini ni eneo lililopo kati ya mimbari na kaburi la Mtume (s.a.w.w.) (Raudha).

4. Umsalimie Mtume (s.a.w.w.) kwa niaba ya wazazi wawili, ndugu na marafiki.
5. Usali rakaa mbili baada ya Ziyara na thawabu zake uzitoe zawadi kwa Mtume (s.a.w.w.) kama ilivyotangulia.
6. Kusimama kwenye kaburi tukufu, kumhimidi Allah, kumtukuza na kuomba dua.
7. Kusali na kuomba dua kwenye Maqam Jibril (a.s.) kama ilivyotangulia.
8. Usali ndani ya nyumba ya Fatima (a.s.) na umzuru huko.
9. Umsalie Mtume (s.a.w.w.) wakati wa kuingia Msikitini na wakati wa kutoka.
10. Usali kwenye mihrabu ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) kama ilivyotangulia, na inapasa ukithirishe kusoma Qur'ani tukufu katika Msikiti wa Mtume (s.a.w.w.), kwani hapo ndio kituo cha wahyi na Chuo kikuu na Shule kubwa ya mafunzo yake yenye manufaa, mawaidha yake yenye kuponyesha, maelekezo yake ya juu kwa Ummah wa kiislamu, na humo ndimo walimohitimu masahaba wakubwa miongoni mwa watangulizi wetu wema, radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yao wote.
11. Usali rakaa mbili kwenye nguzo ya Abu Lubabah inayojulikana kama nguzo ya toba, kama ilivyotangulia.

12. Usali na kuomba dua eneo lililopo kati ya mimbari na kaburi la Mtume (s.a.w.w.) (Raudha), kama ilivyotangulia.
13. Usiinue sauti yako Msikitini.
14. Utoe sadaka kwa mafakiri na masikini huko Madina kadiri uwezavyo. Al-Majlisiy ametaja katika Hadithi sahihi kwamba: “Sadaka ya dirhamu moja huko Madina ni sawa na dirhamu elfu kumi eneo lingine.”
15. Uwafanyie wema masharifu na kizazi cha Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) ili upate thawabu na malipo makubwa.

Pili: Msikiti wa Quba:

Nao ni ule msikiti ambao ulijengwa juu ya uchamungu toka siku ya kwanza, pale Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alipohamia Madina na akashuka hapo Quba, akakaa hapo zaidi ya siku ishirini akiwa anapunguza Sala, akingojea kuja kwa binamu yake Ali bin Abu Talib (a.s.). Msikiti huu uliasisiwa kabla ya Msikiti wa Madina, na humo ndimo ilimoteremkia kauli ya Mwenyezi Mungu: **“Hakika Msikiti uliojengwa juu ya msingi wa kumcha Mwenyezi Mungu tangu siku ya kwanza unastahili zaidi wewe usimame humo. Humo wamo watu wanaopenda kujitakasa, na Mwenyezi Mungu anawapenda wanaojitakasa.”** (Sura Tawba: 108).

Ni Sunna kusali ndani ya msikiti huu mtukufu na kuomba dua humo. Imepokewa kutoka kwa Mtume (s.a.w.w.) kwamba alisema: “Atakayechukua tohara nyumbani kwake na akaja Msikiti wa Quba na kusali humo rakaa mbili atapata malipo sawa na ya Umra.” Hivyo Sali humo Sala

ya maamkizi rakaa mbili, na baada ya Sala fanya tasbihi ya Fatima Zahrau (a.s.), na ni bora uombe dua hii:

اللَّهُمَّ إِنَّكَ قُلْتَ وَقَوْلِكَ الْحَقُّ فِي كِتَابِكَ الْمُنَزَّلِ عَلَى صَدْرِ
نَبِيِّكَ الْمُرْسَلِ: “ لَسَجِدٌ أُسِّسَ عَلَى التَّقْوَى مِنْ أَوَّلِ يَوْمٍ
أَحَقُّ أَنْ تَقُومَ فِيهِ، فِيهِ رِجَالٌ يُحِبُّونَ أَنْ يَتَطَهَّرُوا وَاللَّهُ يُحِبُّ
الْمُطَهَّرِينَ ” اللَّهُمَّ طَهِّرْ قُلُوبَنَا مِنَ النِّفَاقِ، وَأَعْمَانَا مِنَ
الرِّيَا، وَفُرُوجَنَا مِنَ الزِّنَا، وَالسِّنَّتَنَا مِنَ الْكِذْبِ وَالْغَيْبَةِ،
وَأَعْيُنَنَا مِنَ الْخِيَانَةِ، فَإِنَّكَ تَعْلَمُ خَائِنَةَ الْأَعْيُنِ وَمَا تُخْفِي
الصُّدُورُ، رَبَّنَا ظَلَمْنَا أَنْفُسَنَا وَإِنْ لَمْ تَغْفِرْ لَنَا وَتَرْحَمْنَا لَنَكُونَنَّ
مِنَ الْخَاسِرِينَ

“Ewe Mwenyezi Mungu! Hakika Wewe ulisema katika kitabu Chako kilichotelemshwa juu ya kifua cha Nabii Wako aliyetumwa, na kauli yako ni haki, kwamba: **“Hakika Msikiti uliojengwa juu ya msingi wa kumcha Mwenyezi Mungu tangu siku ya kwanza unastahili zaidi wewe usimame humo. Humo wamo watu wanaopenda kujitakasa, na Mwenyezi Mungu anawapenda wanaojitakasa.”** Ewe Mwenyezi Mungu takasa nyoyo zetu na unafiki, matendo yetu na kujionyesha, tupu zetu na zinaa, ndimi zetu na uongo na utesi, na macho

yetu na hiyana, kwani hakika Wewe unajua hiyana ya macho na yanayoficha vifua. Ewe Mola wetu Mlezi! Tumezidhulumu nafsi zetu na kama hutatughufiria na kuturehemu bila shaka tutakuwa miongoni mwa wenye hasara.”

Hapa kuna dua ndefu imetajwa katika mlango wa ziyara wa kitabu *al-Bihar*, tumeacha kuitaja kutokana na kufanya mukhtasari.

Nyuma ya msikiti huu kuna nyumba ya Amirul-Muuminina Ali (a.s.). Mbele ya msikiti huu kuna kisima ambacho maji yake yalikuwa matamu na mengi lakini hivi sasa yamekauka. Na inasemekana kwamba pete ya Mtume (s.a.w.w.) ilidondokea humo ndipo kikaitwa Kisima cha Pete. Na pia kinaitwa Kisima cha Mate ya Mtume (s.a.w.w.) kutokana na lile linalosemwa kwamba Mtume (s.a.w.w.) alitemea mate humo na ndipo maji yake yakawa matamu, na kabla ya hapo yalikuwa ya chumvichumvi.

Tatu: Chumba cha mama yake Ibrahim:

Nacho ni chumba cha mama yake Ibrahim mtoto wa Mtume (s.a.w.w.), na jina lake ni Maria al-Qibtiyyah. Kilikuwa ni makazi ya Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) na msala wake, nacho kimeungana na Msikiti wa Quba. Sali humo rakaa mbili ukiweza, na omba haja yako kutoka kwa Mwenyezi Mungu.

Nne: Msikiti wa al-Fadhikhu:

Nao unaitwa kwa jina la mtende uliokuwepo hapo, nao ni msikiti uliyopo upande wa Mashariki mwa Msikiti wa Quba, na pia huitwa kwa jina la Msikiti wa Mtende. Nao ni ule msikiti ambao jua lilirejeshwa kwa ajili ya Imam Ali

(a.s.), akasali Sala ya Alasiri alipokuwa amepitwa na wakati kwa sababu ya kulazwa na Mtume mapajani mwake, alipomaliza kusali lilitoweka mtoweko wa nyota.Sali humo rakaa mbili za maamkizi ukiweza, na omba haja zako toka kwa Mwenyezi Mungu, na ni bora uombe dua hii:

اللهم صلّ على محمّد وآل محمّد ولا تدع لي في هذا البكان
الكرّم والسجد البعظّم ذنباً إلاّ غفرته ولا هباً إلاّ فرّجته ولا
مرضاً إلاّ شفّيته ولا عيباً إلاّ سترته ولا زرقاً إلاّ بسطته ولا
خوفاً إلاّ آمنتّه ولا شلاًّ إلاّ جمعتّه ولا غائباً إلاّ حفظته وأدنيته
ولا ديناً إلاّ أدّيته ولا حاجة من حوائج الدنيا والآخرة لك فيها
رضى ولى فيها صلاحاً إلاّ قضيتها يا أرحم الرّاحبين

“Ewe Mwenyezi Mungu! Msalie Muhammad na aali Muhammad, na wala usiache kwa ajili yangu katika eneo hili tukufu na msikiti huu muadhamu dhambi yoyote ila uwe umeighfuri, wala tatizo lolote ila uwe umeliondoa, wala maradhi yoyote ila uwe umeniponya, wala dosari yoyote ila uwe umeisitiri, wala riziki yoyote ila uwe umeikunjua, wala khofu yoyote ila uwe umeiondoa, wala mtawanyiko wowote ila uwe umeikusanya, wala yeyote aliye mbali ila uwe umemuhifadhi na kumleta karibu, wala deni lolote ila uwe umelipa, wala haja yoyote miongoni mwa haja za dunia na akhera uliyo radhi nayo na yenye

wema kwangu ila uwe umeitekeleza. Ewe Mwenye kurehemu kushinda wote wenye kurehemu.”

Tano: Msikiti wa Fat’hu:

Pia huitwa Msikiti wa Ahzab (Makundi). Upo juu ya mlima, umeitwa msikiti wa Fat’hu (Ushindi) kutokana na Mwenyezi Mungu kuwapa ushindi Waislamu mikononi mwa Ali bin Abu Talib (a.s.) kwa kumuua Amru bin Abdi Wudi al-Amiriy, na hapo makundi ya upinzani yakashindwa. Allah anasema: **“Na wale waliokufuru Mwenyezi Mungu amewarudisha na ghadhabu yao, hawakupata chochote katika kheri, na Mwenyezi Mungu amewatoshea Waumini katika mapigano, Mwenyezi Mungu ni Mwenye uwezo Mwenye nguvu.”** (Sura Ahzab: 25). Hayo yote ni kutokana dua ya Mtume (s.a.w.w.) aliyoiomba eneo hili. Sali humo rakaa mbili na usome dua hii:

يَا صَرِيحَ الْبَكْرُوبَيْنِ، وَيَا مُجِيبَ دَعْوَةِ الْبُضْطَرِّينِ، وَيَا مُغِيثَ
الْبَهْمُومِينَ، اكْشِفْ عَنِّي ضُرِّي وَهَتِّي وَكَرْبِي وَعَنِّي كَمَا كَشَفْتَ
عَنْ نَبِيِّكَ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ هَبْتُهُ، وَكَفَيْتَهُ هَوْلَ عَدُوِّهِ،
وَاكْفِنِي مَا أَهْبَتَنِي مِنَ أَمْرِ الدُّنْيَا وَالْآخِرَةِ، يَا أَرْحَمَ الرَّاحِمِينَ

“Ewe uliye kilio cha wenye mashaka! Ewe Mwenye kujibu maombi ya wenye kudhikika! Ewe Mwenye kuwasaidia wenye kunyong’onyeshwa! Niondolee dhiki, unyonge, mashaka, na adha, kama ulivyomuondolea Nabii Wako (s.a.w.w.) unyonge wake na ukamtosheleza kitisho cha

adui yake. Na nitosheleze yale yanayonitia unyonge miongoni mwa mambo ya dunia na Akhera. Ewe Mwenye kurehemu kushinda wote wenye kurehemu.”

Sita: Msikiti wa Ali, Msikiti wa Fatima Zahrau (a.s.), na Msikiti wa Salman (r.a.):

Nayo ipo karibu na Msikiti wa Ushindi, ni Sunna kusali ndani ya misikiti yote.

Saba: Nyumba ya Imam Zainul-Abidin, Imam Ja'far as-Sadiq (a.s.) na Msikiti wa Mubahala (Maapizano):

Ni Sunna kusali ndani ya Nyumba ya Imam Zainul-Abidin, Imam Ja'far as-Sadiq (a.s.) na pia katika Msikiti wa Mubahala (Maapizano). Nenda maeneo haya matukufu na usali humo ukiweza, omba humo utakacho, na ni bora uombe dua hii:

اللَّهُمَّ إِنِّي أَسْأَلُكَ صَبْرَ الشَّاكِرِينَ لَكَ، وَعَمَلَ الْخَائِفِينَ مِنْكَ،
وَيَقِينَ الْعَابِدِينَ لَكَ. اللَّهُمَّ أَنْتَ الْعَلِيُّ الْعَظِيمُ، وَأَنَا عَبْدُكَ
الْبَائِسُ الْفَقِيرُ، وَأَنْتَ الْغَنِيُّ الْحَيِّدُ، وَأَنَا الْعَبْدُ
الدَّلِيلُ، اللَّهُمَّ صَلِّ عَلَى مُحَمَّدٍ وَآلِ مُحَمَّدٍ، وَامْنُنْ بِغِنَاكَ
عَلَى فَقْرِي، وَبِحِلْبِكَ عَلَى جَهْلِي، وَبِقُوَّتِكَ عَلَى ضَعْفِي، يَا قَوِي

يَا عَزِيزُ، اَللّٰهُمَّ صَلِّ عَلٰى مُحَمَّدٍ وَّآلِ مُحَمَّدٍ الْاَوْصِيَاءِ
الْبَرِّضِيِّينَ، وَاكْفِنِيْ مَا اَهْبَنِيْ مِنْ اَمْرِ الدُّنْيَا وَاَلْاٰخِرَةِ يَا اَرْحَمَ
الرَّاحِمِيْنَ

“Ewe Mwenyezi Mungu! Hakika mimi nakuomba subira ya wenye kukushukuru, amali ya wenye hofu Nawe na yakini ya wenye kukuabudu Wewe. Ewe Mwenyezi Mungu! Wewe ni Mkuu uliye Adhimu, na mimi ni mja Wako mkata aliye fakiri. Wewe ni Tajiri aliye Muhimidiwa, na mimi ni mja aliye dhalili. Ewe Mwenyezi Mungu! Msalie Muhammad na aali Muhammad na umimine utajiri Wako juu ya ufakiri wangu, uvumilivu Wako juu ya ujinga wangu na nguvu Zako juu ya udhaifu wangu. Ewe Mwenye nguvu! Ewe Mtukufu! Ewe Mwenyezi Mungu! Msalie Muhammad na aali zake mawasii walioridhiwa, na nitosheleze yale yaliyonitia unyonge miongoni mwa mambo ya dunia na Akhera. Ewe Mwenye kurehemu kushinda wote wenye kurehemu.”

Nane: Msikiti wa Kibla mbili (*Qiblatayn*):

Ni Sunna kusali ndani ya Msikiti wa Kibla mbili (*Qiblatayn*) na usome dua hii:

اَللّٰهُمَّ اِنَّ هٰذَا مَسْجِدُ الْقِبْلَتَيْنِ، وَمُصَلِّي نَبِيِّنَا وَحَبِيْبِنَا
وَسَيِّدِنَا مُحَمَّدٍ صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهِ وَسَلَّمَ. اَللّٰهُمَّ اِنَّكَ قَدَّتْ

وَقَوْلِكَ الْحَقُّ فِي كِتَابِكَ الْمُنْزَلِ عَلَى صَدْرِ نَبِيِّكَ الْمُرْسَلِ: قَدْ
 نَرَى تَقَلُّبَ وَجْهِكَ فِي السَّمَاءِ فَلَنُوَلِّيَنَّكَ قِبْلَةً تَرْضِيهَا فَوَلِّ
 وَجْهَكَ شَطْرَ الْمَسْجِدِ الْحَرَامِ اللَّهُمَّ كَمَا بَلَّغْتَنَا فِي الدُّنْيَا
 زِيَارَتَهُ وَمَاثِرَةَ الشَّرِيفَةِ، فَلَا تُحْرِمْنَا يَا اللَّهُ فِي الْآخِرَةِ مِنْ فَضْلِ
 شَفَاعَةِ مُحَمَّدٍ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ، وَاحْشُرْنَا فِي زُمْرَتِهِ
 وَتَحْتَ لَوَائِهِ، وَأَمْتَنَا عَلَى مَحَبَّتِهِ وَسُنَّتِهِ، وَاسْقِنَا مِنْ حَوْضِهِ
 الْبُورِدِ بِيَدِهِ الشَّرِيفَةِ، شَرْبَةً هَنِئَةً مَرِيئَةً لَا نَظْأُ بَعْدَهَا
 أَبَدًا، إِنَّكَ عَلَى كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ

“Ewe Mwenyezi Mungu! Hakika huu ni msikiti wa Kibla mbili (*Qiblatayn*) na msala wa Nabii wetu, kipenzi chetu na bwana wetu Muhammad (s.a.w.w.). Ewe Mwenyezi Mungu! Hakika Wewe ulisema katika kitabu Chako kilichoteremshwa juu ya kifua cha Nabii Wako aliyetumwa, na kauli Yako ni haki, kwamba: **“Hakika tumeona uso wako ukielekea mbinguni, basi bila shaka tutakugeuza kwenye Kibla ukipendacho. Basi elekeza uso wako upande wa Msikiti Mtukufu.”**²Ewe Mwenyezi Mungu! Kama ulivyotufikisha duniani maziara yake na maeneo matukufu ya athari zake basi usitunyime ewe

2

Sura al-Baqara: 144

Mwenyezi Mungu huko Akhera fadhila za uombezi wa Muhammad (s.a.w.w.), na utukusanye katika kundi lake na chini ya bendera yake na utufishe katika mapenzi yake na sunnah yake, na tunyweshe kwa mkono wake mtukufu toka katika birika lake kinywaji tulivu kiburudishacho ambacho baada yake hakuna kiu milele, hakika Wewe juu ya kila kitu ni Muweza.”

Tisa: Misikiti iliyomo ndani ya mji wa Madina:

Nayo ni kama ifuatavyo:

1. Mskiti wa Ghamam
2. Msikiti wa Imam Ali (a.s.)
3. Msikiti wa Zahra (a.s.).

Sali ndani ya kila mmoja na tumia ipasavyo fursa yako ndani ya maeneo haya matukufu, jiombee na kumuomba yule umpendaye, na hasa wazazi wako wawili na Waumini wote wa kiume na wa kike, waombee kheri ya dunia na Akhera, na wala usighafilike kuomba kheri.

FASLU YA NANE

YAHUSU KUWAZURU WAHANGA WA BADRI (R.A.)

Badri ni kijiji kilichopo baina ya Madina na Makka. Hapo walikufa kishahidi masahaba kumi na nne wa Mtume (s.a.w.w.) katika Vita vya Badri. Baada ya kuwazuru wahanga Sali ndani ya Msikiti wa Arshi uliyopo karibu na wahanga wa Badri. Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) alisalia eneo hili katika vita. Sema katika kuwazuru wahanga:

اَلسَّلَامُ عَلٰى رَسُوْلِ اللّٰهِ، اَلسَّلَامُ عَلٰى نَبِيِّ اللّٰهِ، اَلسَّلَامُ عَلٰى
مُحَمَّدِ بْنِ عَبْدِ اللّٰهِ، اَلسَّلَامُ عَلٰى اَهْلِ بَيْتِهِ الطّٰهَرِيْنَ، اَلسَّلَامُ
عَلَيْكُمْ اَيُّهَا الشُّهَدَاءُ الْمُؤْمِنُونَ، اَلسَّلَامُ عَلَيْكُمْ يَا اَهْلَ بَيْتِ
الْاِيْمَانِ وَالتَّوْحِيْدِ، اَلسَّلَامُ عَلَيْكُمْ يَا اَنْصَارَ دِيْنِ اللّٰهِ وَاَنْصَارَ
رَسُوْلِهِ عَلَيْهِ وَاٰلِهِ السَّلَامُ، سَلَامٌ عَلَيْكُمْ بِمَا صَبَرْتُمْ فَنِعْمَ عُقْبَى
الدَّارِ،

اَشْهَدُ اَنَّ اللّٰهَ اَخْتَارَكُمْ لِدِيْنِهِ، وَاَصْطَفَاكُمْ لِرَسُوْلِهِ، وَاَشْهَدُ
اَنَّكُمْ قَدْ جَاهَدْتُمْ فِي اللّٰهِ حَقَّ جِهَادِهِ، وَذَبَبْتُمْ عَنِ دِيْنِ اللّٰهِ وَعَنْ

نَبِيِّهِ، وَجَدْتُمْ بِأَنْفُسِكُمْ دُونَهُ، وَأَشْهَدُ أَنَّكُمْ قُتِلْتُمْ عَلَى مِنْهَاجِ
 رَسُولِ اللَّهِ، فَجَزَاكُمْ اللَّهُ عَنْ نَبِيِّهِ وَعَنِ الْإِسْلَامِ وَأَهْلِهِ أَفْضَلَ
 الْجَزَاءِ، وَعَرَّفْنَا وَجُوهَكُمْ فِي مَحَلِّ رِضْوَانِهِ، وَمَوْضِعِ إِكْرَامِهِ،
 مَعَ النَّبِيِّينَ وَالصِّدِّيقِينَ وَالشُّهَدَاءِ وَالصَّالِحِينَ وَحَسُنَ أُولَئِكَ
 رَفِيقًا، أَشْهَدُ أَنَّكُمْ حِزْبُ اللَّهِ، وَأَنَّ مَنْ حَارَبَكُمْ فَقَدْ حَارَبَ اللَّهَ،
 وَأَنَّكُمْ لِمَنْ الْمُقَرَّبِينَ الْفَائِزِينَ الَّذِينَ هُمْ أَحْيَاءٌ عِنْدَ رَبِّهِمْ
 يُرْزَقُونَ، فَعَلَى مَنْ قَتَلَكُمْ لَعْنَةُ اللَّهِ وَالْمَلَائِكَةِ وَالنَّاسِ
 أَجْمَعِينَ، فَعَلَيْكُمْ سَلَامُ اللَّهِ وَرَحْمَتُهُ وَبَرَكَاتُهُ .

“Amani iwe juu ya Mtume wa Mwenyezi Mungu! Amani iwe juu ya Nabii wa Mwenyezi Mungu! Amani iwe juu ya Muhammad bin Abdillah! Amani iwe juu ya watu wa nyumba yake watakasifu! Amani iwe juu yenu enyi wahanga Waumini! Amani iwe juu yenu enyi watu wa nyumba ya imani na Tauhidi! Amani iwe juu yenu enyi watetezi wa dini ya Mwenyezi Mungu na watetezi wa Mtume Wake (s.a.w.w.)! Amani iwe juu yenu kwa subira mliyofanya, ni nzuri iliyoje nyumba ya baadaye!

“Nashahidilia kwamba hakika Mwenyezi Mungu amewachagueni kwa ajili ya dini Yake na amekuteuweni kwa ajili ya Mtume Wake. Na nashahidilia kwamba hakika

nyinyi mmepigana jihadi ukweli wa kupigana na mmeinusu dini ya Mwenyezi Mungu na sunnah ya Mtume Wake na mmejitema nafsi zenu kumlinda yeye. Na nashahidilia kwamba hakika nyinyi mmeuwawa juu ya njia ya Mtume wa Mwenyezi Mungu, Mwenyezi Mungu awalipeni niaba ya Nabii Wake, Uislamu na watu wake, malipo bora. Na atutambulishwe sehemu ya ridhaa Zake na eneo la heshima Yake pamoja na Manabii, Masiddiki, Mashahidi na Watu wema, na hao ndio marafiki wema. Nashahidilia kwamba hakika nyinyi ni kundi la Mwenyezi Mungu na kwamba mwenye kuwapigeni vita bila shaka amempiga vita Mwenyezi Mungu, na kwamba hakika nyinyi ni miongoni mwa waliokaribishwa waliofuzu, ambao wao ni hai mbele ya Mola wao Mlezi wakiruzukiwa. Laana ya Mwenyezi Mungu, malaika na watu wote iwe juu ya wale waliokuuweni. Amani ya Mwenyezi Mungu iwe juu yenu na pia rehema za Mwenyezi Mungu na Baraka zake.”

Tunakutakia Hijja yenye kukubaliwa,

juhudi zenye kuthaminiwa

na amali zenye kupokewa.

تَتَبَّنِي لَكُمْ حَجًّا مَقْبُولًا وَسَعْيًا مَشْكُورًا وَعَمَلًا مُتَقَبَّلًا

ORODHA YA VITABU VILIVYO CHAPISHWA NA AL-ITRAH FOUNDATION

1. Qur'an Al-Kariim - Tafsir Al-Kashif Juzuu ya kwanza mpaka Thelathini
2. Uharamisho wa Riba
3. Uharamisho wa uwongo Juzuu ya Kwanza
4. Uharamisho wa uwongo Juzuu ya Pili
5. Hekaya za Bahlul
6. Muhanga wa Imamu Husein (A.S.)
7. Mikingamo iliyomzunguka Imamu Ali (A.S.)
8. Hijab vazi Bora
9. Ukweli wa Shia Ithnaashariyyah
10. Madhambi Makuu
11. Mbingu imenikirimu
12. Abdallah Ibn Saba
13. Khadijatul Kubra
14. Utumwa
15. Umakini katika Swala
16. Misingi ya Maarifa

17. Kanuni za Ndoa na maadili ya Familia
18. Bilal wa Afrika
19. Abudharr
20. Usahihi wa Historia ya Uislamu na Waislamu
21. Salman Farsi
22. Ammar Yasir
23. Qur'an na Hadithi
24. Elimu ya Nafsi
25. Yajue Madhehebu ya Shia
26. Ukusanyaji na Uhifadhi wa Qur'an Tukufu
27. Al-Wahda
28. Ponyo kutoka katika Qur'an.
29. Uislamu mfumo kamili wa maisha ya kijamii
30. Mashukio ya Akhera
31. Al Amali
32. Dua Indal Ahlul Bayt
33. Udhuu kwa mujibu wa Kitabu na Sunna
34. Haki za wanawake katika Uislamu

35. Mwenyeezi Mungu na sifa zake
36. Kumswalia Mtume (s)
37. Nafasi za Ahlul Bayt (a.s)
38. Adhana
39. Upendo katika Ukristo na Uislamu
40. Tiba ya Maradhi ya Kimaadili
41. Maana ya laana na kutukana katika Qur'ani Tukufu
42. Kupaka juu ya khofu
43. Kukusanya swala mbili
44. Bismillah ni sehemu ya Qur'ani na husomwa kwa Jahara
45. Kuwaongoza vijana wa kizazi kipya
46. Kusujudu juu ya udongo
47. Kusherehekea Maulidi Ya Mtume (s)
48. Tarawehe
49. Malumbano baina ya Sunni na Shia
50. Kupunguza Swala safarini
51. Kufungua safarini

52. Umaasumu wa Manabii
53. Qur'an inatoa changamoto
54. as-Salaatu Khayrun Mina -'n Nawm
55. Uadilifu wa Masahaba
56. Dua e Kumayl
57. Sauti Ya Uadilifu wa Binadamu
58. Umaasumu wa Mitume - Faida Zake Na Lengo Lake
59. Umaasumu wa Mitume - Majibu Ya Aya Zenye Utata
60. Umaasumu wa Mitume - Umaasumu wa Mtume Muhammad (s)
61. Nahju'l-Balaghah - Juzuu ya Kwanza
62. Nahju'l-Balaghah - Juzuu ya Pili
63. Kuzuru Makaburi
64. Maswali Na Mishkili Eflu - Sehemu ya Kwanza
65. Maswali Na Mishkili Eflu - Sehemu ya Pili
66. Maswali Na Mishkili Eflu - Sehemu ya Tatu
67. Maswali Na Mishkili Eflu - Sehemu ya Nne
68. Maswali Na Mishkili Eflu - Sehemu ya Tano

69. Maswali Na Mishkili Eifu - Sehemu ya Sita
70. Tujifunze Misingi Ya Dini
71. Sala ni Nguzo ya Dini
72. Mikesha Ya Peshawar
73. Malezi Ya Mtoto Katika Uislamu
74. Ubora wa Imam 'Ali Juu ya Maswahaba Na Ushia ndio njia iliyonyooka
75. Hukumu za Kifikihi zinazowahusu Wanawake
76. Liqaa-u-Ilaah
77. Muhammad (s) Mtume wa Allah
78. Amani na Jihadi Katika Uislamu
79. Uislamu Ulienea Vipi?
80. Uadilifu, Amani na Mtume Muhammad (s)
81. Mitala na Ndoa za Mtume Muhammad (s)
82. Urejeo (al-Raja'a)
83. Mazingira
84. Utokezo (al - Badau)
85. Hukumu ya kujenga juu ya makaburi
86. Swala ya maiti na kumlilia maiti

87. Uislamu na Uwingi wa Dini
88. Mtoto mwema
89. Adabu za Sokoni
90. Johari za hekima kwa vijana
91. Maalimul Madrasatain Sehemu ya Kwanza
92. Maalimul Madrasatain Sehemu ya Pili
93. Maalimul Madrasatain Sehemu ya Tatu
94. Tawasali
95. Imam Mahdi katika Usunni na Ushia
96. Huduma ya Afya katika Uislamu
97. Sunan an-Nabii
98. Historia na sera ya viongozi wema (Sehemu ya Kwanza)
99. Shahiid Mfiadini
100. Ujumbe - Sehemu ya Kwanza
101. Ujumbe - Sehemu ya Pili
102. Ujumbe - Sehemu ya Tatu
103. Ujumbe - Sehemu ya Nne
104. Kumswalia Nabii (s.a.w)

105. Mariamu, Yesu na Ukristo kwa mtazamo wa Kiislamu
106. Hadithi ya Thaqaalain
107. Ukweli uliopotea sehemu ya Kwanza
108. Ukweli uliopotea sehemu ya Pili
109. Ukweli uliopotea sehemu ya Tatu
110. Ukweli uliopotea sehemu ya Nne
111. Ukweli uliopotea sehemu ya Tano
112. Safari ya kuifuata Nuru
113. Fatima al-Zahra
114. Myahudi wa Kimataifa
115. Kuanzia ndoa hadi kuwa Wazazi
116. Visa vya kweli sehemu ya Kwanza
117. Muhadhara wa Maulamaa
118. Mwanadamu na Mustakabali wake
119. Imam Ali ('a) Ndugu wa Mtume Muhammad (s) (Sehemu ya Kwanza)
120. Imam Ali ('a) Ndugu wa Mtume Muhammad (s) (Sehemu ya Pili)
121. Khairul Bariyyah

122. Uislamu na mafunzo ya kimalezi
123. Vijana ni Hazina ya Uislamu.
124. Yafaayo kijamii
125. Tabaruku
126. Taqiyya
127. Vikao vya furaha
128. Shia asema haya Sunni asema haya Wewe wasemaje?
129. Visa vya wachamungu
130. Falsafa ya Dini
131. Kuhuzunika na Kuomboleza - Azadari
132. Sunna katika Kitabu Fiqhi al-Sunnah
133. Kuonekana kwa Allah
134. Tabia njema kwa Mujibu wa Ahlul-Bayt (Sehemu ya Kwanza)
135. Tabia njema kwa Mujibu wa Ahlul-Bayt (Sehemu ya Pili)
136. Ushia ndani ya Usunni
137. Maswali na Majibu
138. Mafunzo ya hukmu za ibada

139. Ahlul Bayt ndani ya tafsiri za Kisunni No 1
140. Ahlul Bayt ndani ya tafsiri za Kisunni No 2
141. Ahlul Bayt ndani ya tafsiri za Kisunni No 3
142. Abu Huraira
143. Vipengee kadhaa katika Swala ya Jamaa na Msikiti.
144. Mazingatio kutoka katika Qur'an - Sehemu ya Kwanza
145. Mazingatio kutoka kaitka Qur'an - Sehemu ya Pili
146. Mazingatio kutoka katika Uislamu - Sehemu ya kwanza
147. Mazingatio kutoka katika Uislamu - Sehemu ya Pili
148. Qur'ani Tukufu – Pamoja na Tarjuma ya Kiswahili
149. Falsafa ya Mageuzi ya Imam Husein (a.s)
150. Amali za Mwezi Mtukufu wa Ramadhani
151. Elimu ya Tiba za Kiislamu - Matibabu ya Maimamu
152. Uislamu Safi
153. Majlisi za Imam Husein Majumbani
154. Uislam wa Shia
155. Amali za Makka

156. Amali za Madina
157. Asili ya Madhehebu katika Uislamu
158. Sira ya Imam Ali kuhusu Waasi
159. Ukweli uliofichika katika neno la Allah
160. Uislamu na Mifumo ya Uchumi
161. Umoja wa Kiislamu na Furaha
162. Mas'ala ya Kifiqhi
163. Jifunze kusoma Qur'ani
164. As-Sahifatul Kamilah as-Sajjadiyyah
165. Hayya 'Alaa Khayri'l-'Amal Katika Adhana
166. Ukweli kuhusu Funga ya Siku ya Ashura
167. Dua za Miezi Mitatu Mitukufu (Rajabu, Shaabani na Ramadhani)
168. Uadilifu katika Uislamu
169. Mahdi katika Sunna
170. Kazi na Bidii ni njia ya maendeleo
171. Abu Talib – Jabali Imara la Imani
172. Ujenzi na Utakaso wa Nafsi
173. Vijana na Matarajio ya Baadaye

174. Usalafi – Historia yake, maana yake na lengo lake
175. Ushia – Hoja na Majibu
176. Mateso ya Dhuria wa Mtume (saww)
177. Maombolezo – Msiba wa Bwana wa Mashahidi (a.s.)
178. Shahidi kwa Ajili ya Ubinadamu
179. Takwa
180. Amirul Muuminina ('as) na Makhalifa
181. Utawala na Uendeshaji katika Sera ya Imam Ali (a.s.)
182. Kuelewa Rehma ya Mwenyezi Mungu
183. Mtazamo kuhusu msuguano wa kimadhehebu
184. Upotoshaji Dhahiri katika Turathi (Hazina) ya Kiislamu
185. Nchi na Uraia – Haki na wajibu kwa Taifa
186. Mtazamo wa Ibn Taymiyyah kwa Imam Ali (a.s.)
187. Uongozi wa kidini – Maelekezo na utekelezaji wa Kijamii
188. Huduma ya Afya katika Uislamu
189. Historian a Sira za Viongozi Waongofu – Sehemu ya Pili
190. Uwazi baina ya Maslahi na Vikwazo

KOPI NNE ZIFUATAZO ZIMETAFSIRIWA KWA LUGHA KINYARWANDA

1. Amateka Na Aba'Khalifa
2. Nyuma yaho naje kuyoboka
3. Amavu n'amavuko by'ubushiya
4. Shiya na Hadithi

BACK COVER

Hija ni fursa ya Ummah wa Kiislamu kufikia hali ya Kiibrahim katika sekta ya kisiasa, kijamii, kitamaduni na kiroho. Mwenyezi Mungu amesema: *“Hakika Nyumba ya kwanza waliyowekewa watu ni ile iliyoko Makka yenye kubarikiwa na mwongozo kwa walimwengu.”* (Sura Aali Imran: 96).

Watu wamezoea zaidi kutimiza Hija yao kwa mwonekano wa nje katika siku za mkutano huu wa kimungu ambao huwaleta pamoja Waislamu toka pande zote za dunia bila kujali rangi zao, makabila wala mataifa na tamaduni za asili. Kwa kuwa Hija ni mkusanyiko wa kiroho wenye kulenga kuchanua na kustawi katika nyanja zote za maisha ya mwanadamu, ni vizuri mahujaji wetu wakaelewa kwamba ibada hii ni kama ibada nyingine katika kuilea jamii katika sekta zote za maisha ya kisiasa, kitamaduni na kijamii, na hivyo ni lazima tuitumie fursa hii kama Bunge la Waislamu la Kimataifa na Baraza Kuu la Waislamu duniani kupanga mikakati yao ya kiroho, kisiasa, kiuchumi, kijamii na kiutamaduni, ili kwamba lengo la Nabii Ibrahim (a.s.) lidhihirike ndani ya maisha yetu ya kila siku.

Ni juu ya Waislamu ambao hubeba ujumbe wa Mungu Mwenyezi, kufaidika kisiasa na kijamii na maudhui ya Hija, na kamwe wasiridhike na mwonekano wa nje. Lakini ni lazima watambue kwamba ibada ya kisiasa na kijamii ya Hija inaweza kupatikana iwapo tu tutatimiza na kufikia ibada ya kimaadili na kiroho.

Kimetolewa na kuchapishwa na:

Alitrah Foundation

S.L.P. 19701 Dar es Salaam, Tanzania
Simu: +255 22 2110640
Simu/Nukushi: +255 22 2127555
Barua Pepe: alitrah@yahoo.com
Tovuti: www.ibn-tv.com
Katika mtandao: www.alitrah.info